**3 JUNI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Thelathini na Nane – Tarehe 3 Juni, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati zifuatazo ziliwasishwa Mezani na:

**NABU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA K.n.y. WAZIRI WA FEDHA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Maswali na tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI; nimuite Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 484

**Uhitaji wa *X-Ray Machine* Vituo vya Afya**
**Nkende na Kibumaye - Tarime**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka huduma ya *x-ray machine* kwenye Vituo vya Afya Nkende na Kibumaye – Tarime?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Waziri, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI A MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa huduma za kiuchunguzi za mionzi katika vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi nchini. Katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi 2024/2025 jumla ya mashine za kidijiti za *x–ray* 318 zimenunuliwa na kufungwa katika vituo vya kutolea huduma za afya kote nchini. Aidha, Halmashauri ya Mji Tarime imepokea mashine mbili za *x–ray* na kuzifunga katika Hospitali ya Nyamwaga na Kituo cha Afya cha Sirare.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya kununua mashine za *x–ray* na kuzipeleka kwenye vituo vya afya vitakavyokuwa vimekamilisha ujenzi wa

majengo ya huduma za mionzi kote nchini vikiwemo Vituo vya Afya vya Nkende na Kibumaye katika Halmashauri ya Mji wa Tarime.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni takribani miezi miwili sasa *x-ray machine* iliyopo katika Hospitali ya Mji wa Tarime haifanyi kazi kabisa na wamekuwa wakiifanyia ukarabati mara kwa mara inaonekana imechoka na kwa sababu Halmashauri ya Mji ya Tarime inatoa huduma hii siyo tu kwa wakazi wa Mji wa Tarime, bali wa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti na Rorya.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja sasa ya kupeleka *x-ray machine* walau mbili ambazo zinafanya kazi na mpya ziweze kuwahudumia wananchi hawa, ili moja ikiharibika nyingine iweze kufanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, pamoja na majengo mazuri ambayo tuna-*appreciate* mmetujengea Hospitali wa Tarime likiwepo lile la *emergency*, lakini bado kumekuwa na changamoto ya vifaa vingine vya kuweza kusaidia kutoa huduma bora. Kwa mfano mashine iliyopo ambayo ni *washing machine* ya kuweza kufua mashuka ya wagonjwa imeharibika na ni ya muda mrefu.

Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka sasa wa kupeleka *washing machine* mpya ya kuweza kutoa huduma bora kwa wananchi wale wa Mji wa Tarime na wengine wanaokuja kupata huduma pale?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI A MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika dhamira muhimu sana ya Serikali ni kuhakikisha vituo vya

huduma za afya, hospitali za halmashauri zinapima magonjwa kwa kutumia vifaa vya kisasa. Moja ya vifaa hivyo ni mashine za *x-ray*, na ndiyo maana Serikali imenunua zaidi ya *x-ray* 318 za kidijiti katika miaka hii miwili na zimepelekwa kwenye vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusuiana na mashine ya *x-ray* katika Hospitali ya Mji wa Tarime kuharibika, ni suala la dharura. Natumia nafasi hii kutoa maelekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Tarime, Mganga Mkuu wa Halmashauri na Mganga Mkuu wa Mkoa kufanya tathmini ya haraka kuona namna gani *x-ray* mashine hiyo inatengenezwa na kuanza kutoa huduma mapema iwezekanavyo na ikiwa mashine hiyo haitengenezeki walete taarifa mapema ili tuweze kuwasiliana na Bohari ya Dawa *(MSD)* na kupata mashine nyingine ili kuhakikisha kwamba tunarejesha huduma za *x-ray*, katika hospitali hiyo ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, vifaa tiba vinanunuliwa na Serikali Kuu lakini pia kuna vifaa ambavyo vinanunuliwa na halmashauri yenyewe ikiwemo mashine za kufulia. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kutoa maelekezo kwa Mkurugenzi pia kuona uwezekano wa kununua mashine ambayo ipo ndani ya uwezo wa mapato ya ndani ya halmashauri ili huduma hizo ziweze kurejea katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Tarime. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sylivia Sigula.

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nkasi, Kata ya Kate, tunamshukuru Mheshimiwa Rais ametujengea kituo cha afya na vifaa vimeenda vya kisasa, lakini hakuna wataalam wa ku-*operate* vifaa hivyo na hospitali hiyo haifanyi kazi.

Je, ni lini mtapeleka wataalam ili Kituo cha Afya cha Kate kiweze kufanya kazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI A MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ajira zote ambazo zimekuwa zikitolewa na Serikali ikiwemo ajira 34,720 za watumishi wa sekta ya afya ambazo zimetolewa katika kipindi hiki cha miaka minne. Moja ya wataalam ambao wamekuwa wakiajiriwa ni wataalam wa mifumo, vifaa tiba, *x-ray, ultrasound* na wengine kama maabara na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Sigula kwamba Serikali inatambua baadhi ya maeneo bado kuna upungufu wa wataalam hao, lakini tumeshatoa maelekezo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri kufanya *reallocation* ya watumishi ndani ya mkoa na ndani ya halmashauri ili vile vituo ambavyo vina upungufu mkubwa zaidi vianze kutoa huduma za msingi wakati vibali vya ajira vikiendelea kutolewa.

Mheshimiwa Mbunge kwa hiyo, nikuhakikishie tu kwamba tutafuatilia hilo na kuhakikisha wataalam hao wanapelekwa kwa ajili ya kuanza kutoa huduma hizo muhimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Kituo cha Afya Kiponzelo kilichopo katika Jimbo la Kalenga, Kata ya Maboga, kinahudumia zaidi ya vijiji vitano na kuna changamoto ya *x-ray* ambayo ni mbovu kwa muda mrefu.

Je, hamuoni sasa kuna haja ya kupeleka hizo *x-ray* mashine ambazo mmezitoa ziende katika kituo cha afya hicho ili kiwasaidie wananchi wa pale?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI A MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha 2024/2025 ambao tunauhitimisha, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 63.7 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba zikiwemo *digital x-rays* na tayari tumeshaainisha vituo vya afya ambavyo vina ukosefu wa mashine hizo kikiwemo Kituo cha Afya cha Kiponzelo ambacho tulishapata taarifa Mheshimiwa ameuliza zaidi ya mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaingiza kwenye orodha hiyo na tunaamini wakati wowote manunuzi yakikamilika, tutapeleka mashine ya *x-ray* katika Kituo cha Afya cha Kiponzelo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na shughuli za kiuchumi kule Tarime, uchimbaji, pamoja na shughuli za bodaboda kuna ajali nyingi sana Tarime Vijijini na Wilaya ya Tarime kwa ujumla. Ni lini mpango wa Serikali kupeleka *x-ray* mashine katika Kituo cha Afya Bumela, Sungusungu, Kerende, Magoma pamoja na Mtana ili watu wangu waweze kupata huduma za *x-ray machine*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kumekuwa na ongezeko kubwa la ajali na hususan ajali za pikipiki maarufu bodaboda ambazo mara nyingi sana majeruhi wanahitaji kupata huduma za *x-ray* kama Mheshimiwa Waitara alivyosema na ndio maana Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba zikiwemo mashine za *x-ray*. Tayari katika Halmashauri ya Tarime Vijijini wamepata *x-ray* na tunaendelea na taratibu za manununzi kwa ajili ya kupeleka *x-ray* katika vituo ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge vituo ulivyovitaja tutakwenda

kwa awamu kuhakikisha kwamba tunapeleka mashine za *x-ray*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Jafari Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi. Halmashauri ya Rorya ina vituo vya afya vinne kwa maana ya Utegi, Nyamagaro, Kinesi pamoja na Rabour, lakini vituo vya afya vyote hivi vinne havina Jengo la Mionzi *(x-ray)* na wala hawana mashine za *x-ray*. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo hili na ununuzi wa kifaa hiki cha *x-ray?*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ujenzi wa majengo ya *x-ray* katika vituo vyetu vya afya yanafanyika kwa vyanzo mbalimbali vya mapato zikiwemo fedha za mapato ya ndani pia fedha kutoka Serikali Kuu.

Kwa hiyo, ninaomba kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Chege kwamba Serikali inatambua lazima tuwe na majengo hayo ya *x-ray* na nitumie nafasi hii kumuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Rorya kwanza kutenga fedha kwenye mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza ujenzi wa majengo ya *x-ray* angalau kwenye vituo viwili vya afya wakati Serikali Kuu ikitafuta fedha kwa ajili ya kwenda kujenga majengo hayo. Nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge lazima Serikali itakwenda kujenga majengo hayo na pia kupeleka mashine za *x-ray* ili vituo hivyo viwe na huduma zote muhimu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Nimuite sasa Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo aweze kuuliza swali lake. Kwa niaba yake litauliwa na Mheshimiwa Mama Ishengoma.

Na. 485

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Chifutuka**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA K.n.y. MHE. KENNETH E. NOLLO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Chifutuka – Bahi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya Chifutuka kilipokea shilingi milioni 500 mwaka 2017/2018 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la maabara, jengo la upasuaji, jengo la wazazi, chumba cha kuhifadhia maiti na nyumba ya mtumishi. Ujenzi wa majengo hayo umekamilika na majengo yanatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya kukamilisha miundombinu inayopungua katika Kituo cha Afya cha Chifutuka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa majengo ya Kituo cha Afya cha Magubike ikiwemo ujenzi wa wodi ya wanaume pamoja na chumba cha watoto njiti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, ni lini Serikali itapeleka wafanyakazi wa kutosha wa afya kwenye vituo vya afya Mkoani Morogoro? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Mbunge mama yangu Dkt. Christina Ishengoma ameuliza mara kadhaa kuhusiana na ujenzi wa wodi hizo, wodi ya wanaume pia chumba wodi ya watoto njiti katika Kituo cha Afya cha Magubike. Tayari tulishakubaliana Ofisi ya Rais – TAMISEMI kuingiza Kituo cha Afya cha Magubike kwenye vituo vya kimkakati ambavyo fedha kupitia Mfuko wa Benki ya Dunia utakwenda kujenga miundombinu hiyo inayosalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tayari inaendelea na taratibu kwa ajili ya kuanza ujenzi wa majengo hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Selemani Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi. Kwanza niishukuru na kuipongeza Serikali kwa kujenga miundombinu ya vituo vya afya na Hospitali ya Wilaya ya Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Tanganyika ina mtaalam mmoja tu wa mionzi ambaye anafaya kazi kwenye vituo vya afya na hospitali ya wilaya. Ni lini mtampeleka msaidizi wake ili aweze kufanya kazi vizuri kwa wananchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni

kweli kwamba Hospitali ya Halmashauri ya Tanganyika ina mtaalam mmoja wa *x-ray* na tunafahamu kwamba tunahitaji kuwa na wataalam angalau wawili au watatu ili kuwa na uhakika na huduma za afya pindi yule mtaalam mmoja anapopata dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali imeendelea kuajiri wataalam hao, lakini kimsingi wataalam hao wapo wachache kwenye soko na mpango wa Serikali tumeendelea kufanya mafunzo ya muda mfupi kwa wataalam wa sekta ya afya waliopo kazini ili waende kuziba pengo la wataalam wa *x-ray* katika halmashauri zetu. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Kakoso kwamba baada ya wataalam hao waliopo kwenye kozi za muda mfupi kuhitimu tutahakikihsa tunaleta wataalam katika Hospitali ya Tanganyika ili kuondoa pengo la watumishi katika sekta hiyo.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Mohamed Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, mwaka 2022/2023 Serikali ilikuwa na mpango wa kujenga vituo vya afya kwenye kata zote za mipakani. Moja ya kata hizo ilikuwa ni Kata ya Mpendo, Jangalo, Lahoda na Kinyamshindo kwenye Jimbo la Chemba. Ninataka kujua huo mkakati uliishia wapi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi wa mwaka 2007 – 2017 ambao ulikuwa unaelekeza ujenzi wa kituo cha afya kwenye kila kata na ujenzi wa afya kwenye kila kijiji, lakini Serikali ilifanya tathmini na kuona uhalisia wa utekelezaji wa mpango huo na tija ya kuwa na mpango huo Serikali ikaja na mpango mwingine mbadala, kwamba badala ya kujenga kituo cha afya kwenye kila kata tutajenga vituo vya afya kwenye kata za kimkakati ambazo

zitakidhi vigezo vya idadi ya watu angalau 15,000 na umbali kutoka kituo cha afya cha jirani zaidi angalau kilometa tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Monni kwamba vile vituo vya afya ambavyo vinakidhi vigezo vya kata za kimkakati Serikali itaendelea kuandaa mpango kwa ajili ya kwenda kujenga vituo hivyo vya afya, vile ambavyo havikidhi vigezo vitapata huduma katika maeneo ya karibu na vituo vingine ambavyo vitakuwa na vituo vya afya.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Japhet Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ni lini Serikali itapeleka fedha kukamilisha Vituo vya Afya vya Idiwili, Luanda na Isangu, Vwawa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Luanda, Kisangu na hicho kingine ambacho Mheshimiwa Hasunga amekitaja ni miongoni mwa vituo vya afya ambavyo Serikali imeshapeleka fedha na kuanza ujenzi wa miundombinu awamu ya kwanza. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ujenzi wa vituo hivi vya afya unafanyika kwa awamu. Tulianza na awamu ya kwanza ya majengo ya *OPD,* maabara, kichomea taka na mengine ili huduma za msingi zianze lakini tutakwenda awamu ya pili kwa ajili ya kujenga majengo yanayopungua ikiwemo wodi na majengo mengine.

Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Hasunga kwamba Serikali inaendelea kutekeleza mpango huo na tutafika kukamilisha majengo hayo katika Jimbo la Vwawa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Christina Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kuna Hospitali ya Wilaya pale Iselamagazi lakini kuna baadhi ya majengo hayajakamilika ikiwepo wodi za wanawake na wanaume. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kukamilisha majengo hayo?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumefanya ziara katika Hospitali ya Halmashauri ya Shinyanga. Yapo majengo ambayo yamekamilika, lakini yapo majengo ambayo bado hayajakamilika na kuna majengo ambayo yanahitajika. Serikali ilishatekeleza awamu ya kwanza ya ujenzi wa majengo yale kwa kupeleka zaidi ya shiingi bilioni mbili. Tunaendelea na mpango mwingine kwa ajili ya kukamilisha majengo ambayo hayajakamilika.

Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Christina kwamba Serikali tayari imeweka mpango kwa ajili ya kwenda kukamilisha majengo hayo mengine ili hospitali ile iwe na majengo yote muhimu na itoe huduma ambazo zinatarajiwa kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuniona. Nimekuwa nikikumbusha sana Serikali juu ya kujenga kituo cha afya katika Kata ya Kivavi na Serikali imeniahidi kwamba tutapewa kituo kimoja katika Halmashauri ya Mji ya Makambako.

Je, ni lini sasa tutapatiwa fedha hizo za kujenga kituo cha afya katika Kata ya Kivavi?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makambako mara kwa mara amefuatilia sana kuhusiana na uhitaji wa kujenga kituo cha afya katika Kata ya Kivavi na kwa bahati nzuri tayari Serikali imeshaweka kata hiyo kwenye mpango wa Benki ya Dunia kwa ajili ya kwenda kujenga kituo hicho cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Deo Sanga kwamba tunasubiri tu suala la utaratibu wa kifedha na mara taratibu zikikamilika tutaanza ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Kivavi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Mageni.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru, Kituo cha Afya cha Nyambiti katika Jimbo la Sumve ni kituo cha afya cha kimkakati kwa sababu kipo Makao Makuu ya Jimbo. Pia ni kituo cha afya ambacho hakina jengo la upasuaji na wananchi walifanya juhudi kubwa kulijenga na tukapata na mfadhili akatuletea mpaka vifaa, lakini vifaa hivyo vinaharibika kwa sababu ya kukosekana kwa jengo.

Je, ni lini Serikali itatuunga mkono sisi wananchi wa Sumve katika kujenga jengo la upasuaji katika Kituo cha Afya cha Nyambiti?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na suala hili. Ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Nyambiti kina upungufu wa majengo na tulishamuelekeza

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kwimba kuleta taarifa ya fedha zinazohitajika kujenga jengo la upasuaji, ili huduma za upasuaji zianze katika Kituo cha Afya cha Nyambiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba nitumie nafasi hii kumkumbusha Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kwimba kuleta mapema iwezekanavyo makadirio ya mahitaji ya fedha kwa ajili ya kujenga jengo la upasuaji ili vifaa hivyo vianze kutumika na wananchi wa Kwimba wapate huduma ambazo zinastahili.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea kwa swali linalofuata, ninamuita Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 486

**Uvunaji wa Maji ya Mvua katika Shule zote Nchini**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza kujenga mifumo ya uvunaji maji ya mvua katika shule zote nchini?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, sensa ya elimu msingi ya mwaka 2024 inaonesha kuwa shule 5,311 za sekondari zina vyanzo vya maji vya uhakika ambapo shule zenye maji ya bomba ni 2,960, visima ni shule 1,217 na wanaovuna maji ya mvua ni shule 1,134. Aidha, shule 20,509 za msingi zina vyanzo vya maji vya uhakika ambapo shule zenye maji ya bomba ni 10,965, visima shule 4,966 na shule zinazovuna maji ya mvua ni 4,578.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya Serikali ya kufikisha huduma za maji safi na salama katika shule za msingi na sekondari nchini ni pamoja na ujenzi wa shule mpya au miundombinu ya vyoo kujumuisha fedha za ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa itaendelea kuweka mikakati mbalimbali ya kuhakikisha shule zinakuwa na huduma ya maji safi na salama, kwa kuzingatia vyanzo vya maji vya eneo husika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Fiyao.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza niseme wazi, natambua jitihada kubwa ambazo zinafanywa na Serikali kuhakikisha kwamba katika kila shule kunakuwa na maji, lakini bado kuna changamoto kwa baadhi ya shule, mfano ni shule ya sekondari Ileje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hii ina wanafunzi kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha sita, imekuwa ikikumbwa na uhaba mkubwa wa maji, changamoto hii inapelekea wanafunzi kwenda kutafuta maji kwenye mito ili kuweza kukidhi mahitaji kwenye shule hii jambo ambalo linahatarisha usalama wa wanafunzi hususani wanafunzi wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba shule hii inapata maji ya uhakika ili wanafunzi waweze kuepukana na changamoto hii.

Swali langu namba mbili, ninataka kujua mpango wa Serikali ni upi kuhakikisha mnapeleka fedha katika Shule ya Msingi Ilanga iliyoko Kata ya Mlale, Wilaya ya Ileje, shule ambayo iliezuliwa na

mvua na kupelekea majengo matatu tu, kuna madarasa matatu ambayo yanatumiwa na wanafunzi kuanzia darasa la awali mpaka darasa la saba.

Je, ni lini Serikali mtapeleka fedha ili wanafunzi waendelee kusoma kama walivyokuwa wanasoma hapo awali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama alivyosema, moja ya mikakati ya Serikali ni kuhakikisha kwamba shule zetu zote zinakuwa na maji safi na salama ili kuwawezesha wanafunzi kuwa na afya njema, lakini pia kusoma katika mazingira tulivu.

Kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kumuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ileje, lakini pia Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya wapite katika shule hiyo, wafanye tathmini ya uwezekano wa kupata maji, waangalie uwezekano wa vyanzo vya maji ambavyo vinaweza vikapatikana kwa haraka, pia wawasiliane na Mamlaka za Maji *RUWASA* katika eneo hilo ili kufanya utaratibu wa haraka wa kupeleka maji katika shule ya sekondari ya Ileje ili watoto wasome katika mazingira bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusiana na madarasa ambayo yameezuliwa, ni wajibu wa halmashauri kwanza kutumia mapato ya ndani kufanya marekebisho madogo madogo kwenye madarasa ili watoto waendelee na masomo, lakini kama fedha hiyo haipo ndani ya uwezo wa halmashauri, namuelekeza Mkurugenzi alete taarifa Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tuweze kuona namna nzuri ya kupata fedha mapema na kwenda kurekebisha madarasa hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Sasa nimwite Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 487

**Ukarabati wa Mabweni ya Wasichana Kilindi *(Kilindi Girls')***

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakarabati mabweni ya wasichana ya kidato cha tano na sita katika Shule za Kilindi na Mlongwema?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitoa fedha za ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali katika Shule za Wasichana Kilindi na Mlongwema kwa ajili ya kuboresha mazingara ya ujifunzaji na ufundishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025 Serikali imetoa shilingi milioni 312 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa manne, bweni moja, umaliziaji wa bweni moja na bwalo moja katika Shule ya Wasichana Kilindi. Aidha, bweni lililokamilishwa ni ambalo lilikuwa chakavu kutokana na kuanza kutumika kabla ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imetoa shilingi milioni 578.5 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili, madarasa 11, matundu 17 ya vyoo na ukarabati wa mfumo wa maji wa bweni katika Shule ya Sekondari Mlongwema. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati au ujenzi wa

miundombinu katika maeneo mbalimbali katika shule za kidato cha tano na sita ili kuboresha mazingira ya elimu nchini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Husna Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati natembelea hizo shule hali ilikuwa ni mbaya na hairidhishi, hali siyo nzuri kwa ujumla. Mabweni yapo kwenye hali mbaya. Je, Serikali ina mkakati madhubuti na mahsusi kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa mabweni katika shule hizi mbili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu ujenzi unafanyika kutokana na upatikanaji wa fedha, je, kuna mpango gani wa kukarabati majengo haya ili kuwasaidia watoto wanaosoma pale angalau kuwa katika mazingira yanayovutia? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Serikali imeweka mpango mkakati kwanza kwa kuainisha maeneo au shule ambazo zina miundombinu chakavu yakiwemo mabweni, mabwalo na madarasa na Serikali imekuwa ikitenga fedha katika kila bajeti kupitia programu mbalimbali ikiwemo *SEQUIP* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mabweni na miundombinu mingine inajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Sekiboko kwamba kwa hali ya mabweni katika hizi Shule za Sekondari ya Kilindi na Mlongwema, Serikali itaweka kipaumbele kutafuta fedha mapema iwezekanavyo na kwenda kukarabati mabweni hayo ili wanafunzi waweze kuishi katika

mabweni bora zaidi na kuweza kupata elimu katika mazingira mazuri zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo katika Shule ya Sekondari ya Kilindi kutokuwa na mabweni, kumekuwa na shida ya mabweni katika Shule ya Sekondari ya Ikuti Wilaya ya Rungwe, wananchi na halmashauri imejitahidi sana kujenga na kufikia ngazi ya *lintel*, ni lini Serikali mtaona sasa ni wajibu wenu kupeleka fedha ili kuweza kumalizia mabweni yale? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi kila mwaka wa fedha kwa ajili ya kukamilisha mabweni na miundombinu mingine ya shule, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe pia ni moja ya shule ambazo zimepelekewa fedha nyingi sana kwa ajili ya ujenzi wa mabweni, mabwalo, madarasa na shule nyingine mpya. Kwa hiyo, Serikali imekuwa ikitimiza wajibu huo kwa dhati kabisa na ninakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwanza niwapongeze wananchi wa Rungwe kwa kuchangia nguvu zao katika Shule ya Sekondari ya Ikuti kwa ajili ya kujenga mabweni, ni jambo zuri na Serikali tayari imechukua *stock* ya maboma hayo kwa ajili ya kutafuta fedha kwa ajili ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kupeleka fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunakamilisha mabweni haya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya tumalizie na swali la mwisho, nimuite sasa Mheshimiwa George Natany Malima, aweze kuuliza swali lake.

Na. 488

**Ujenzi wa Barabara za Lami Mji wa Mpwapwa**

**MHE. GEORGE N. MALIMA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami unaoendelea katika Mji wa Mpwapwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza ujenzi wa barabara kwa tabaka la lami na uwekaji wa taa 41 katika Mji wa Mpwapwa kwa mikataba miwili yenye thamani ya shilingi bilioni 1.11 ambapo kilometa tatu zinajengwa. Mradi huo umefikia 70% na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2025.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuihudumia miundombinu ya barabara na madaraja ya Mji wa Mpwapwa kwa kuijenga, kuikarabati na kuifanyia matengenezo kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malima.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara kwa tabaka la lami katika Mji wa Mpwapwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa

Awamu ya Tano. Ahadi ilikuwa ni kujenga kilometa 10 za tabaka la lami, lakini sasa hivi ujenzi unaoendelea ni wa kilometa tatu tu.

Ni nini tamko la Serikali kwa kilometa saba zilizobaki? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tamko la Serikali ni kwamba tayari imeanza kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano na kujenga kilometa hizo 10 za barabara ya lami katika Mji wa Mpwapwa na ndiyo maana tumeanza na kilometa tatu, tutaendelea kwa awamu katika kila mwaka wa bajeti kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Felista Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Barabara ya Kisawio - Mamandizi ambayo inaelekea Kituo cha Afya cha Uru Kusini kilichojengwa kwa gharama kubwa sana za Serikali, haipitiki na inapelekea wananchi wagonjwa kubebwa kwa machela. Ni lini Serikali itajenga barabara hii kwa kuwa nimeuliza mara kwa mara na kujibiwa inajengwa, ni lini Serikali itaijenga barabara hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya vipaumbele vya Serikali ni kuhakikisha maeneo yote ya huduma za kijamii yanakuwa na barabara bora zinazopitika na hususani maeneo ya huduma za afya lazima tuweke kipaumbele kuhakikisha kwamba barabara zinapitika, kwa sababu ni maeneo

ambayo yanakuwa na magari ya wagonjwa na wagonjwa mahututi wanahitaji kuwahishwa kwenye vituo vingine vya rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa ni kweli ameuliza mara kadhaa na Serikali tumempa *commitment,* taratibu zinazoendelea ndani ya Serikali ni kufanya tathmini ya gharama ya fedha zinazohitajika kwa ajili ya barabara hiyo na kupeleka fedha mapema iwezekanavyo kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali hii ni sikivu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, itakwenda kutekeleza ujenzi wa barabara hiyo ili wananchi wa Kituo cha Afya cha Uru Kusini wapate huduma bora zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tuhamie Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Nimuite sasa Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, aweze kuuliza swali lake.

Na. 489

**Kada Tofauti na Ualimu Kupewa Madaraja Mserereko**

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kada nyingine wanapewa madaraja mserereko kama ilivyo kada ya ualimu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa niaba yake Naibu Waziri Mheshimiwa Deus Clement Sangu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 6(1)(b) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298 jukumu la kuwapandisha vyeo watumishi ni la mwajiri husika. Jukumu hili hutekelezwa baada ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kutoa mwongozo kuwataka waajiri kuandaa na kuwasilisha ikama na bajeti ya mwaka husika wa fedha na ofisi kuridhia utekekelezaji wa bajeti hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imewapandisha vyeo kwa mserereko watumishi wasio walimu 1,284. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetoa mwongozo unaohusu upandishaji vyeo na ubadilishaji kada ikiwemo na kwa watumishi waliocheleweshwa kupandishwa vyeo. Hivyo, nitoe wito kwa waajiri wote katika sekta ya umma kutekeleza kwa wakati mwongozo huo ili kuepusha malalamiko kwa watumishi wa umma wenye changamoto za kupandishwa vyeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa kazi kubwa waliyofanya kupandisha madaraja ya watumishi Tanzania, lakini pamoja na pongezi hizo ninayo maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, je, Serikali ina mkakati gani kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miongozo hii wanayoituma kwa waajiri ya upandishwaji madaraja pamoja na ubadilishaji wa kada ili yafanyike kwa wakati kupunguza malalamiko kwa watumishi?

Swali la pili, napongeza sana *speed* iliyopo ya kupandisha madaraja kwa mfumo wa mserereko hasa walimu, kwa vile kada

zingine wengi wanakwenda kustaafu na kumekuwa na malalamiko mengi miongoni mwa kada zisizo za ualimu.

Je, Serikali haioni kuna haja ya kuweka *speed* ile ile ya kupandisha madaraja kwa mserereko kwa kada nyingine? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza ninapokea pongezi za Serikali alizozitoa Mheshimiwa Dkt. Alice, kwa namna Serikali ilivyoshughulikia upandishaji vyeo wa watumishi wa umma hasa katika kipindi hiki cha uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mkakati wa mwongozo tulioutoa mwezi Aprili, 2024 kuwataka waajiri wote katika sekta ya umma walete orodha ya watumishi wale wanaostahili na wenye sifa ya kupandishwa vyeo ifikapo mwishoni mwa mwezi Mei mwaka huu. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili tutalifuatilia na ninashukuru sana waajiri wengi wameweza ku-*respond* na kuleta hao wanaostahili kupandishwa vyeo na nitumie Bunge hili kutoa rai kwa wale ambao bado hawajatimiza ndani ya wiki moja wakamilishe ili tutakapoanza mwaka mpya wa fedha watumishi wote ukiachia walimu na ambao siyo walimu waweze kupandishwa vyeo kwa kadri ambavyo tumepanga bajeti ya takribani shilingi bilioni 207.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *speed* ya kupandisha kada nyingine nikutoe shaka Mheshimiwa Dkt. Alice, haya ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kama nilivyosema bajeti ipo na azma yake ni kwamba tutakapofika mwaka mpya wa fedha 2025/2026 kusiwe na malalamiko ya watu waliolimbikizwa madaraja, wawe tumeondoa ili tuanze ukurasa mpya katika mwaka mpya wa fedha, nakushukuru.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Nimuite sasa Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, aulize swali lake.

Na. 490

**Kupeleka Ajira kwenye Ngazi ya Halmashauri**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza: -

Je, kwa nini Serikali isipeleke ajira kwenye ngazi ya halmashauri ili kuweka uwiano wa nafasi katika kila jimbo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2008, Toleo la 2 Aya ya 4.2, nafasi za ajira hutolewa kwa ushindani na kwa kuzingatia sifa stahiki kwa mujibu wa Miundo ya Maendeleo ya Utumishi ya kada husika. Vilevile mgawanyo wa nafasi za ajira mpya katika utumishi wa umma huzingatia mahitaji ya watumishi yaliyoainishwa na mwajiri na kisha kuidhinishwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika ikama na bajeti kwa mwaka wa fedha husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Ofisi ya Rais, Utumishi kuidhinisha kibali cha ajira mpya, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma huendesha usaili wa kuwapata watahiniwa stahiki na kisha kuwapangia katika maeneo yenye uhitaji ili kujaza nafasi wazi kulingana na mahitaji ya mwajiri kwa mwaka husika. Kwa msingi huo nafasi za ajira mpya haziwezi kutolewa kwa uwiano sawa kwa kila jimbo, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa Mbulu Vijijini kuna zaidi ya nafasi 220 hazina kabisa watumishi na ufanyaji wa kazi umekuwa mgumu. Je, Serikali imejipangaje sasa kusaidia Jimbo la Mbulu na Mbulu Vijijini na Halmashauri ya Mbulu ili kuwa na utendaji mzuri wa kazi ndani ya jimbo hilo? *(Makofi)*

Swali la pili, natambua majibu yako ya Sera ya mwaka 2008, sasa hivi kuna tatizo kubwa la ajira katika maeneo yetu na hasa vijana wengi wamekuwa wakitafuta hizi ajira na zimeshakuwa kama bomu.

Je, ni mpango gani wa Serikali kutatua eneo hili ili kusaidia vijana wengi kupata ajira kama nilivyouliza? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, nimpongeze sana Mheshimiwa Flatei, amekuwa mstari wa mbele kufuatilia sana suala la ajira na watumishi kwa ujumla katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimjibu maswali yake yote mawili kwa ujumla, kwanza naomba Mheshimiwa Flatei, nikuhakikishie Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeonesha mfano dhahiri wa kutoa kipaumbele katika ajira kwa vijana. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alitoa kibali cha ajira 47,404. Haitoshi mwaka 2024/2025 alitoa kibali cha ajira 45,000 lakini pia mwaka wa fedha ujao na kwenye bajeti yetu ya Ofisi ya Rais,

Utumishi mlitupitishia kibali cha ajira 41,500. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais ameonesha kwa nia ya dhati kwamba anawapenda vijana wa Kitanzania na kwa kadri fedha zinavyopatikana na bajeti amekuwa akitoa tu vibali vya ajira, kwa kweli tumpongeze Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Flatei kuwa katika ajira hizi nilizotaja zote, tayari kuna ikama imepangwa kwa ajili ya watumishi kwenda kwenye jimbo lake. Kwa hiyo kama pia Mkurugenzi alikuwa hajawasilisha maombi kwa mwaka ujao wa fedha aandae maombi na alete Ofisi ya Rais, Utumishi ili tuweze kumpa kipaumbele.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Nishati, nimuite sasa Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, aulize swali lake.

Na. 491

**Kusambaza Umeme wa *REA* Arumeru Mashariki**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha kusambaza umeme wa *REA* kwenye vitongoji 37 ambavyo vipo gizani katika Jimbo la Arumeru Mashariki?

**MWENYEKITI:** Kwa niaba ya Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri Judith Salvio Kapinga.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Arumeru Mashariki lina jumla ya vitongoji 330 ambapo kati ya hivyo, vitongoji 284 vimepatiwa umeme, 17 vipo katika hatua ya utekelezaji kupitia mradi wa ujazilizi na mradi wa kupeleka umeme katika vitongoji Awamu ya Pili A. Vitongoji 29 zabuni imetangazwa ili kupata wakandarasi wa

kutekeleza miradi kupitia mradi wa kupeleka umeme vitongojini Awamu ya Pili B.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa miradi hii kutawezesha vitongoji vyote vya Jimbo la Arumeru Mashariki, kufikiwa na umeme, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali na nichukue nafasi hii kwa kweli kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita na kuipongeza kwa kazi nzuri sana ambayo inafanya katika kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanakuwa nuruni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za Mashariki mwa Jimbo langu kwa maana ya King'ori, Leguruki, Maruvango, Ngarenanyuki na Ngabobo zinapata maji kutoka msitu wa Mlima Meru lakini maji haya yana *fluoride* nyingi. Taasisi ya *KOICA* imejitolea kutuletea mitambo ya kusafisha maji haya na kuhakikisha kwamba yanakuwa *free of fluoride*.

Je, ni lini Serikali itatupelekea umeme wa uhakika kwenye Kitongoji cha Seneto eneo ambalo *KOICA* wameweka hii mitambo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge na nikiri Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia jambo hili kwa muda sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tulishamuelekeza Meneja wa Arumeru Mashariki na tayari wameshatenga fedha kwa ajili ya mwaka wa ujao wa fedha kwa ajili ya kupeleka umeme wa uhakika

katika Kitongoji hiki cha Seneto, Kata ya Leguruki kwa ajili ya kutibu *fluoride* na kuondoa *fluoride* katika maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge suala hili tunaenda kulitekeleza na mimi kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri nimkumbushe Meneja wa Arumeru Mashariki ahakikishe kuanzia mwezi wa saba jambo hili linatekelezwa ili wananchi wa Arumeru Mashariki hususan katika maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge wapate maji ya uhakika ambayo yanaondolewa *fluoride* katika mitambo ile. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Je, ni lini Serikali itawaunganishia umeme wananchi wa Kitongoji cha Orera katika Kijiji cha Mweka, Kata ya Kibosho Mashariki? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, katika Jimbo hili la Moshi Vijijini yupo mkandarasi ambaye anatekeleza miradi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji katika vile vitongoji 15 vya kila Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitongoji hiki cha Orera ambacho Mheshimiwa Mbunge amesema na chenyewe kipo katika mradi huu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mkandarasi ambaye anaitwa *Silex Engineering* yupo *site* anaendelea na kazi ya upimaji. Kwa hiyo, niwahakikishie wananchi hawa wa Orera wataenda kupata umeme hivi karibuni kwa sababu tayari mkandarasi yupo *site*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Ally Makoa.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ninapenda kujua; ni lini sasa watatupelekea umeme kwenye Mitaa ya Mongoroma, Chandimo na Hachwi? Hii mitaa na yenyewe ina haki ya kupata umeme tafadhali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsantena nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake. Ni kweli kuna mitaa ya Kondoa Mjini ambayo ilikuwa haina umeme na tulishapunguza baadhi ya mitaa imebaki hii mitaa mitatu ambayo Mheshimiwa Mbunge amesema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kuwa tunaendelea kutenga fedha katika bajeti ya *TANESCO* ili kwa mwaka ujao wa fedha tuendelee kupunguza na kwenda kuweka umeme katika mitaa hii mitatu. Tutaenda kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha na bajeti ambayo imetengwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Kajege.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Jimbo la Mwibara bado lina vitongoji vingi ambavyo havina umeme. Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika vitongoji hivyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na miradi ya vitongoji inayoendelea katika Jimbo la Mwibara pia watanufaika na mradi huu mkubwa unaokuja kupeleka umeme kwenye Vitongoji Awamu ya Pili B kwani Jimbo la Mwibara na lenyewe limetengewa vitongoji.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itaendelea kupeleka umeme kwenye vitongoji kadri ya upatikanaji wa fedha na kwa mradi huu wataendelea kunufaika pia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Dkt. Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Kata ya Ilula - Kijiji cha Igingilanyi, Wilaya ya Kilolo nguzo zimewekwa tangu mwezi wa 11 mwaka jana mpaka leo hii umeme haujawashwa na wananchi wanasubiri kwa hamu. Je, lini sasa umeme huo utawashwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake; ninalifahamu eneo lile tulipata changamoto kidogo kwa sababu eneo hili lilikuwa la ziada, lakini nimhakikishie tayari tumeshajipanga mpaka kufikia mwezi wa saba tutakuwa tumepeleka pale nyaya na kufikisha umeme katika eneo husika. Nimkumbushe Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Nishati Vijijini wamuongezee mkandarasi *addendum* pale ili aweze kukamilisha kazi hii ili wananchi waendelee kunufaika na upatikanaji wa umeme katika eneo hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika vitongoji vya Mkoa wa Simiyu ambavyo havina umeme? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, tayari kuna miradi ya vitongoji inaendelea katika Mkoa wa Simiyu lakini kwa mradi wa kupeleka umeme katika Vitongoji Awamu ya Pili

B na Mkoa wa Simiyu pamoja na majimbo yake yote na yenyewe yako katika mkakati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwenye vitongoji 15 vya Mbunge katika Jimbo la Babati Mjini vitongoji sita *line* kubwa ipo mbali hivyo tukaomba *TANESCO* mtusogezee umeme kwenye hivyo vitongoji ili *REA* waendelee. Ni lini mtatupatia hizo fedha?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, baada ya kutoka hapa ninaomba nifanye mawasiliano na wenzangu ili kuweza kuona ni kwa namna gani tutaweza kusaidia katika maeneo haya sita ambayo amesema Mheshimiwa Mbunge ili na wananchi wake na wenyewe waendelee kunufaika na miradi hii ya kupeleka umeme.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge nikitoka hapa basi tutafanya mawasiliano kuona namna gani tutatafuta hizo fedha kwa ajili ya kuanza kupunguza kero hii katika maeneo ambayo ameyasema.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Nimwite sasa Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 492

**Kuongeza Uzalishaji Pamoja na Soko la Pareto Nchini**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani wa kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa soko la zao la pareto?

**MWENYEKITI:** Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Mheshimiwa David Silinde.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Serikali katika mwaka wa fedha 2024/2025 imetekeleza mikakati mbalimbali ili kuongeza uzalishaji wa zao la pareto nchini ikiwemo kusambaza mbegu bora kilo 890 za pareto kwa wakulima 3,500 katika maeneo ya uzalishaji na kuboresha mifumo ya upatikanaji wa soko kwa kusajili kampuni 11 za kununua na kuchakata pareto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka wa fedha 2025/2026 imepanga kuongeza uzalishaji wa pareto kufikia tani 5,000. Lengo hilo litafikiwa kupitia mikakati mbalimbali ikiwemo kusambaza mbegu bora za pareto kilo 5,300 kwa wakulima; kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la pareto kwa wakulima viongozi 19,000 na wakaguzi wa pareto 50; na kuratibu ujenzi wa makaushio 150 ya pareto katika Halmashauri za Makete, Ileje, Mbeya, Ludewa, Mbulu na Arusha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana, pamoja na uzalishaji mdogo huu wa pareto nchini, lakini Tanzania inaongoza Afrika kwa uzalishaji wa zao hili la pareto. Kuna changamoto kubwa sana ya mnyororo wa thamani ya hili zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima analipwa shilingi 3,700 kwa kilo wakati yule mnunuzi akiisaga analipwa shilingi 6,000 kwa kilo na ukitengeneza ikiwa *crude* kwa kilo inauzwa 200,000 na *refinery* inauzwa shilingi 1,000,000 kwa kilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia huu mnyororo unaona kabisa kuwa mkakati uliopo siyo mzuri na haumsaidii sana mkulima wala kuisaidia nchi yetu. Je, ni kwa nini sasa Serikali isirudishe bodi maalum ili iweze kusimamia zao hili muhimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa sababu tuna kiwanda cha kuzalisha viuatilifu pale Kibaha ambacho kinaweza kuzalisha viuatilifu kutumia pareto. Ni kwa nini, Serikali isiwe na mkakati maalum sasa ili zao hili liweze kutuletea viuatilifu ambavyo ni *organic* kutoka hapa hapa nchini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, mimi nimthibitishie tu Mheshimiwa Njeza kwamba moja ya zao ambalo sisi Serikali tunalipa kipaumbele sasa hivi ni pamoja na zao la pareto. Pia mnatambua kabisa kwamba tangu Mheshimiwa Rais ameingia madarakani ndio unaweza kuona mazao ambayo yalikuwa yamepotea sasa hivi yananyanyuka ikiwemo zao la pareto ambalo kwa sasa sisi ni wa kwanza Afrika na wa pili nafikiri duniani.

Kwa hiyo, kuhusu bodi kwa sasa yanasimamiwa na Bodi ya Mazao Mchanganyiko, lakini ni jambo ambalo lipo katika mipango yetu kulingana na uzalishaji jinsi unavyoendelea. Kwa hiyo, jambo hilo niseme tu tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kufufua kiwanda kwa ajili ya kuzalisha viuatilifu na lenyewe lipo katika mipango ya Serikali. Kwa hiyo, nimwondoe shaka Mheshimiwa Mbunge katika hili.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea na swali linalofuata. Nimwite sasa Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, aweze kuuliza swali lake.

Na. 493

**Kuboresha Miundombinu ya Umwagiliaji Bagamoyo**

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ya umwagiliaji katika Jimbo la Bagamoyo hasa katika Mradi wa *JICA*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Skimu ya *Bagamoyo Irrigation Development Programe (BIDP)* yenye ukubwa wa hekta 100 iliendelezwa na Serikali kupitia ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Japan *(JICA)* kwa lengo la kufundishia wakulima katika Kijiji cha Sanzale, Kata ya Magomeni, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. Skimu hiyo imeendelea kufanyiwa ukarabati na kuendelezwa na Serikali kwa awamu tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika mwaka wa fedha 2025/2026 imepanga kufanya maboresho ya miundombinu ya umwagiliaji katika skimu hiyo ili kuhakikisha inazalisha kwa tija na kuongeza ufanisi wa matumizi ya rasilimali maji. Kazi ya tathmini ya uchakavu wa miundombinu ya umwagiliaji kwa ajili ya kupata gharama halisi za ukarabati wa miundombinu hiyo inaendelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Muharami Mkenge.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru pia nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; eneo la skimu ya umwagiliaji hili lina ukubwa wa hekta 100 tu kama ulivyosema, lakini wenzetu wa Magereza wana eneo kubwa sana ambalo limepakana na skimu hii. Je, Wizara yako iko tayari kwenda kuzungumza na hawa watu wa Magereza kutuongezea hili eneo ili lote liwe la skimu ya uwagiliaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Serikali ina mpango wa kujenga mabwawa makubwa kwa ajili ya uwagiliaji na pale Bagamoyo kuna mradi mmoja ambao upo katika Wizara yako Mradi wa Bwawa la Mandela; je, ni lini Serikali sasa itaanza mpango wa kujenga bwawa hili ili liweze kusaidia umwagiliaji katika mashamba ya *Bagamoyo Sugar* na skimu nyinginezo katika Jimbo la Bagamoyo na Chalinze? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, mimi nimpongeze sana Mheshimiwa Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo kwa maswali mawili ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, utayari wa sisi Serikali; sisi muda wote tuko tayari na tutazungumza na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani kuhakikisha jambo hili linakuwa na tija kwa pamoja. Hata hivyo, moja ya mipango tuliyonayo katika ujenzi wa miundombinu ninafikiri tutawafikia mpaka katika eneo hilo. Kwa hiyo, hilo tutalifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; kuhusu Bwawa la Mandela ambalo amelizungumzia hapa ni kwamba Bwawa hilo ni miongoni mwa yale mabwawa 100 tunayoyafanyia tathmini sasa hivi. Kwa hiyo, lipo katika mipango yetu ya Serikali na tukishakamilisha maana yake tutalipa kipaumbele yawe yale mabwawa ya mwanzoni kwa ajili ya kuanza kujengwa. Kwa hiyo, na lenyewe lipo katika mipango yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Eric Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kuniona. Ninatoa shukrani nyingi sana kwa Wizara ya Kilimo na Serikali kwa ajili ya Miradi ya Sukuma na Magulukenda.

Je, Serikali ina mpango gani kwa wananchi wa Bonde la Bupandwa, Kafunzo na Luhorongoma ili waweze kupata mradi wa umwagiliaji mwaka huu wa fedha? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimthibitishie tu Mheshimiwa Shigongo na anafahamu kwamba moja ya kazi kubwa ambayo tunafanya sisi Wizara ya Kilimo ni kumalizia tathmini katika maeneo yote ambayo ameyaainisha na baada ya hiyo tathmini maana yake tutaanza kutafuta mkandarasi ili yaanze kujengwa. Kwa hiyo, yapo katika mipango yetu ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji. Nimwite sasa Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mbunge wa Mwanga, aulize swali lake na kwa niaba yake litaulizwa na Mheshimiwa Priscus Tarimo.

Na. 494

**Kukamilisha Miradi ya Maji - Mwanga**

**MHE. PRISCUS J. TARIMO K.n.y. MHE. JOSEPH A. TADAYO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha Miradi ya Maji Kijiji cha Mangio, Mwaniko na Msangeni – Mwanga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Andrea Kundo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji Mwai-Mwaniko-Mangio uliopo Wilaya ya Mwanga, Mkoani Kilimanjaro. Kazi zinazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ukarabati wa matanki mawili yenye ujazo wa lita 90,000 kila moja, ujenzi wa nyumba ya mitambo *(pump house),* ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 17 sanjari na ujenzi wa vituo 30 vya kuchotea maji. Utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 60% na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2025 na kunufaisha wananchi wapatao 5,551 waishio kwenye Vijiji vya Mwai, Mwaniko na Mangio. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu hayo mazuri ya Serikali lakini ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; upatikanaji wa maji katika Mkoa mzima wa Kilimanjaro na maeneo ya Arusha ambayo inajenga ile *Pangani River Basin* inategemea sana utunzaji wa mazingira. Je, mamlaka zinazozunguka *basin* hiyo pamoja na Wizara wana mpango gani wa utunzaji wa mazingira? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Mamlaka ya Maji Moshi imewekeza fedha nyingi sana kwa ajili ya majitaka hasa kwenye Kiwanda kile cha Ngozi cha Karanga na kwa wakazi lakini inaonekana yale mabwawa yamefikia *limit*. Serikali inashirikiana vipi na sisi kuhakikisha kwamba yale mabwawa yanapata fedha kwa ajili ya upanuzi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa vivutio vya mazingira ni pamoja na uwepo wa vyanzo vya maji ikiwemo chemichemi, maziwa, mabwawa pamoja na mito na ni asilimia kubwa (zaidi ya 80%) ina mchango mkubwa sana kwa maisha ya binadamu, wanyama pamoja na mimea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Sheria yetu Na. 5 ya mwaka 2019 imeipatia majukumu Wizara ya Maji kupitia Bodi za Mabonde ya Mito kuhakikisha kwamba wanashirikiana na wadau kulinda, kutunza, kusimamia na kuhifadhi vyanzo vya maji na kuhakikisha kwamba mazingira yanaendelea kutunzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sanjari na hilo kupitia Mfuko wetu wa Maji wa Taifa katika kanuni ambazo Mheshimiwa Waziri alizisaini tumetenga 10% katika mapato ya Mfuko wa Maji ili ziende kwa mabonde kwa ajili ya kwenda kuhakikisha kwamba tunasimamia, kulinda na kuhakikisha kwamba mazingira katika maeneo hayo yanakaa vizuri kwa sababu vyanzo vya maji ndio msingi wa maji tunayoyapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipengele cha pili tunatambua kwamba Mji wa Moshi unaendelea kuwa msafi na kuendelea kwake kuwa msafi ni kwa sababu ya kazi nzuri sana ya Mheshimiwa Mbunge ambayo anaifanya kwa kushirikiana na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabwawa pamoja na kile kiwanda ambacho Mheshimiwa Mbunge amesema ili kuendelea kuondosha maji na kuwa *sustainable* ni lazima tuwe na mabwawa ya uhakika ambayo yataweza kupokea yale maji na sasa yameelekea kufikia ukomo wake. Tayari Mamlaka ya Maji Moshi wameshaandika andiko kwenye Mfuko wa Taifa ili wapatiwe fedha kwa ajili ya kwenda kupanua yale mabwawa ili kuwa na uhakika wa ukusanyaji wa maji taka kutoka katika Mji wa Moshi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, mmesimama wengi ninaomba maswali mafupi, moja kwa moja nenda kwenye swali. Tuanze na Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na tunaishukuru sana Serikali tayari imechimba visima vitano katika Jimbo la Mbulu Mjini na hadi sasa baadhi ya visima vimeanza kutoa huduma kwa wananchi.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa jumla kitaifa kuendeleza vile visima vitano kwa ajili ya programu ya visima 900 nchini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba zoezi la kwanza ilikuwa kuchimba na kuangalia wingi wa maji na baada ya hapo tunafanya usanifu ili kuhakikisha kwamba tunatengeneza mtandao wa wananchi kupata huduma ya maji. Pia tunapogundua kwamba maji yale hayatoshi kupelekwa kwa wananchi wengi sana tunatengeneza *point source* katika eneo lile la kisima ili wananchi angalau waanze kupata maji wakati Serikali ikiwa inatafuta fedha za kufanya usanifu wa kupanua mradi huo ama kutoka katika mradi mwingine ulioko karibu, lengo ni kwamba wananchi wafikiwe na huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imejipanga na kwa bajeti ya shilingi trilioni 1.06 hakika tutaenda kuhakikisha kwamba changamoto zote hizo tunazimaliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na niipongeze Serikali kwa jinsi ambavyo wanakubali na kuhakikisha wanamsikiliza Mheshimiwa Rais kumtua mwanamke ndoo kichwani.

Kwa kuwa kuzalisha maji safi na salama ni gharama sana, lakini bado upotevu wa maji uko juu; je, ni lini ile programu ya kuelimisha wanawake kuhusu utunzaji wa maji safi na salama hayo itaanza hususan mkoani Kilimanjaro? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninapenda sana kupokea kwanza ushauri wa mama yangu Mheshimiwa Shally Raymond ambapo kwa kweli amekuwa akilipigia chapuo sana hili suala la kuwaelimisha kwa sababu suala la maji kwanza kuwa na elimu ili tuweze kutunza vyanzo na miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa sana Serikali inaendelea kupokea ushauri kutoka kwa wadau akiwepo Mheshimiwa Mbunge. Tutalifanyia kazi na pale fedha zitakapopatikana tutaanza programu hiyo mara moja ili wakina mama wapate elimu hiyo stahiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Nicodemas Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninakushukuru kwa kuniona, lakini ninakushukuru pia kwa maelekezo yako. Ninaenda moja kwa moja kwenye swali kwa ufupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri, visima vitano tumechimba mwaka 2024, lakini Mji wa Mbogwe yaani watu wa Mbongwe, hayo maji hayatoshi. Lini Mradi wa Maji mkubwa wa Ziwa Victoria utaanza kutekelezwa, kupelekwa Mbogwe pamoja na Bukombe?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napokea shukrani za Mheshimiwa Mbunge wa Mbogwe kwa kutambua mchango mkubwa wa Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kumchimbia visima vitano na yeye amekiri kabisa kwamba vimekamilika. Suala la maji kutoka Ziwa Victoria ni ndoto ya Watanzania wengi, kutumia maji ya Ziwa Victoria, lakini ndoto hii inakamilishwa na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, zoezi la kufikisha maji Mbogwe linatanguliwa na usanifu wa mradi. Utakapokamilika basi zoezi la ujenzi wa mradi kuja Mbogwe utafanyika bila kuwa na taswishwi yoyote. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Oliver.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Je, lini mradi wa maji kutoka Kanazi, Kemondo, utafika Vijiji vya Muhutwe na Mayonde, Jimbo la Muleba Kaskazini, kwa Mheshimiwa Mwijage?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Oliver. Ninafahamu anavyoendelea kuwapigania wananchi wa Kagera kwa ujumla akiwa mwakilishi wa akinamama mashuhuri kabisa, lakini pia ninaomba nilipokee hili, ili nimpatie taarifa stahiki ambazo zinaendana na uhalisia uliopo kule. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nilikuona, Mheshimiwa Anathropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukru sana. Takwimu zinaonesha kwa mwaka 2024 mikoa yote Tanzania Bara, kuondoa miwili ya Kilimanjaro na Iringa, wamepata

kipindupindu na tunajua sababu za kipindupindu ni pamoja na kunywa maji machafu. Sasa pamoja na uchimbaji wa mabwawa, kwa maana ya kupata maji, je, ni mkakati gani wa Serikali kuhakikisha inaweka *water purifiers,* ili kuondoa changamoto ya kipindupindu ambayo imekuwa inajitokeza na kujirudia miaka yote?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kipindupindu; kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuliongelea hili kwa sababu linalenga moja kwa moja kwenye afya za watoto, akinamama na wakazi wote wa nchi hii, lakini suala la kipindupindu ni jambo mtambuka ambalo linagusa sekta mbalimbali. Sisi kama Serikali, tutaendelea kushirikiana na wadau wote wanaoguswa na jambo hili, ili tuwe na mkakati wa pamoja. Lengo ni wananchi wetu tuhakikishe kwamba hawapatwi na magonjwa kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi Wizara ya Maji tunaendelea kusisitiza kuhakikisha kwamba maji yetu yanatibiwa ili yawafikie yakiwa ni salama na ni safi. Lengo ni kwamba mpaka sasa tumeshafikia 80% ya kufikisha huduma ya maji safi na salama kwa wananchi vijijini na 91% kwa upande wa mjini. Kwa hiyo, hiyo ni sehemu mojawapo ya mkakati wa Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha kwamba wananchi hawapati magonjwa ambayo yanatokana na kunywa maji machafu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Ndege.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na niishukuru kwanza Serikali kwa kutukamilishia mradi wa visima katika Kijiji cha Riroda na Hewasi na tayari mabomba yameshaanza kusambazwa.

Je, ni lini sasa mradi huu utakamilika, ili wananchi waweze kupata huduma ya maji?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, ameuliza hili swali mara kadhaa na leo hii ninafurahi na yeye amekiri kwamba tayari mabomba yamesambazwa. Ninaamini kabisa kwamba utaratibu wa ukamilishaji wa mradi huu upo ndani ya utaratibu wa mkataba ambao tumesaini na mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Mbunge awe mvumilivu, mradi huu utakamilika kwa wakati. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushuru sana na ninaishukuru Wizara ya Maji walipeleka shilingi milioni 830 katika Kijiji cha Unyali, lakini wiki mbili zilizopita niliuliza swali hili wakaniambia kwamba hela shilingi milioni 180 itaenda kumalizia huu mradi. Sasa ni lini hiyo hela itafika kwa sababu sasa wiki mbili zimepita?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere na naomba nirejee, sikusema zitapelekwa, nilisema zimeshapelekwa na tayari zipo zinafanya kazi na ndivyo ambavyo nilijibu siku ile. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nini mkakati wa Wizara kuhakikisha wanachimba visima kwenye vituo vya afya ambapo wamekuwa na madeni makubwa ya maji kutokana na kwamba hawana uwezo wa kulipa maji kwa wakati na badala yake wawe na visima?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu analenga hospitali gani na vituo vya afya katika Mkoa wa Tabora. Hakika tunajua kabisa kwamba lengo lake ni kuhakikisha kwamba hatupati changamoto katika vituo vyetu vya afya kwa kukosa maji kwa sababu ya bili. Tunatambua kwamba sasa tumeshaweka mkakati, tunapofanya usanifu tunafikiria pia taasisi za Serikali, shule, vituo vya afya na zahanati, usanifu wetu uhakikishe kwamba unajumuisha taasisi hizi ili maji yanapohitajika yasiwe na changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tuna mkakati wa pamoja kuhakikisha kwamba vituo vya afya havikosi maji na hata shule ambapo watoto wetu wanasoma, hawakosi maji. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kukumbusha hili na Serikali tutaendelea. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, namuita sasa Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, aulize swali lake. Mheshimiwa Vita Kawawa simuoni! Mheshimiwa Omari Kigua.

Na. 495

**Kutatua Migogoro ya Mipaka ya Hifadhi Kata za Mputa na Mchomoro, Namtumbo**

**MHE. OMARI M. KIGUA K.n.y. MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatatua migogoro ya mipaka ya Hifadhi Kata ya Mputa na Mchomoro, Namtumbo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Geofrey Mizengo Pinda.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** Alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina jukumu la kutafsiri Matangazo ya Serikali kuhusu Mipaka ya Hifadhi na Mipaka ya Kiutawala. Katika kutekeleza jukumu hili, Wizara yangu inashirikiana na Wizara za Kisekta, ikiwemo Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia migogoro ya mipaka ya hifadhi katika Kata za Mputa na Mchomoro, Wilayani Namtumbo, Wizara itaunda timu ya wataalam inayojumuisha watumishi kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambayo itashirikiana na Halmashauri za Vijiji vyenye migogoro ya mipaka katika kutatua migogoro husika. Timu hiyo inatarajia kuanza kazi kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2025.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan Kungu, maswali ya nyongeza, kwa niaba ya Mheshimiwa Vita Kawawa.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, kutokana na swali la Mheshimiwa Vita Kawawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali na kwa kuwa changamoto ile imekuwa ni kubwa; majibu yanasema kuna timu ambayo itakwenda kushughulikia changamoto ile. Ninataka kufahamu, je, ni lini hasa watakwenda kutatua changamoto hiyo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, ni kwamba kabla ya mwisho wa mwezi huu wa sita tutakuwa tumepeleka timu ambayo itakwenda kupitia maeneo haya. Kusema ni lini hasa kwa sababu ni muundo wa timu kutoka karibu sekta tatu, Wizara yetu, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; mawasiliano yanaendelea ili kuandaa hii timu iweze kwenda eneo hilo haraka zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Noah Mollel.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, kumekuwepo na mgogoro kati ya wananchi wetu wa Wilaya ya Arumeru na Longido katika Vijiji vya Engutukoiti na Engikareti. Mgogoro huu umechukuwa muda mrefu sana na tumekuwa tukifuatilia Wizarani mara kwa mara.

Sasa nataka kufahamu, ni lini Serikali kwa maana ya kupitia Wizara ya Ardhi, itakwenda kuhitimisha mgogoro huu ili wananchi waweze kuishi kwa amani na utulivu kwa sababu hata jana wameongea kwenye ITV na kuleta mtafaruku mkubwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mgogoro wa Arumeru na Longido ni mipaka ya kiutawala. Tumemuelekeza Kamishna wetu wa Mkoa wa Arusha aende kwenye eneo hilo la mgogoro ili kubainisha hasa nini chanzo cha mgogoro kwa sababu mipaka hii imekwishawekwa siku nyingi na kumekuwepo na utulivu wa miaka mingi katika eneo hili, lakini sasa tukajue kisa hasa ni nini. Kwa hiyo, naendelea kumuelekeza Kamishna wa Ardhi, Mkoa wa Arusha, aende haraka sana na kuleta taarifa Wizarani ili tuone namna nzuri ya kwenda kulitatua.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Tumalize maswali, Wizara ya Afya.

Tumuite sasa Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Donge, aulize swali lake.

Na. 496

**Kuwezesha Watanzania Kupata Huduma ya Afya kwa Usawa**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka huduma za afya bure kama ilivyo katika elimu ya msingi na sekondari?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Waziri. Mheshimiwa Dkt. Mollel.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** Alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuboresha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya kwa wananchi wasio na uwezo. Tangu mwaka 1995 Serikali imekuwa ikitekeleza Sera ya Msamaha wa Gharama za Matibabu kwa Wananchi Wasio na Uwezo. Hata hivyo, kutokana na changamoto ambazo zimeendelea kujitokeza

katika utekelezaji, Serikali iko katika hatua za utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Sheria hiyo itatoa fursa kwa watu wasio na uwezo kugharamiwa bima ya afya na Serikali ili kuwawezesha kupata huduma za afya bila kikwazo cha fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Soud.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Pia namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza; kama unavyojua kwamba Tanzania ni nchi ya ujamaa na misingi mikubwa ya ujamaa ni kutoa huduma zile muhimu katika hali ya usawa na haki. Sasa je, Mheshimiwa Waziri hauoni haja ya kuja na mpango maalum wa dharura ili kuweza kusaidia kuimarisha huduma hizi za afya kwa wale wenye vipato vya chini na vipato vya kati, ili wasitwezwe utu wao na kuweza kudhalilika wakienda hospitali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali namba mbili; kwa kuwa bima ya afya ndiyo ipo katika utaratibu na inaweza ikachelewa kidogo, sasa je, hatuoni haja ya kuja na mpango wa dharura, tukatenga fedha maalum katika bajeti ya kila mwaka ili kusaidia hao wenye mazingira magumu na wananchi ambao wanashindwa kuweza kukimu hizi dharura za kiafya katika huduma zao?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kumpongeza Mbunge mwenzangu kwa namna ambavyo kwa kweli, ameliona hili swali ambalo ni nyeti na Wabunge wengi wamekuwa wakilisemea. Namhakikishia tu kitu kimoja, ujamaa unaanzia kwenye familia, lakini ni kweli hata sisi

tunapopanga mipango ile mizuri ya kijamaa ndani ya familia wakati wote tunaweza tukawa tumetimiza 60%/70% ya malengo ambayo tulikuwa tumejipangia. Hata hivyo, kwenye eneo hili sasa ambalo tunalizungumzia nimewahi kusema hapa kwa miaka mitatu iliyopita, mwaka 2022 tulifanya uchunguzi na kupiga mahesabu, tukakuta kwenye eneo hili tu la kusaidia watu wasioweza kulipa malipo Serikali ilitumia shilingi bilioni 667.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwa wanawake na watoto utaona kwa mwaka 2024 tu, Serikali imetumia shilingi bilioni 157 kusaidia. Ni kweli kwamba kinachohitajika ili kuwahudumia wote ni zaidi ya shilingi bilioni 227 ambazo kwa wakati huo, kama unavyojua Mbunge mwaka huu ulitupitishia shilingi bilioni 200 kwa ajili ya dawa na vifaatiba. Kwa hiyo, nakuhakikishia kuna mifumo ya kufanya ili kuhakikisha hili unalotaka litekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, tunaanza kwa Mtendaji wa Kata kupata barua. Anapokwenda na ile barua, itaheshimika na atatibiwa bila matatizo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumalizie swali letu la mwisho. Wizara ya Maliasili na Utalii, namuita Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba, aulize swali lake.

Na. 497

**Kuvitambua Vivutio vilivyoko Momba**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE** Aliuliza: -

Je, lini Serikali itavitambua vivutio vilivyopo Jimbo la Momba kama vile Nyayo za Mtu wa Kale, Nkanyama, Maporomoko ya Mfuso na Yala (Mpona)?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri Dunstan Luka Kitandula.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** Alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ilitekeleza zoezi la kutambua vivutio vya utalii katika Wilaya ya Momba kwa lengo la kuviendeleza na kuvitumia kama bidhaa za utalii. Miongoni mwa vivutio vilivyobainishwa ni Nyayo za Mtu wa Kale, Nkanyama, Maporomoko ya Mfuso na Yala (Mpona) na Kimondo cha Ivuna. Baada ya kuvibaini vivutio hivyo, zoezi linalofuata ni kufanya tathmini ya vivutio vilivyobainishwa ili kupata vivutio ambavyo viko karibu na miundombinu wezeshi kwa ajili ya kuvipa kipaumbele katika uendelezaji kwa kushirikiana na halmashauri husika na wadau wa sekta binafsi, ili kupata matokeo ya haraka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa nafasi. Naomba nipongeze majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio makubwa ambayo yapo kwenye sekta hii ya utalii, lakini miongoni mwa changamoto kubwa ambayo inaikumba sekta yetu ya utalii hapa nchini ni watalii wanapokuja, wakitazama vile vivutio hawawezi kurudi tena kwenye nchi yetu, kwa ajili ya kutazama vivutio vingine maana vivutio vilivyopo ni vilevile.

Swali langu, Serikali inaonaje kuongeza wigo mpana na kuweka vivutio vingi ili mtalii huyu anapokuja hapa nchini, akitembelea mbuga za wanyama, akienda sijui kwenye vitu gani, akutane na utalii wa chakula, simulizi za watu wa kale na mambo mbalimbali ili apate orodha ya vitu vingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; inaonekana kwamba utalii unafanya vizuri Kaskazini tu, Arusha labda na Kilimanjaro na

kwa mikoa michache kama Morogoro pale Mikumi na Iringa kwa sababu ya Ruaha, lakini mikoa mingine imeachwa nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatolea mfano, kule Zambia kuna maporomoko ya *Victoria Falls*; mtalii huyu inabidi anapotoka Arusha anaenda Morogoro, afike Iringa atembee na gari, afike labda Uyole pale akutane na mila za Wasafwa, aende Songwe akutane na mila za Wandali na Wanyamwanga, aende na gari mpaka kufika Zambia, lakini arudi kwenda Dar es Salaam kupanda ndege na kuondoka, hivi tunapoteza mapato hapa katikati.

Je, ni mkakati upi wa Serikali kuongeza vivutio vingi, lakini kutokuweka matabaka kwenye mikoa kadhaa kwa sababu tuna vivutio vingi nchini kote? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, zipo hisia kwamba utalii wetu umejikita zaidi kwenye utalii wa wanyamapori, 80% ya utalii wetu umejifunga hapo. Kwa hiyo, kama Wizara tumeweka mkakati sasa wa kuibua aina nyingine za utalii na kuwa na vivutio mchanganyiko ili kuhakikisha kwamba utalii usijikite tu kwenye wanyamapori, lakini uende kwenye maeneo mengine. Kama ambavyo wengi wenu mnafahamu, mwezi uliopita tu Mei, Tanzania ilipata heshima ya kuwa mwenyeji wa mkutano mkubwa wa pili wa utalii wa vyakula katika Ukanda wa Afrika, hizi ni miongoni mwa jitihada tunazofanya kuhakikisha tunakuwa na utalii wa aina tofauti tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kule kwenye Ukanda wa Bahari tuna utalii mwingine wa kutumia meli zinazoleta watalii kwenda kwenye maeneo ya fukwe kuangalia maeneo yetu ya magofu na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, jitihada zimeanza za kuhakikisha kwamba

tunafungua uwanja mpana wa kuwa na vivutio mchanganyiko ili watalii waweze kukaa kwa muda mrefu na vilevile wavutike kurudi kutembelea nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili eneo ambalo tunasema mikoa mingine ni kama imefungwa hivi, haipati watalii wa kutosha, ni kweli Serikali imeliona hilo na ndiyo maana tumekuja na mkakati mkubwa sana wa kufungua mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ambako uwekezaji mkubwa umefanyika na Serikali kuhakikisha tunafungua ukanda ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile jitihada hizi zinazofanywa na Wizara ya kwenda kwenye mikoa yetu na kutambua vivutio vilivyopo kwenye maeneo hayo ili na vyenyewe viweze kuendelezwa na kufungua fursa za utalii mpana kwa nchi yetu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeona changamoto hizi na zinafanyiwa kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha. Niwaletee wageni ambao wako ndani ya ukumbi wetu leo hii.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; wageni wa Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Akson na hawa ni makada wa CCM wakiongozwa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, Ndugu Leonard Mahenda au kwa jina lingine Manguzo ambao ni Ndugu Hashraf Abdul, Salum Mzamidu, Daniel Nyanda, Ndugu Paschal Masome, Ndugu Jackson Kalani na Ndugu Majaliwa Aloyce. Karibuni sana kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni ambao ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kwanza nitaanza na wageni 78 wa Mheshimiwa Antony Peter Mavunde - Waziri wa Madini, na hawa ni wanafunzi 70 na

walimu nane wa Shule ya Msingi Amani kutoka Jijini Dodoma. Tuwaone na karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni 30 wa Mheshimiwa Dkt. Godwin Aloyce Mollel - Naibu Waziri wa Afya, hawa ni wauguzi kutoka hospitali za mikoa na wilaya na viongozi wa Chama cha Wauguzi Tanzania waliomaliza muda wao na waliopo madarakani. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Mollel ana wageni wengine wanne ambao ni Kamati ya Utekelezaji ya UVCCM Wilaya ya Siha wakiongozwa na Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Siha, Komredi Emmanuel Abas. Wako pale juu, karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, huyu ni Ndugu Joseph Posta, ndugu yake kutoka Jijini Dodoma. Karibu sana. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Florent Laurent, huyu ni Ndugu Nickson Rutagwerela, Kada wa CCM kutoka Misenyi Mkoa wa Kagera. Karibu sana. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, huyu ni Ndugu Pili Mokiwa, mpiga kura wake kutoka Bagamoyo, Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Kuna wageni watatu wa Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, hawa ni rafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wageni wawili wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, hawa ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana pale. *(Makofi)*

Tuna wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, hawa ni jamaa zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Wako hapo, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, hawa ni Watendaji wa *Chiku Mugo Foundations* kutoka Jijini Dodoma. Karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Tuna wageni tisa wa Mheshimiwa Bernadeta Kasabago Mashashu ambao ni ndugu zake kutoka Wilaya ya Bukoba, Mkoani Kagera. Wako pale, karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Tuna wageni 12 wa Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, hawa ni wanafunzi wa Chuo cha Mipango cha Jijini Dodoma wanaotoka Kiteto, Mkoani Manyara. Wako pale tumewaona na karibuni. *(Makofi)*

Tuna wageni 12 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, hawa ni watumishi wa Mungu kutoka Wilaya ya Kilolo, Mkoani Iringa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Kabati ana wageni wengine; hawa ni Kwaya ya Ebeneza, Kanisa la Anglikana kutoka Veyula, Mkoani Dodoma. Wako pale juu, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 52 wa Mheshimiwa Juliana Masaburi, hawa ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Awali na Msingi Montessori Msimbazi, Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni saba wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe; hawa ni wanakikundi wa Roi kutoka Jijini. Jiji gani hamjasema hapa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni Ndugu Henry Luhamba kutoka Dodoma. Yuko pale, karibu. *(Makofi)*

Ndugu Jacob Kapinga, mwalimu kutoka Manispaa ya Songea, Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 71 na walimu watano kutoka Shule ya Msingi Wisdom Junior kutoka Kata ya Msambara, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Mkoani Kigoma. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Mollel na hawa ni wafanyakazi wa *Mo Dewji Foundation;* hawa ni wadau wanaotoa huduma bure kuhudumia watoto wenye changamoto ya kichwa kikubwa na mgongo wazi kwa kushirikiana na Hospitali ya *MOI*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Sijawaona, wako wapi hawa? Wako pale, karibuni sana. Tunawashukuru kwa kazi yenu. *(Makofi)*

Halafu tuna makada saba wa CCM wakiongozwa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu. Hawa tumekwishawasoma tayari. Hawa Manguzo tumeshawasoma tayari. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mengine mawili hapa; kwanza, mnataarifiwa kwamba Kamati ya Kanuni za Bunge imeanza kazi yake ya kuzipitia na kufanya marekebisho katika Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023. Waheshimiwa Wabunge wote wenye mapendekezo ya marekebisho katika Kanuni hizo mnatarifiwa kuwasilisha mapendekezo hayo kwa Katibu wa Bunge ili yaweze kuzingatiwa na Kamati kabla ya kuwasilishwa ndani ya Bunge letu. Kama una mawazo, mapendekezo, yapeleke kwa Katibu wa Bunge na itakapokuja hapa yawe yako ndani, siyo unaanza kuyasemea hapa. Ingawa hutazuiwa kusemea hapa, lakini itasaidia zaidi ukiyapeleka mapema.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine; mnataarifiwa na kushauriwa kwamba pitieni kwenye kishikwambi kuna marekebisho madogo yamefanyika kwenye ratiba ya Vikao vya Bunge au ya Shughuli za Bunge zinazoendelea. Kwa hiyo, kwenye vishikwambi vyenu imeshawekwa. Haya ndiyo matangazo pekee niliyonayo.

Baada ya hapo tunaendelea. Katibu.

**NDG. AZIZA MAKWAI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano ya hoja iliyo mbele yetu ya Wizara ya Afya. Nina orodha ya wachangiaji hapa. Tutaanza na mchangiaji wa kwanza Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati inayohusika na masuala haya.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kingu, naomba ukae kidogo.

Ninaomba wafuatao wajiandae baada ya Mheshimiwa Kingu kumaliza. Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga. Mheshimiwa Kingu, endelea.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa heshima ya kuwa mchangiaji wa kwanza asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niendelee kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI ambao mimi ni Mwenyekiti wao, kwa namna ambavyo tumeweza kufanyakazi kwa kipindi kifupi cha kuisimamia na kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niseme mambo machache; pamoja na kwamba jana tumetoa taarifa ya Kamati, tumeeleza mafanikio na changamoto, ninataka nikwambie kitu kimoja, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha huu mwaka ambao nimekuwa Mwenyekiti, ninataka nitumie fursa hii, nitakuwa mchoyo sana wa fadhila kama sitaeleza weledi mkubwa na ushirikiano mkubwa ambao Kamati hii umeipata kutoka kwa Waziri - Mheshimiwa Jenista Mhagama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ninawasihi sana wananchi wa Peramiho, kwa uhodari wa mama huyu, kwa namna na muda mfupi aliokabidhiwa kuiongoza Wizara hii ya Afya, Wizara ambayo ni *very complex,* Wana-Peramiho na Watanzania nataka niwaeleze, mama huyu ameonesha umahiri wa hali ya juu sana. Ameonesha umahiri wa hali ya juu sana kuiongoza Wizara hii ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimwambie Mama Jenista mama yangu, tabia yake ya unyenyekevu na ushirikiano ndio umetufanya Kamati yetu tuweze kufanya kazi na yeye. Pale ambapo tulikuwa tunamwambia hili hapana, alikuwa unanyenyekea na kurudisha majibu yanayotakikana kwa maslahi ya watu wetu. Hongera sana mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimsemee Naibu wake, kaka yangu Dkt. Mollel. Ninamshukuru sana kwa niaba ya Kamati, Naibu wangu Waziri, naye pia ni kijana mnyenyekevu na msikivu. Ahsante sana Dkt. Mollel, amekuwa msaada mkubwa sana kwa Kamati yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimebahatika kusafiri na Mheshimiwa Jenista kwenye nchi kadhaa katika mambo ya kampeni hizi za kimataifa. Huyu mama si wa kawaida, ninaomba niseme hivyo. Unaweza ukahisi kwamba mama huyu ameweza kuwa na *connection* na Mawaziri wa Afrika kama vile ameweza kuwa na *connection* na Wabunge kwenye Bunge hili, kwa namna ambavyo ameweza kuzoeana nao. Mama Jenista ni hazina kwa nchi yetu.

Mimi ninampongeza sana dada yangu na Mungu ambariki. Atashida Ubunge na *In Shaa Allah* akirudi hapa kama ataendelea kuiongoza Wizara hii, hayo siyo ya kwangu, lakini sisi Watanzania na kama Kamati tumeridhika sana na ushirikiano wake, yeye, naibu wake na Katibu Mkuu wake, kaka yangu Shakalaghe, mtu mahiri kabisa, pamoja na watendaji wote wa Wizara. Ahsanteni sana kwa ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nishauri mambo matatu; la kwanza; katika vifurushi ambavyo *National Health Insurance Fund* wamevileta, ninataka niwakumbushe Watanzania ili Watanzania waweze kupata picha wasije wakafikiri kwamba hii ndiyo bima ya afya sasa imeshaleta vifurushi. Vifurushi hivi ni *option* kwa watu ambao wanahitaji kupata huduma za *extra* za matibabu kama ilivyo katika mifuko mingine. Kwa mfano, tuna watu wa *Jubilee Insurance*, wana bima zao zingine zinakwenda mpaka milioni nane, milioni saba. Kwa hiyo, hivi si vifurushi vya *universal health coverage*, hizi ni *option* kwa mtu ambaye anataka kukata *Jubilee, NHIF* wameamua kujipanga kibiashara na wao wawe kama mashirika mengine ya kutoa bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ukisoma vifurushi hivi, bado wameweza ku-*accommodate* Watanzania. Kwa mfano, kifurushi cha mtu mmoja cha Tarangire, kipo kifurushi ya shilingi 168,000 ambacho kinampa mtu mmoja *access* ya kupata matibabu sawa sawa na mtu ambaye amekwenda kwenye *Jubilee Insurance* akaamua kukata kifurushi cha *level* hii. Itakapokuja *Universal Health Coverage, rate* ambazo zitatumika nchi nzima, hizo zitakuwa ni *rate entry* kwa Taifa zima, hazitakuwa na ubaguzi kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ninaomba lieleweke ili kusudi Bunge hili lisije likaonekana kwamba limejadili kitu ambacho kitaleta taharuki kwa umma na kikawafanya *NHIF* waonekane kwamba huenda hawajatii maelekezo ya sheria tuliyoitunga ya Bima ya Afya kwa Wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni vifurushi *optional* ambapo na wao wameamua kuingia kibiashara kama ilivyo kwa makampuni mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu *MSD;* ninataka nimshauri Mheshimiwa Waziri, dada yangu. Hivi tunashindwa nini sisi Tanzania? Tumeweza kuwa na *energy security* kwenye nchi, tumeweza kuwa na *water security* kwenye nchi, tumeweza kuwa na *food security* kwenye Taifa letu, hivi ni kitu gani kinatushinda sisi kama Watanzania kuhakikisha ya kwamba tunakuwa na viwanda vya kutosha vya kuzalisha dawa katika Taifa letu ili kusudi fedha nyingi tunazozitumia kuagiza dawa ziweze kubaki ndani ya nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikushauri Mheshimiwa Waziri dada yangu amtafute mtu anayeitwa Meja Jenerali Kingu aliyekuwa Balozi wa Tanzania Algeria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikwambie, Taifa la Algeria ni marafiki zetu sana sisi Watanzania. Algeria wameweza kuzalisha dawa zao ndani kwa matumizi ya ndani na *export* kwa zaidi ya 80% mpaka 90% kwa viwanda vya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nishauri, walishafanya *engagement* na watu wa *MSD* kama sikosei. Mavere ni kijana, Taifa hili limemwamini na amefanya kazi kubwa sana ya kizalendo kuleta mageuzi makubwa *MSD*. Tumeona ameweza kupandisha kiwango cha ukusanyaji wa maduhuli na usambazaji wa dawa, ninampongeza sana kaka yangu. Hata hivyo, kwenye jambo hili la uzalishaji wa dawa kwenye Taifa letu, ili nchi yetu iweze kuwa na mambo ya usalama wa afya, ninawashauri, Algeria wameweka milango wazi kwa Tanzania. Waende wakafanye majadiliano na Taifa la Algeria ili tuweze kufanya *PPP* katika uzalishaji na usambazaji wa dawa katika Taifa letu. Tuweze kuokoa fedha za Watanzania zinazopotea kwa kununua dawa nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimwambie Mheshimiwa Jenista Mhagama, dada yangu, akiweza kuwasaidia *MSD* pamoja na *private sector* watakuwa wametenda haki na kuacha *legacy* jambo ambalo litakuwa limefufua ndoto na matarajio ya Mwalimu Nyerere aliyokuwa ameyawaza ya kuifanya Tanzania liwe Taifa la kuzalisha bidhaa zake ndani na kuuza kwa majirani zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakwenda mbali, *MSD* tulishapewa mpaka *opportunity* ya ku-*supply* dawa kwenye nchi za *SADC*. Ninawaomba sana watu wa Wizarani pamoja na Wizara ya Fedha, na ninashukuru sana Mheshimiwa Waziri wetu wa uwekezaji yuko hapa Profesa Kitila Mkumbo. Ninamwomba kama yangu akae na *MSD*, Wizara ya Fedha, Wizara ya Afya na Wizara ya Viwanda na Biashara, watengeneze *blueprint, specifically* kwenye sekta ya uzalishaji wa bidhaa za dawa ili waweze kuacha *legacy* na wamfute machozi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika sekta ya uzalishaji wa dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili la vifurushi nimeeleza, lakini nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sita-*recommend* kazi nzuri inayofanywa na mwanamama Mkurugenzi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa Wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekuwa kwenye Kamati hii kwa muda mrefu sasa. Wakati Irene anaingia madarakani mfuko huu ulikuwa umeanza kuleta hofu kwa Watanzania. Leo tunapozungumza makusanyo kwa mwezi dada huyu amepandisha fedha zinakwenda mpaka takribani shilingi bilioni 110. Hongera sana Mkurugenzi wa *NHIF* dada yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa ninalomwomba, aendelee kushirikiana na watu wake, pale ambapo Kamati ya Kisekta inatoa ushauri wasiupuuze ushauri. Kwa mfano, hata hili la vifurushi tuliwaambia wakimaliza kuvitengeneza wavirudishe kwenye Kamati. Sasa angalia watu hawana elimu ya kutosha, watu wamepata taharuki, kumbe jambo hili ni jema kabisa. Ikiwa

wangeleta kwenye Kamati watu leo hapa Waheshimiwa Wabunge wangekuwa ma-*champions*, wangewaelekeza Wabunge wenzao wajue kwamba vifurushi hivi ni *option*, siyo *universal health coverage*. Hili jambo ni *simple* kabisa wala hakuna sababu ya kuwa na taharuki kwa nchi wala kwa Bunge. Kwa maelezo yangu ninaimani nimewasaidia kuliweka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho na la tatu, ushauri ninaoutoa kuhusu nafasi ya *Chief Medical Officer (CMO)* wa Serikali kwenye Taifa letu, mimi nina maoni tofauti. Ninashauri, kulingana na unyeti wa nafasi ya *CMO* kwenye nchi yetu, kulingana na unyeti wa nafasi na *roles* zake *CMO* kwenye Taifa letu, ninawashauri Wizara wakae na wafikirie kama wanaweza wakatunga sheria ya kufanya Ofisi ya *Chief Medical Officer* wa nchi yetu iweze kuwa chini ya Wizara, lakini ipewe *independence* ambayo itaweza ku-*safeguard interest* za nchi katika kazi anazozifanya *CMO*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya *CMO* ni nyeti sana, kuna wakati mwingine zinaweza zikatokea rabsha za kisiasa zikamfanya *CMO* akashindwa kufanya majukumu ambayo yatalinda *interest* ya nchi yetu, *interest* ya watu wetu na kuhakikisha *professionalism* inafuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nitoe ushauri, waangalie namna kama inawezekana, wakaifanya taasisi hii ikawa *independent* chini ya Wizara, lakini usimamizi wake ukawa kwa namna ambayo wataweza kutanguliza mbele maslahi ya nchi na kuhakikisha kwamba Taifa letu linakuwa salama nyakati zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Elibariki Kingu, ahsante sana kwa mchango wako.

Sasa nimwite Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Thea, Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga ajiandae, baada ya hapo ajiandae Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uzima na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupambania afya za wananchi wa Tanzania na amekuwa mtekelezaji wa kwanza wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2020 – 2025, Ibara ya 83 inayosema "Kuhakikisha wananchi wanapata afya na siha bora." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri huyu Mheshimiwa Jenista Mhagama na Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Mollel; Katibu Mkuu, Dkt. Shekalaghe na watendaji wote wa Wizara hii ya Afya mpaka ngazi ya kijiji. Watu hawa wanafanya kazi kubwa sana kuhakikisha Watanzania wana afya njema. Watendaji hawa wameendelea kuwa na ari ya kufanya kazi na ninaomba waendelee kufanya kazi hiyo kwa uaminifu na tusonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninapongeza kazi kubwa zinazofanywa na watoa huduma za afya kule vijijini hawa *Community Health Workers* ni kazi kubwa sana. Ninaomba kama walivyoahidi wenyewe wataendelea kuongeza kada hii, ili waendelee kufanya kazi hii kwenye ngazi ile ya vijiji na mitaa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza kwa mageuzi makubwa yaliyofanywa kwenye Wizara ya Afya. Mageuzi haya nikitolea mifano michache tu, tunaona vifo vya wanawake wakati wa uzazi vimepungua kwa kiasi kikubwa sana kutoka wanawake 556 kwa kila vizazi hai 100,000 hadi kufikia vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000

mwezi Februari, 2025. Haya ni mageuzi makubwa sana na ndiyo yaliyofanya mpaka Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan akapata tuzo ile ya *The Global Goalkeeper Award*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili tunaomba vifaa viongezwe kwenye yale maeneo ya watoa huduma hawa wanaohudumia watoto na akinamama kwenye vile vyumba vya uzazi na huduma za watoto wachanga. Ninapongeza pia Wizara kwa kutambua kazi kubwa inayofanywa na wauguzi nchini Tanzania, tunaona ukurasa wa 144 mpaka 147 unaongelea kuhusu huduma za wauguzi nchini. Pia tunaona 80% ya huduma za afya zinafanyika na wauguzi na wakunga nchini Tanzania, hii kazi kubwa sana, tuwapongeze sana wauguzi na wakunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu katika eneo hili, ninaomba kuwe na elimu. Elimu iendelee kutolewa kwa wauguzi na wakunga kuanzia ngazi ya kijiji mpaka ngazi ya Taifa kwa kuthamini mchango wao wa huduma za afya katika nchi yetu. Pia hata maeneo yao yaboreshwe, kwa mfano kuna hospitali nyingi katika nchi hii bado wauguzi na watoa huduma za afya hawana maeneo mazuri ya kuishi (nyumba za kuishi) katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye Mkoa wangu wa Lindi, sisi Wana-Lindi tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuboresha huduma za afya, zahanati zimejengwa, vituo vya afya, hospitali za wilaya na hata hospitali ya mkoa, zimejengwa. Pia kuna huduma za *ICU* pamoja na huduma za dharura na vitendea kazi vimewekwa kwenye maeneo hayo. Tunashukuru sana kwa huduma hizo. Sisi Wana-Lindi tunashukuru, kwa maana huduma za *ICU* zinaokoa maisha. Pale ambapo mgonjwa anazidiwa sana, anapopewa huduma hizi za *ICU* (wagonjwa mahututi) inaboresha afya yake na pia inaokoa maisha yake. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hospitali yetu ya Mkoa wa Lindi pale Sokoine, majengo ni chakavu. Nimeona kwenye hotuba

ya Mheshimiwa Waziri kwamba majengo hayo yamehamishwa, yamejengwa majengo mapya kwa ajili ya uchakavu. Sasa ninachoomba jengo lile la hospitali ya mkoa ambayo ni ya rufaa, inayojengwa maeneo ya Mitwero, nimetembelea pale nimekuta bado majengo mengine hayajakamilika. Ninaomba majengo yale yakamilike ili huduma itolewe vizuri, kwa maana pale ilipokuwepo mpaka sasa hivi majengo yale ni chakavu sana, Hospitali ile ya Sokoine ya Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa eneo lingine tunashukuru kwa majengo yale ya *EMD* ambayo ni majengo ya huduma za dharura, pia na *ICU*. Pia tunaomba kwa sababu huduma hizi ni nyeti sana, tunaona kwa Mkoa wa Lindi wilaya nyingine zina *EMD*, lakini wilaya moja tu ndiyo ina *ICU*. Kwa unyenyekevu mkubwa sisi Wana-Lindi, tunaomba majengo yale ya *EMD,* pia hospitali zote zikamilike, kuwe na majengo ya wagonjwa mahututi, lakini pia na huduma za wagonjwa wa dharura kwa sababu hizi huduma ni muhimu sana katika huduma za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sisi Wana-Lindi tunashukuru kwa Madaktari Bingwa wa ile Kampeni ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tunashukuru wilaya zote wame-*cover,* wameenda kutoa huduma zile, hii imerahisisha wagonjwa ambao hawakuweza au wasingeweza kupata huduma za kibingwa kutokana na umbali au rasilimali fedha wamepata huduma zile kwenye wilaya zao, kwa kweli tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hawa Madaktari Bingwa wa Kampeni ya Dkt. Samia, imewezesha pia madaktari na watoa huduma katika hospitali za wilaya wamepata ujuzi na maarifa kiasi kwamba hata walivyoondoka bado wale waliobaki kutoa huduma kwenye maeneo yale wameendelea kuwa na ujuzi na maarifa kutokana na madaktari wale wa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la rasilimali watu; Mkoa wa Lindi ni mkoa uliopo pembezoni, lakini pia tuna changamoto nyingi,

tuna changamoto ya kuwa na rasilimali watu wa huduma za afya wachache, tukiacha huduma za madaktari bingwa. Tunaona Hospitali ya Mkoa wa Lindi tukianzia hapo Sokoine hakuna Madaktari wa Dawa za Usingizi, hakuna Madaktari wa Mionzi, hakuna Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani *(physician),* lakini hakuna Madaktari wa Magonjwa haya ya *ENT* (koo, pua na sikio), madaktari hawa wengine wameenda kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kabisa wale waliokuwepo sasa kuna upepo fulani ama kuna shida fulani ya kuhama, tunakuwa nao wakati fulani, lakini wanahama au wanahamishwa kwenda hospitali nyingine kubwa. Sasa ninaomba Mheshimiwa Waziri utakapokuwa unapanga mipango mbalimbali ya kuhusu kusambaza Madaktari Bingwa, ninaomba utukumbuke Mkoa wa Lindi katika hospitali yetu ile ya Mkoa ya Sokoine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi hii na ninapongeza kwa kazi kubwa ya Waziri huyu Mheshimwia Jenista Mhagama na tunamwombea kule Peramiho apate tena nafasi ya Ubunge na arudi tena hapa tuendelee kuchapa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tecla Ungele, umewasemea vizuri watumishi hasa wauguzi.

Sasa nimwite Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula ajiandae.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, nami nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha katika Bunge hili kwa miaka mitano sasa, ni baraka tu za Mungu na ni upendo wake. Pia nipende kuwashukuru

sana sana wananchi wa Mdunduwalo kwa sala zao na kuniombea nikaweza kuwa salama na mwenye afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi nyingi sana kwa Wizara ya Afya, Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu wake. Kijiji cha Mdunduwalo kilipata shida sana, ninajua Mheshimiwa Mbunge huyo ambaye ni Waziri, lakini na zahanati ile sasa imekamilika. Nikushukuru sana kwa sababu Wizara yako ilileta kile kifaa cha kuhifadhi dawa za chanjo, ahsante sana Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitoe pongezi kwa watendaji wako ambao ni wanafunzi wangu wazuri akiwemo Dkt. Mafumiko, pamoja na Dkt. Paul Muhame wa dawa asilia. Wale ni vijana wangu niliwafundisha *biology*, kwa hiyo una vijana wazuri ambao ni tunda langu hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niseme kwamba ninawapongeza na kuwashukuru Wabunge wote ambao mmenitia moyo wakati ninatetea vyuo vikuu akiwemo Mheshimiwa Profesa Muhongo, Mheshimiwa Dkt. Bashiru, Mheshimiwa Mama Anne Kilango, Mheshimiwa Profesa Manya; rafiki zangu akina Mheshimiwa Janeth na Mheshimiwa Esther Matiko, mmenipongeza na mlinitia moyo wakati ninapambana na eneo hili la vyuo vikuu, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nizungumze kama alivyozungumza Mheshimiwa Tecla, ma-*nurse* wanahitajika sana na tukumbuke kwamba ma-*nurse* wanahitajika sana duniani kote sasa hivi. Mheshimiwa Waziri ma-*nurse* katika dunia hii walifariki wengi sana wakati wa *Corona*, hata Tanzania ma-*nurse* wamepungua. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, sasa mjikite kwenye kuona kwamba ma-*nurse* wetu wanapata elimu ya chuo kikuu tena wawe wengi kama walivyofanya Aga Khan. Aga Khan wameweza kusomesha sasa ma-*nurse*. Kwa hiyo na sisi Tanzania tujikite katika kuona sasa ma-*nurse* wanapata elimu na waongezeke, kwa sababu idadi yao imepungua sana. Wewe unajua una zahanati nyingi

Tanzania, una vituo vya afya, una hospitali za rufaa, lazima ma-*nurse* wanaokaa muda mrefu na wagonjwa, waongezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia tena, ninaona sasa Waziri Mheshimiwa Jenista, wewe ni ndugu yangu, siyo tu ndugu wa hivi hivi, unajua wewe ni ndugu yangu, hebu acha *legacy* kwenye hili eneo la *teaching hospitals*. Naibu wako alijibu hapa alisema "ooh! Sasa hivi kuna ushirikiano mzuri na nini." Mimi ninakuomba leo utoe tamko, *teaching hospitals; MUHAS,* Benjamin pamoja na *UDOM*, wapate 80% ya kuhusika kwenye zile *teaching hospitals* zao. Mloganzila ichukuliwe kwa 80% na *MUHAS,* Benjamin nayo 80% na *MUHAS*. Maprofesa wako hapo wananisikiliza, wanajua umuhimu wa *teaching hospitals* kwa vile vyuo vyote vinavyofundisha masomo ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wameongea na mimi nimeongea, mimi ni daktari tu, lakini jana ameongea Mheshimiwa Profesa Muhongo, sasa hata Mheshimiwa Profesa Muhongo mawazo yake kweli hamyachukui? Ameongea Mheshimiwa Dkt. Bashiru. Hebu hakikisha sasa hivi unaacha *legacy*, watatucheka huko duniani. Ninaomba ulichukue hilo Mheshimiwa Jenista, lifanyie kazi na utoe tamko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nwenyekiti, nije kwenye hili suala la matumizi ya *P2*. Mimi nililiongea, sasa kuna watafiti wenzangu wamekaa wamelisema. Kuna Dkt. Jane Muzo anatoka Aga Khan, kuna David Myemba yeye anatoka *MUHAS*, wametoa madhara 10 ya *P2*. Kwa ruhusa yako kuna Wabunge hapa hawajui hizo *P2*, hawazijui kabisa. Hapa nina hizo *P2,* ninaomba utume mtu aje azichukue, Wabunge wazione, waone watoto wao wakiweka kwenye meza wasione kwamba ni kidonge cha kawaida, wazijue hizi *P2*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara yake, Waheshimiwa Wabunge nisikilizeni; hizi *P2* kwa sababu zinatumika hovyo bila elimu Mheshimiwa Jenista, ninaomba mtoe elimu ya wazi kabisa. Ninakwambia hiki kizazi kitapotea. Mabadiliko ya mzunguko wa

damu na kiharusi, kwa maana wanatumia hovyo, wanaweza wakapata *stroke*, hii ni kutokana na utafiti wa hawa niliowataja, wanaweza wakapata *cancer* ya uzazi, mimba zinaweza zikatoka mara kwa mara, wakati mwingine wanapata damu nyingi na wakati mwingine wanapata damu kidogo *(spot),* wakati mwingine wanapata hata magonjwa ya zinaa.

Kwa hiyo, hili suala nimelizungumza kwa sababu juzi tu kuna mama mmoja alitoka Arusha, wale walioalikwa kwenye chama, akaniambia; "Mheshimiwa hivi mnaongelea hili suala la *P2*." Sasa ujue kumbe hata akinamama wameanza kuogopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la *P2* tusifanye mzaha Mheshimiwa Jenista, angalia namna gani mtatoa elimu bora ya matumizi hayo kwa sababu inaonekana kuna hasara zaidi kuliko faida. Nimelisema hilo na ninaomba Waziri sasa mtalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ninaweza kumalizia ni kuhusu huu Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote. Kuna hivi vipimo vya *CT-Scan*, *MRI* na *Dialysis.* Walisema wenzangu, hivi vitu tulienda pale Temeke hivi vipimo ni ghali sana, kuanzia shilingi 200,000 na kuendelea. Sasa nimwombe Waziri, hii elimu ya Bima ya Afya kwa Wote bado, itoeni hii elimu ili vipimo hivi watu wote waweze ku-*afford*. Kukiwa na Bima ya Afya mtu ataweza kupima, lakini *otherwise* ninawaambia zile mashine ziko pale zitawasaidia tu watu wenye pesa. Kwa hiyo, mtoe elimu ili angalau watu waweze kujua sasa Bima ya Afya kwa Wote itasaidia nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaomba kwenye tiba asili, Serikali mshirikiane na watu waliotusaidia. Leo kuna mtu anaitwa Shekilindi, amesaidia sana watu wakati wa *Corona*, dawa ya kisukari, magonjwa ya meno; kuna rafiki yangu mmoja ananiangalia pale, sijui ni Mheshimiwa Mariam Nyoka. Sasa msaidieni huyu, mshikane naye, Shekilindi anasaidia sana, watu wanakwenda pale anasaidia, je, Serikali kwa nini msimhusishe huyu? Mtafute Paul Muhamepamoja na wengine na muwashirikishe Shekilindi aweze

kusaidia watu katika magonjwa ya kisukari, meno, *pressure* na magonjwa mengine. Sasa watu kama hawa wanafanya kazi nzuri, tunawafuata tu wakati wa *Corona*, hebu muwashirikishe asaidie kufanya hiyo kazi ili tuweze kuepukana na magonjwa haya madogo madogo, msione aibu. Tezi dume watu wanaona aibu, jamani wanaume wenye tezi dume mwende mkamwone Shekilindi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Waziri nikuombe hebu toa tamko zile dawa za kuua vizalia vya malaria, kidogo nimalizie hapo. Zile dawa za kuua vizalia vya malaria, hivi wakurugenzi mliwaaagiza je, wameenda kuchukua? Mpaka lini sisi tutateseka na hii malaria? Waende wakachukue zile dawa pale Kibaha, tutokomeze malaria. Yaani ninyi mnawaagiza humu ndani, lakini wala hawaendi kuchukua. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri hebu pambana nao, waambie, utoe amri wakachukue dawa, zisambaze kwenye sehemu ambazo mbu wanazaliana ili tuepukane na malaria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, kwa mchango wako mzuri. Sasa nimwite Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji ajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi ya kuchangia Wizara yetu ya Afya. Ni bahati njema kusimama mbele ya Bunge lako leo kuunga mkono mafanikio makubwa ya Wizara yetu ya Afya chini ya mama yetu Mheshimiwa Jenista Mhagama, Naibu Waziri wake na Wakuu wake wa Idara katika Wizara yake na viongozi wote wa Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaanza kwa kuunga mkono hoja. Nimemsikia Mheshimiwa Waziri akisoma hotuba hapa akiomba

shilingi trilioni moja *point* sita na kidogo. Ameeleza mafanikio makubwa ya bajeti iliyopita na mipango na mikakati ya bajeti ijayo. Mfano, ameelezea vizuri mafanikio ya utalii wa afya. Kwa mara ya kwanza nchi ya Tanzania ambayo ilikuwa inasemwa vibaya huko nyuma, leo kuna watu wanatoka maeneo mbalimbali kuja kutibiwa Tanzania, hayo ni mafanikio makubwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yetu haya ni lazima sisi wenyewe Watanzania tuendelee kuyapongeza, tuendelee kuyashukuru kwa sababu kwa vyovyote vile hakuna mtu atakayekuja kuongoza nchi moja na siku moja tutapata mafanikio ya kila kitu. Hata hawa wanaotaka kukitoa Chama Cha Mapinduzi na wanaosema vibaya nchi yetu na viongozi wetu, hata ukiwa hapa nchi hii wao hawawezi kumaliza yote kwa wakati mmoja. Changamoto za maendeleo tunasema zinatokea wakati wowote mpaka mwisho wa maisha. Mimi ninamshukuru sana na nitasimama na Rais wangu potelea mbali, liwalo na liwe katika changamoto zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa nachangia masuala ya afya, nataka kusisitiza na kukumbusha maneno ya Sheikh wetu mmoja wa Mkoa wa Dar es Salaam, Sheikh Walid Alhad. Sheikh Walid anasema kwamba anatusisitiza duniani huku unaweza ukaviheshimu vitu vingi sana na kuviogopa, lakini Sheikh Walid anasema jaribu kuheshimu sana moto, maji na mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheikh Walid anasema nawakumbusha Watanzania kwamba nchi hii inaongozwa na mwanamke, sasa msichukulie poa. Kwa hiyo, nami nataka kumkumbusha mtu yeyote mzee mchekea mwezi sisi waswahili tunasema ni muhimu sana ukazingatia hayo kwamba Mheshimiwa Rais wetu ni mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Afya ni mwanamke, ni mama jasiri, umekuja jimboni kwangu wewe na amekuja Mheshimiwa Naibu Waziri kabla hujaja Mheshimiwa Waziri

wa Afya, umekuja jimboni kwangu na Mheshimiwa Naibu wako amekuja jimboni kwangu, kabla hujaja Mheshimiwa Waziri wa Afya alikuja Naibu Waziri Mheshimiwa Mollel, akanifanyia siasa kubwa sana pale jimboni kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka nimkumbushe ahadi yake moja nzuri aliyonisaidia kufanya pale, lakini wakati amekuja alitembelea pia *St. Francis Hospital* na alitembelea hospitali yetu ya kansa. Nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri wakati ule Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya amekuja alikuta changamoto kubwa sana katika hospitali yetu ya Rufaa ya *St. Francis* na ndiyo maana wakati nauliza swali la nyongeza nilizungumzia kuwashukuru kumleta Mkurugenzi wa Hospitali yetu ya Rufaa mwanajeshi, askari *Mr. Fusi. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna mafanikio makubwa sana Mheshimiwa Waziri yametokea katika Hospitali yetu ya *St. Francis* kwa sababu ni hospitali ambayo Serikali inashirikiana na kanisa na sisi mpaka tufikie *level* ile itakuwa bado hatua ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka niwape pongezi nyingi sana kwa kumleta yule *Comrade Fusi* ili muone namna ambavyo mnaweza kumuongezea muda wa kubaki pale katika hospitali ile. Mara zote tulikuwa tunasikiliza maoni ya wananchi wakilalamikia Hospitali ya *St. Francis Referral* ya Ifakara, Malinyi, Ulanga, Mlimba Ifakara yenyewe Mikumi huku kote watu ambao hawawezi kwenda Morogoro katika Hospitali yetu ya Rufaa ya Morogoro wanatibiwa katika *St. Francis Hospital. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka nikwambie yale malalamiko ya rushwa, uuzaji wa damu *Mr. Fusi* amekomesha. Nakutana na wazee wananiambia wanapokelewa na ma-*sister* pale wa kanisa wanahudumiwa, *Mr. Fusi* ameboresha kitengo cha mapokezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amejaribu kufanya *St. Francis* sasa inashirikiana na taasisi nyingine zote na hapa, kitu kikubwa ninachojifunza Mheshimiwa Waziri wa Afya kama kuna maeneo magumu basi ongea na Mheshimiwa Waziri wetu wa Ulinzi hapo awe anakuletea watu kama wale na hizi salamu zangu mzipeleke kwa *Comrade CDF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama namtania na kumdanganya Mheshimiwa Waziri wa Afya pita Ifakara sasa hivi uliza mpaka bodaboda wa nje ya hospitali ameshawaita, amewajengea umoja, sasa hivi anawajengea banda pale. Ni mkurugenzi mzuri mmetuletea kama kweli Jeshi letu lina watu wa namna ile basi sehemu zote zenye utata utata hivyo ni vizuri mkapeleka watu kama wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwa hiyo, nakupongeza sana nami mswahili nikitaka kukupongeza Mheshimiwa Waziri nasema wewe ni mwanamke wa *mbeko,* mwanamke wa *ulua, maslahi shamsi, mbeja* mwenye umbeja Mwenyezi Mungu aendelee kukujalia baraka tele uendelee kuiongoza Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatusemi yale ambayo tunakuona kwenye vyombo vya habari huko ukimpigania Profesa Janabi, ukiwaapigania viongozi wengine waendelee kuchukua nafasi duniani, lakini kwa mambo makubwa ambayo unayafanya katika sekta yetu ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla sisi katika Jimbo la Kilombero, Halmashauri wa Mji wa Ifakara Mheshimiwa Dkt. Mollel alivyokuja pale Mheshimiwa Waziri, tulitembelea kituo chetu cha Afya ya Kibaoni na Mheshimiwa Naibu Waziri tukamwambia Kituo chetu cha Afya cha Kibaoni ni kituo ambacho kinahudumia watu wengi sana, tunashukuru Serikali tumejenga Kituo kingine cha Mbasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri alituahidi kwamba tutapata shilingi milioni 300 za kupanua Kituo cha Afya cha Kibaoni na kujenga Jengo la Wagonjwa wa Nje mnasema *OPD,* zile fedha mpaka leo hazijaja Mheshimiwa Naibu Waziri, nakukumbusha hapa mbele ya Mheshimiwa Waziri kwamba ni muhimu sana ukatusaidia zile fedha zikaja Kituo cha Afya cha Kibaoni kikaweza kujengewa Jengo la *OPD* na kwa namna yoyote ile tukaweza kupata huduma bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kushauri kwamba Wizara ya Fedha ipeleke pesa kwa wakati katika Wizara ya Afya kwa maana afya ni bora kuliko magari, wakati mwingine kuliko hata barabara. Kwa hiyo, kama Wizara ya Fedha nimeona kwenye Kamati hapa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Afya anasema uendaji wa fedha katika Wizara yako si mzuri, naomba fedha ziende kwa wakati na hasa kwenye *MSD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hivi hamuwezi kugawa dawa zote hizi zinazotakiwa kuhudumia ni kwa wakati mmoja kwa mfano sisi Halmashauri ya Mji wa Ifakara, Jimbo la Kilombero, Wilaya ya Kilombero mnaweza mkajua dawa muhimu na magojwa muhimu yanayotukabili wananchi wetu wakapata dawa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naunga mkono hiki kifurushi cha shilingi 168,000 ambacho hata jana nimemkatia mwananchi wangu mmoja wa Kibelege pale. Kukatia hizi bima kama kweli tunajihakikishia tunapata dawa na huduma wananchi wetu wapo tayari, nami nitashiriki kutoa elimu na tunaomba bei ya mpunga mwaka huu iwe nzuri. Bei ya mpunga ikiwa nzuri mwananchi akiuza gunia moja la mpunga atalipia kifurushi cha shilingi 168,000; lakini akienda katika kituo cha afya, akienda katika hospitali basi apate tiba ya kutosha ili aone gunia lake la mpunga limeenda kihalali. Sambamba na wazee wetu wapate tiba nzuri kabisa za kutibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata mafanikio makubwa sana, tumejenga vituo vya afya viwili kwa maana ya *Msolwa Station* na Mbasa kwa kushirikiana na Madiwani na viongozi wa vijiji na viongozi wa mitaa; tuna zahanati 12 ambazo hizi zinawezekana zipo TAMISEMI Mheshimiwa Waziri wa Afya, lakini tunaomba *MSD* iwezeshwe. Nafahamu *MSD* imefanya kazi kubwa sana kwetu, kwa maana kwamba kwa mfano Kituo cha Mbasa kabla hakijaisha vifaa vimekuja. *Msolwa Station* kule kabla hakijaisha vifaa vimekuja, Hospitali yetu ya Halmashauri ambayo tuna mpango nayo iende kuwa hospitali kubwa zaidi hata baadaye tukipata mkoa mpya imepata vifaa na wataalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, wataalam katika hospitali yetu ya halmashauri bado hawatoshi. Naomba sana mtuongezee wataalam katika Hospitali yetu ya Kibelege, na Mheshimiwa Waziri wa Fedha akiwaletea fedha basi mtusaidie kuboresha mpaka tupate *fence* katika hospitali ile ambayo kwa kweli itasaidia sasa wananchi wa jimbo zima na hata wale watakaoshindwa kutibiwa Ulanga, sasa Malinyi na Mlimba wanaweza wakaja pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusisitiza kwa kumalizia kwamba suala la bima ya afya ni suala la msingi sana na leo Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Afya ametuambia kuhusu kifurushi cha shilingi 168,000. Nami nataka kusisitiza inawezekana shilingi 168,000 imeshushwa kutoka shilingi 300,000. Mimi nilishanunua vifurushi vya shilingi 300,000, shilingi 240,000 sasa tuna shilingi 168000 ndiyo watu wa bima ya afya wameweka *class* kama *SGR* ukitaka kupata shilingi 150,000 ukitaka kupanda cha shilingi 100,000; cha ngapi unapata, sisi tutalipia sana watu wetu hiki cha shilingi 168,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kipunguzwe zaidi, lakini la msingi hata kikibaki shilingi 168,000 nataka kusisitiza ni muhimu sana katika afya watu wakapate dawa, watu wakapate huduma kuna baadhi ya maeneo kumekuwa na tabia ya watu wafuate huduma

sehemu fulani, hili bado jambo linafanyika sio kwa watu wote, lakini kwa baadhi ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Halmashauri ya Ifakara Dkt. Erasto - *DMO* wetu amepunguza kwa kiasi kikubwa sana jambo hili, lakini kuna baadhi ya maeneo unakuta kuna malalamiko, nilisema pale Mbasa, naona sasa hivi yameboreshwa huduma imeanza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mtusaidie dawa za msingi zipatikane. Kwa mfano sisi labda tunasumbuliwa sana na malaria kutokana na bonde letu la maji, dawa za malaria zinazotibu watu wetu zisikosekane, mkifanya utafiti kuna magojwa mtayagundua Ifakara ambayo dawa zile zipatikane kwa bei rahisi, mtu asiende akatibiwa, akapimwa malaria au kichocho ama nini akaambiwa tena dawa mpaka akanunue tena kwa gharama kubwa zaidi, ndiyo maana hata ile bima ya mwanzo ya jamii kule haikufanya kazi vizuri ndiyo hii bima ya shilingi 168,000 itafanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *challenge* ya kutibu watu ni kubwa, ninajua kisa hata cha Mwalimu Nyerere anasema amekaa nyumbani kwake pale wakati anasikia haya mambo ya kulipa gharama za matibabu na yeye alikuwa anaamini tiba ni bure, anasema ameletwa mtu anaanguka kifafa, lakini anaambiwa hana pesa akalipe, sasa tutafanyaje katika nchi yetu, tunaendelea kuzaa, tunaendelea kuzaliana, tunaendelea kuwa wakulima wazuri, lakini sisi sote tunataka huduma ya afya bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna gani maskini wa nchi hii, kuna watu maskini kule chini. Mheshimiwa Mbunge unatoka nyumbani unasema leo sitoi hata mia, unakutana na mtu nje hali yake ngumu, akiumwa ukimpeleka hospitalini; juzi nimekutana na mama mmoja ameungua moto mguu kwenda kumcheki tu shilingi 300,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lazima tuangalie kwa ujumla namna gani Mtanzania ambaye hana uwezo hata shilingi 168,000

hii. *DC* anaweza kupewa mamlaka ama Mkurugenzi wa Halmashauri akijiridhisha na Mganga wa Wilaya akatibiwe kwa barua yao bure tuwasaidie Watanzania wetu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ajiandae.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa nami nichangie katika hoja hii iliyopo mezani. Nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kuweza kupata nafasi siku ya leo kuja kuchangia hapa. Nami niungane na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kusema kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na njema ambayo ameifanya katika kubadilisha kabisa sekta hii ya afya ambayo ilikuwa na changamoto nyingi, lakini kwa sasa imeweza kuhudumiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Waziri, Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na Naibu wake kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya. Kwa kweli Mheshimiwa Jenista ni kiraka kama Mheshimiwa Rais alivyosema kwamba katika Waheshimiwa Mawaziri kiraka wake mmojawapo ni Mheshimiwa Jenista, kweli umeonekana ni kiraka kwa sababu kila unapowekwa una-*fit,* hongera sana Mheshimiwa na Peramiho walisikie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia maeneo machache tu kwanza kupongeza sana programu ile ya madaktari bingwa wanaotembea katika maeneo na kutoa huduma, kwa kweli huduma ile imekuwa ni njema sana kila wanakokwenda wanaacha faraja kwa wananchi na wengi wanakuwa wana magonjwa pengine ambao wameshindwa kuhudumiwa katika hospitali zingine za kawaida kutokana na kutokuwa na pesa, lakini huduma hii

imeweza kuwabeba kwa kiasi kikubwa hongera sana Mheshimiwa Rais kwa kuja na mawazo chanya mawazo ambayo yanagusa mtu wa kawaida kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine napenda tu kukumbushia Wizara, Hospitali ya Kanda ya Bugando ni hospitali ambayo inahudumia karibu mikoa nane, lakini pia nishukuru Serikali kwa kuiteua pia kufanya huduma ya saratani na kuweza kuwekeza pale kwa kuweka jengo kubwa na zuri, kuweka miundombinu ambayo inaweza kuwekewa zile mashine kwa ajili ya saratani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya pale kidogo inasuasua kutokana na mashine zilizopo pale zinashindwa kukidhi mahitaji ya watu na mashine inafanya kazi mpaka masaa 16 na inapokuwa imezidiwa haiwezi tena kuendelea kufanya kazi. Kwa hiyo, unakuta ile azma nzuri ya Serikali ya kusogeza huduma kwa wagonjwa wa kanda ile inakuwa tena haina maana kwa sababu mashine ile inapokuwa imezima wanalazimika kuwapeleka *Ocean Road,* jambo ambalo ni changamoto kubwa sana kwa wagonjwa katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana kwa sababu kumekuwa na ahadi nyingi na mara ya mwisho Waziri Mheshimiwa Jenista alihudhuria pale Mwanza walipokuwa na *function* yao, pale Bugando na akaahidi kwamba watasaidia katika kuwaletea mashine zingine hasa ile mashine wanayoita *linear accelerator* inatakiwa sana, nadhani Mheshimiwa Dkt. Mollel anafahamu vizuri sana kwa sababu ni mtaalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana msaidie Hospitali ya Bugando kwa sababu inazidiwa, lakini huduma ile inahitajika sana na wote mlikuwa mnaona tulivyokuwa tunasema kwamba wagonjwa wengi Kanda ya Ziwa wanakuwa wanaonekana pale *Ocean Road.* Sasa kwa kusogeza huduma basi tuiwezeshe na ile hospitali iweze kufanya kazi kuweza kukidhi mahitaji ambayo yapo,

na kwa nyakati tofauti tofauti viongozi kila akienda wanaahidi, kila wakienda wanaahidi. Niombe sana basi ahadi hizi zikatekelezwe ili hospitali ile iweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la wataalam, madaktari bingwa ambao wanapangwa katika hospitai zetu za wilaya wataalam wale wanastahiki zao kulingana na utaalam ule. Sasa anapokwenda wilayani wakati mwingine anapangwa hata kwenye kituo cha afya kwenda kufanya kazi pale, sasa unakuta ile huduma ya ushauri ile *consultation fee* hawezi kuipata kama anavyopata siku zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ningeomba kwa sababu sasa tunawapeleka mpaka kwenye hospitali za chini waweze kupata stahiki zao kulingana na ujuzi walionao ili tuweze kuwatia moyo katika suala zima la kuona ni namna gani tunaweza pia kuwatia moyo hata wanapokwenda kutoa huduma sehemu ambazo ni za chini kabisa katika huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kutoa pongezi kwa Wizara katika ile huduma wanayoitoa kwa kutoa mtoto tumboni, nadhani ni kwa uzazi wa *operation*. Naomba nitoe ushauri hapa kuongezeka kwa huduma hizi sioni kama zina tija sana kwa sababu sasa hivi vijana wengi wanashawishika kujifungua kwa njia ya *operation,* anaogopa kujifungua kwa njia ya kawaida. Kwa hiyo kadri tunavyoongeza hizo huduma nadhani pia tunaleta ushawishi na anapojifungua kwa *operation* nadhani kuna *limit* ya watoto na sidhani kama Tanzania tumefikia wakati na kuwa na watoto labda mmoja au wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningeomba ushauri zaidi utolewe kwa mabinti ni namna gani anaweza akabeba ujauzito, akafanya mazoezi gani na katika kujifungua akajifungua kawaida ili tuwaepushe na uzazi wa *operation* kwa sababu uzazi wa *operation* una *limit* utakwenda watoto wawili, watatu halafu basi huwezi kuongeza tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana kwa sababu hapa inaonekana huduma zimeongezeka kutoka 388; mwaka 2021 mpaka kufikia 577 Machi, 2025. Kwa hiyo, bado pia ni nzuri imeongezeka, lakini haina tija kwa watu wetu kwa sababu kuna *limitation* tunaweza tukawa tunapunguza idadi yetu kwa kuweka kipingamizi hicho cha wazazi kujifungua kwa *operation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie suala la watoto wenye uzito pungufu ambao nao wanaongezeka kutoka 80 mpaka kufikia 365. Huduma hii inapatikana katika hospitali zetu za wilaya 200; umesema kwenye taarifa katika hospitali zetu za wilaya 318 bado pia ushauri upo pale pale kwenye masuala ya lishe inakuwaje mtoto anazaliwa akiwa na upungufu wa uzito? Tunahitaji kuwafundisha watu wetu pia katika suala zima la lishe, bila kufanya hivyo tutazaa watoto wenye uzito pungufu, lakini pia afya zao zinakuwa siyo nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado nalo hili nishauri wakunga wetu, manesi wetu wanalo jukumu kubwa la kushauri sana katika suala zima la lishe ili tuweze kuona ni jinsi gani tunaweza kuepukana na watoto hawa wanaozaliwa na upungufu mzito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie utalii wa tiba; kwa kweli nimpongeze na hongera nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais kwa kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika zile hospitali za kanda na hospitali za rufaa. Tumeona nchi zaidi ya nane wanakuja kutibiwa hapa, kwa hiyo, kama tunaweza kupata watu kutoka nje maana yake huduma zetu hapa ni nzuri, huduma zetu zinafaa na mpaka zinawavutia nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niweze tu kupongeza na kusema kwamba tuongeze bidii katika kuboresha huduma hizi ili tuweze kupata wagonjwa wengi wanaokuja kwa kutibiwa hapa ambao tunaita ni tiba ya utalii ambayo inasaidia sana katika kuleta pia pesa za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la matibabu ya Waheshimiwa Wabunge nje ya nchi. Nadhani tuna hospitali yetu kule India ambayo mara nyingi tunaenda, naomba nishauri sana, Serikali ione namna ya kuongeza nchi zingine ambazo zinaweza kuleta kutibu wagonjwa badala ya kujikita katika hospitali moja ya India. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema India ni mabingwa kweli, lakini pale unapokwenda msongamano wa watu ni mkubwa mno, kwa hiyo, kunakuwa na changamoto pia katika suala zima la kupata matibabu. Kwa hiyo, ningeomba sana hili lifanyiwe kazi ili watu waweze kupata *option* ya kwenda kutibiwa katika maeneo mengine kutokana na hali halisi ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niongelee suala la jimboni kwangu tunacho Kituo cha Afya cha Buzuruga, kituo kile ni kikubwa sana kwa sasa kinafanya kazi kama hospitali ya wilaya na tunatambua hasa katika vituo vya afya wagonjwa wanatakiwa walau 10,000 hawazidi sana hapo, lakini kituo kile kwa sasa kinatibu watu zaidi ya 200,000 kwa mwaka sasa uone kwamba ni namna gani hapo tunavyofanya siyo kwa mwaka kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba tuone ni namna gani tunaweza kukipandisha hadi walau hata katika kutoa huduma za pale waweze kupata vifaa tiba na mambo mengine ya dawa sawa na hospitali ya wilaya kwa sababu wanatibu wagonjwa zaidi ya uwezo wake na kituo kile ni kikubwa na ni tegemeo kubwa sana katika wilaya, lakini pia katika kata za jirani ambazo zinatoka katika wilaya jirani ya Nyamagana, niombe hili kwa sababu imekuwa na changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la kutibiwa kwa wazee, tumesema wazee kweli wanatibiwa bure, lakini pia sheria inge-*categories* ni wazee wa aina gani kuna? Kuna wazee wengine wana uwezo wa kuweza kujitibisha, lakini kuna wazee wengine ambao hawana uwezo kabisa, lakini unakuta naye pia anapata

changamoto akifika pale hapati matibabu anayostahili kwa sababu tu pengine ya kutoelewa watoa huduma au namna ya sheria yetu ilivyokaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuweze ku-*categories* kuona ni wazee wapi? Kwa sababu unaweza ukasema kuanzia miaka 60, miaka 60 wengi tu hata ni miaka zaidi ya 60 naweza nikasema na mimi nitibiwe bure, lakini kumbe nina uwezo wa kufanya hivyo. Kwa hiyo, tuangalie na tuweze ku-*categories* ni wapi ambao wanastahili kuweza kufanyiwa hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niombe kwa Wizara, tunahitaji pia kuwa na *ambulance* katika vituo vyetu vya afya hatuna *ambulance* katika maeneo hayo tuliyonayo kidogo imechoka na tuna vituo vya afya vitano. Sasa katika vituo hivyo vyote kama *ambulance* ni moja na nyingine inasuasua kidogo, ni changamoto, niombe sana haya ili tuweze kuona tunakwendaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais ambaye amepewa tuzo ya *Bill Gate Keeper* wanasema ya *goalkeeper* ambayo amepunguza vifo vya kinamama wajawazito. Kwa kweli nampongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu tulikuwa na vifo vingi na vimeshuka mpaka 101. Niombe tu watumishi wetu waendelee kufanya kazi kwa bidi, vifo vipungue walau tubaki na *digit* mbili au moja ikiwezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, ameshaonesha uhodari na kupewa tuzo, basi tuendelee kupunguza vifo hivyo ili tuweze kuwa na huduma nzuri kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na napongeza kwa kazi nzuri wanayofanya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mabula kwa mchango wako, nimuite sasa Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mheshimiwa

Boniphace Mwita Getere atafuatiwa na Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray ajiandae.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa ruhusa yako hii sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue fursa hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia kuwa na hali ya uzima na afya na hivi sasa nimesimama hapa ili nichangie Wizara ya Afya. Ninamshukuru Waziri Mheshimiwa Jenista pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dkt. Mollel, Mawaziri hawa wanafanya kazi vizuri sana na wanaisimamia hii Wizara ya Afya hasa katika hospitali zetu humu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kuna baadhi ya mambo mengi humu hospitalini yamepungua kweli kutokana na hii Wizara jinsi inavyofanya kazi, lakini kuna baadhi ya mambo mengine bado yapo na yanaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa katika ajenda yangu nataka nizungumzie kuhusu afya ya jamii; afya ya jamii bado kabisa kuna baadhi ya hospitali ukienda hata kama unayo ile bima ya afya bado wanataka uwape na chenji kidogo ndipo unapopata zile dawa, kama si hivyo huwezi ukapata dawa, maana ile bima ya afya wanasema mpaka sasa hivi wanasema dawa zetu hazikidhi kutokana na hii bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna baadhi ya wananchi wetu humu nchini, wanyonge na maskini wana bima zao za kinyonge kabisa, wale ndiyo hawapati dawa kabisa, utamuona mtu anatoka hospitali na unyonge hana pesa ya kwenda kujihudumia, yale maradhi yanazidi kumuumiza. Kwa hiyo, Waheshimiwa Mawaziri, naishauri Serikali hili suala la bima lisimamiwe na liweze kufanya kazi vizuri humu katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea kuna tiba ya afya humu nchini, hasa tiba ya jamii, tiba hii ya jamii wenzangu humu wameizungumzia, kuna baadhi ya hospitali zile kubwa zinawatoa madaktari kwenda kupima afya ya jamii katika maeneo yetu humu nchini. Mimi ninaishukuru sana Serikali yangu hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali yetu pia kule Zanzibar kwa kulisimamia hili la baadhi ya kwenda kuwapima afya ya jamii watu huko wanakokaa maeneo yao, kwa sababu wenzetu kule wanakaa, wanafanya kazi zao, lakini kumbe wana maradhi ndani kwa ndani yanawaumiza hawajui, lakini ninapokwenda kule afya ya jamii wanapopimwa wanagundulika na yale maradhi, hasa *pressure*, sukari na baadhi ya maradhi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nishukuru fursa hii, kwa kufanya hivi wazidi kufanya vizuri ili hawa wananchi wawatoe kule nchini, kule nje ili waweze kwenda kutibiwa katika hospitali zile na wanapogundulika kama wana maradhi madogomadogo basi kama kuna dawa wanakuwa wanapewa dawa bure. Kwanza nishukuru sana katika Serikali zetu hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea kuna maradhi ya sukari, *pressure* na shinikizo la damu, maradhi haya yanakuwa siyo ya kuambukiza, lakini haya maradhi sugu, baadhi ya maradhi haya wengine tuliokuwa nayo humu, basi kama kipindi hiki cha baridi unapata taabu sana. Haya hayataki ufurahi, haya hayataki unune, hayataki baridi sana, hayataki joto sana. Haya maradhi ni maradhi sugu. Vyovyote unavyoishi maradhi haya basi utakuta yanakuathiri katika mwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba kuna baadhi ya hospitali ukienda unakuta dawa, lakini kuna baadhi ya hospitali zingine wanakuwa hawana dawa. Wale wananchi wetu kule wanapata taabu, wenye maradhi haya ya sukari na shinikizo la damu wanakuwa wanaathirika na wanarudi nyumbani wengine wanafikia kufariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, nakuomba hili suala mlisimamie ili hawa wananchi wetu waweze kwenda kutibiwa maradhi haya ya sukari, *pressure* pamoja na shinikizo la damu, maana baridi hii tena watu wanaanza kuganda damu mwilini. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, hili ndilo ninaloliomba kwa sasa hivi kuishauri Serikali yangu ifanyie kazi wagonjwa wetu wa sukari na *pressure* wajisikie wawe tayari kufanyiwa matibabu na wajione kwamba hivi sasa niko afadhali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya hospitali, kuna nchi za wenzetu hawa humo nchini wanakuwa wanahudumia sana wake zao, wanahudumia sana wake zao hasa wanapokuwa wajawazito, wanawaendeleza wake zao mpaka wanafika kujifungua, wanawasimamia mpaka wanafika kwenda kujifungua kule hospitali wanakwenda wale wanaume, lakini hapa nchini baadhi yetu hawana mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu akishampiga mimba mtoto mwanamke hata kama mkewe basi hawezi kumshughulikia, anamuaacha kama alivyo, umefika muda Mungu kamsalimu salama anazaa imekuwa pale basi, lakini ninakwambia hili suala nalo vilevile lisimamiwe hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaume wapewe elimu, waweze kwenda kuwasimamia wake zao hasa wakati wa kwenda kujifungua. Yule mtoto anapotoka kwenye tumbo la yule mama basi baba awepo pale amuone jinsi anavyoathirika yule mwanamke, imuingie imani ya kuweza kukaa na mkewe vizuri. Wanaume humu wanatutelekeza, tunapochukua mimba hatuwezi kushughulikiwa na wanaume wetu, hata kama ile dawa basi hawezi, ukimwambia mume wangu mimi sina dawa nisaidie nipate angalau hii dawa ya damu tu mwilini, anakwambia mimi pesa sina! Kwa nini umeenda shirikisha lile suala mle ndani, kwa nini? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hili lisimamieni muweze kulifanyia kazi, wanawake waweze kuzaa vizuri na wanaume wao kule hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho ninalotaka kuzungumzia, kuna baadhi ya hospitali, kuna maradhi, kuna ushirikishwaji kwenye hatua za watoto. Watoto wetu humu nchini baadhi, hasa wale watoto njiti, watoto njiti wakishazaliwa wale wanataka huduma nzuri sana, ukifanya masihara mtoto yule atakwenda na maji. Muda wote wakishazaliwa wanakuwa wabovu watoto wale, hawawi wazima na ndiyo tunapoomba walelewe kule hospitali, wanapolelewa kule hospitali, kama kwa baadhi ya miezi miwili/mitatu kisha wale watoto wapewe wazee wao waende nao nyumbani kwa kwenda kumfanyia huduma nyingine, pale inakuwa afadhali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto njiti akishazaliwa akipewa mzazi inakuwa shida na hili ndilo lililokuwepo, mtu akishamzaa mtoto wake njiti anakaa wiki tu hospitali na huko nyuma wanakaa zaidi ya miezi mitatu kisha ndipo mtoto wake anapewa. Kwa hiyo, nashauri hili nalo Serikali ilisimamie suala la watoto njiti ili waweze na wao kupata uhai, waishi kama sisi wazee wao waje wafanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja asilimia mia moja, ahsante sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, ahsante sana Mwenyekiti kwa ruhusa yako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji kwa mchango wako. Nilimuita Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, atafuatiwa na Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray. Wafuatao wajiandae, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Selemani Kakoso.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najiuliza maswali hapa wakati Wabunge wanachangia, nikajiuliza swali moja, hivi ikitokea kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limekataa

kupitisha bajeti ya Wizara ya Afya hivi kutatokea nini? Tutaenda kugombea au tutakaa humu Bungeni? Maana yake si wananchi wote huko watapata matatizo? Kwa hiyo, hii ni Wizara ambayo inaitwa mtakuja, kwa hiyo, haina namna yoyote ya kutounga mkono Wizara ya Afya ili watu wetu waendelee kupata afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwanza mimi naunga mkono hii Wizara kabla sijaendelea kwa sababu siwezi kwenda huko wakaniambia watu wamekufa huko tena nikaanza kupiga simu kwa Mheshimiwa Jenista, haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Jenista na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dkt. Mollel, Katibu Mkuu, Mganga Mkuu wa Serikali na watumishi wote wa Wizara ya Afya. Kimsingi, sasa sijui Mheshimiwa Rais huwa anaona, huwa anaona nikimweka huyu na huyu watakuwa sawa, maana Mheshimiwa Dkt. Mollel yeye mawazo yake yote wala siyo kutafuta madaraka, mawazo yake yote Mheshimiwa Dkt. Mollel ni namna ya kutafsiri vifungu vya dawa na vifungu vya afya ndiyo akili yake. Namna umpigie simu, ukimpigia simu Mheshimiwa Dkt. Mollel ya kumsaidia mtu anaona ndiyo wito wake, hapo hapo atapiga simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ameingia dada yangu Mheshimiwa Jenista na yeye ni hivyo hivyo. Kwa kweli mioyo yao labda Mungu ndiye anayejua kwenye mipango yao. Wana mioyo ya ki-Mungu tunawaombea waendelee kuwepo watusaidie. Kwa kweli tunaomba watu wa majimbo yenu wasikie Wabunge tunasema nini, wasiwasumbue wawaache mje mtusaidie nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Rais, kwenye Jimbo langu ninayo Hospitali ya Wilaya ambayo imejengwa kwa zaidi ya shilingi bilioni 4.6 na sasa tumepewa shilingi milioni 680; shilingi milioni 680 itaenda kumaliza Hospitali ya Butiama ya Wilaya, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu ilikuwa imekwama

kidogo, sasa itaenda kumalizika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata vituo viwili vya afya, Kituo cha Mgeta na Kituo cha Unyali, vyote vina shilingi bilioni moja na milioni mia mbili na kitu, lakini Kituo cha Afya cha Unyali hakijakamilika na kitaendelea kukamilika, tumeomba Serikali itakimalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, hizi shilingi milioni 250 zilizotoka sasa hivi nimepata Kituo kipya cha Afya cha Mihingo, kiukweli watu wale walikuwa na tatizo kubwa. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kupata hizi fedha ili ziweze kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mollel, wewe ulikuja juzi, ulikuja Mara, wakati Katibu Mkuu wa CCM, wa chama chetu na Mgombea Mwenza wa Chama Cha Mapinduzi, Dkt. Nchimbi alipokuja kukagua utekelezaji wa Ilani kwenye Hospitali ya Rufaa Kwangwa, Mheshimiwa Dkt. Mollel ulipata maelekezo kwamba ile hospitali, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia ameipeleka mpaka imebaki ni kama 35%, tunaomba hayo maeneo yaliyobaki ya ujenzi na vifaatiba vilivyopo pale mmalizie. Maagizo yote ulipewa na unayajua. Tunataka tupate hospitali ile, ikamilike ili watu wetu wa Mkoa wa Mara watibiwe palepale katika Hospitali ya Kanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza mambo mengi sana kuhusu vifurushi vya bima ya afya. Nilikuwa napitia kifurushi kimoja kimoja, nikapitia kifurushi cha Tarangire, yaani watu umri wa miaka 18 hadi 35 wanasema ni shilingi 160,000; miaka 36 hadi 59 shilingi 192,000; miaka 60 na kuendelea mpaka miaka 115 maana sijasikia mtu amefika miaka 120 ni 115 nimewahi kusikia ni shilingi 240,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi vifurushi vya Tarangire vitatusaidia sisi kutibiwa ndani ya nchi yetu. Sasa kuna watu

wanazungumza ukubwa wa fedha kwa vifurushi, lakini nataka niwaambie sijui kama mnaenda hospitali. Juzi nimeenda matibabu ya mtu wa kawaida tu ana *pressure* kidogo tu dawa zake nimekuja *private* kununua wameniambia shilingi 240,000; ukienda pale Hospitali ya Benjamin Mkapa dawa hizo hizo ni shilingi 130,000. Ukiwa na bima ya afya, ukienda hospitali matibabu yako yanakurahisishia kuishi. Kwa hiyo, tusiangalie ukubwa wa hivi vifurushi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kifurushi kingine kinaitwa Mikumi, hiki kina shilingi 240,000 kutoka miaka 0 hadi 17, miaka 18 hadi 35 shilingi 432,000, miaka 36 hadi 59 shilingi 540,000, miaka 60 na kuendelea ni shilingi 708,000. Hivi vya Tarangire havina magonjwa yenye utata, hivi vya Mikumi vina magonjwa yenye utata, una tatizo la figo, una tatizo la moyo, una tatizo la magonjwa sugu inakusaidia. Sasa mimi sioni ukubwa wa fedha hiyo, watu waelimishwe, kwa sababu kuna jamaa mmoja aliniambia anataka kwenda India na kwenda India *private* lazima uwe na shilingi milioni 30 au shilingi milioni 20. Hivi kweli shilingi milioni 20 kwa hizi hela ambazo zimetajwa hapa ni kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kifurushi ambacho amekitaja hapa ambacho ni *Tanzanite* kinakuruhusu kwenda kutibiwa nje, miaka 0 hadi 17 shilingi 1,500,000, miaka 18 hadi 35 shilingi 2,700,000, miaka 36 hadi 59 shilingi 2,800,000, umri wa miaka 60 hadi 115 shilingi 6,700,000. Hivi kweli kwenda India kama watakupeleka kwa shilingi 6,700,000 si ni bure? Bure kabisa! Mimi nimetoka India juzi, wakikuacha tu bima ya afya, wakikutoa nje, kile chakula cha nje tu, unakula pale wiki mbili unakula karibu shilingi milioni 20, milioni ngapi.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa wapi?

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Noah.

## TAARIFA

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Getere kwa mchango wake mzuri, lakini afahamu kwamba kuna maskini wa maskini katika vijiji vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa asilinganishe na matajiri wenye uwezo wa kulipa vifurushi vikubwa na ndiyo maana michango ya Wabunge inaelekea kwamba kazi nzuri inayofanywa na Wizara iendelee kufanya kazi nzuri ya kuangalia na watu maskini wa maskini, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere, unapokea mchango wa Mheshimiwa Noah?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aah, sasa unajua hapa duniani tumeumbwa watu tofauti tofauti, na ninaipokea taarifa yake, siwezi kusema ninamkatili, lakini na yeye aelewe hapa duniani tumeumbwa watu tofauti, ukisema kwenda India tutumie shilingi 500,000, tukisema kwenda India tutumie shilingi 100,000 tutafia hapa wote. Ni lazima, kwa mfano kwa hivyo vifurushi vilivyowekwa ninaamini kwamba shilingi 6,700,000 Serikali imeweka wakikupeleka India kwa shilingi milioni labda 25 au 30, hiki ni kifurushi wamekuwekea tu, sicho kinachokutunza wewe.

Kwa hiyo, mimi naomba watu waelewe kwamba lazima tujikite kwenye bima ya afya ili tuendelee kuishi, vinginevyo tutafia hapa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nijue kifurushi cha bima ya afya kwa Wabunge, bima ya afya kwa Bunge ina upendeleo fulani. Serikali inaisha mwezi wa kumi na moja, bima ya afya ya hapa inaisha mwezi wa saba, yaani wewe Mbunge uko kwenye harakati za kugombea bima ya afya imeisha, ukiugua unafia hapo, hapana. Bima ya afya ya Wabunge na yenyewe iende kwenye mwezi wa kumi na moja ifike kama Serikali ilivyo. Haiwezekani mimi niko

kwenye kampeni, ninapambana, nimepata matatizo ya afya ninafia hapa, hakuna bima ya afya inaisha mwezi wa saba, haiwezekani jamani.

Kwa hiyo, lazima tuipeleke huko mbele ili na sisi tuweze kupata bima ya afya, tuendelee kuishi, lakini vinginevyo Serikali iendelee kufanya marekebisho, iendelee kuboresha bima ya afya, ikae vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Getere. Nilimuita Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane atafuata na baada ya hapo Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Afya. Kwanza kabisa niunge bajeti mkono kwa sababu ni bajeti nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo amewekeza kwa kiwango kikubwa sana kwenye Wizara hii ya Afya, amewekeza kwa sababu kwa kiwango kikubwa ameweza kuweka vifaatiba katika kila hospitali, vituo vya afya mpaka zahanati. Leo hii katika zahanati zetu kuna vifaatiba, kwenye vituo vya afya kuna vifaatiba, lakini ukija kwenye hospitali zetu za Wilaya na Mikoa tumepata vifaatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watumishi wote wa Wizara hii kwa sababu wanaitendea haki Wizara ya Afya, hongereni sana na tunawatakia kila la kheri muendelee kuchapa kazi bila kuchoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mheshimiwa Rais. Kwa mara ya kwanza

leo katika Hospitali yetu ya Mkoa wa Manyara tumepata mashine kwa ajili ya kusafisha damu kwa wagonjwa wa figo. Hii ni hatua ya pekee kwa sababu wagonjwa wetu wengi. Wananchi wa Mkoa wa Manyara wamekuwa wakisafiri umbali mrefu kuja hospitali ya Benjamini Mkapa na wengine imewalazimu kuhama makazi kwa sababu ya kufanya *dialysis* katika hospitali ya Benjamin Mkapa. Kwa hiyo, kuletwa kwa huduma hii katika mkoa wetu imekwenda kuwapunguzia gharama wananchi wa Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, gharama ya nauli kuja Benjamin Mkapa, lakini wengine walikuwa wanaenda kupangisha nyumba, hivyo gharama hizo zinakwenda kuondoka na wananchi wanakwenda kupata huduma ya *dialysis* katika Hospitali ya Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kwa sasa hivi kumekuwa na mlipuko au kumekuwa na ongezeko kubwa la magonjwa ya figo, magonjwa ya kansa kwa wananchi walio wengi. Mimi ninaiomba sasa Wizara, kwa kuwa tumefanya uwekezaji mkubwa sana kwenye vifaatiba na kujenga hospitali za kutosha, vituo vya afya vya kutosha sasa ione namna gani inakwenda kuweka mkakati. Kwanza, kujua kwa nini kumetokea ongezeko kubwa la magonjwa ya figo pamoja na kansa ili wananchi waweze kupewa elimu ya kutosha kuepukana na ugonjwa huu wa kansa na figo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani tulijua kwamba ugonjwa wa figo ni kwa ajili ya wazee, lakini sasa hivi watoto wadogo waliozaliwa wanapata pia tatizo la figo. Kwa hiyo, hili lazima kama Serikali iweke mkakati wa pekee na kuweka uwekezaji mkubwa kugundua chanzo ni nini na namna ya kuondokana na huu ugonjwa kwa sababu umeendelea kuongezeka kwa kasi kubwa kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ningependa kabisa Serikali ione namna gani pamoja na kwamba kuna ongezeko

kubwa la haya magonjwa, lakini ione kwamba kuna uwezekano mkubwa wa *lifestyle* ya kwetu sasa tunavyoishi nayo, yawezekana vyakula tunavyovitumia na matumizi mengi ya dawa ndiyo maana sasa ugonjwa huu umeendelea kuongezeka siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sasa Serikali ifanye uchunguzi hasa kwenye vyakula. Mfano tunatumia dawa kwenye mboga mboga, mazao na matunda, hebu Serikali iweke utafiti pale tuone kwamba zile dawa zinazotumika kwenye mboga mboga huenda ndiyo tatizo kubwa. Pia dawa zinazotumika yawezekana wafanyabiashara walio wengi kwa sababu ya tamaa na kukosa uaminifu, dawa inapigwa ndani ya wiki moja mtu anaenda kuchuma mboga anapeleka sokoni, anauza, halafu mboga unaenda kupika ina harufu ya dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili liangaliwe na hili linawezekana pale ambapo Serikali ione namna ya kuweka vifaa vya kupima pale sokoni ili kuona kama kuna ubora wa vyakula tunavyokwenda kuvitumia na kama chakula kina sumu basi kisitumike. Hili linawezekana kwa sababu Serikali imewekeza sana kwenye vifaatiba. Badala ya kuendelea kutibu basi tuanze kwenye kuzuia kwanza, kuanzia kwenye vyakula tunavyotumia maeneo ya sokoni kama mboga mboga pamoja na matunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielekee sasa kwenye hospitali yetu ya mkoa; Hospitali ya Mkoa wa Manyara tumepata *CT-Scan* lakini *CT-Scan* tuliyonayo haina mtu wa *radiology* hivyo inasababisha kwamba watu wengi wanafanya vipimo, lakini hawapati majibu kwa muda kwa sababu mpaka watafute mtaalam wa kusoma yale majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni uwekezaji mkubwa umefanyika, tuna *CT-Scan* lakini haifanyi kazi kama inavyotakiwa. Kwa hiyo, niombe Serikali ituletee mtaalam wa *radiology* pale mkoani ili wananchi waendelee kupata huduma ya *radiology*

badala ya kuendelea kuhangaika kwenda *Mount Meru* na Benjamin Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru Serikali kwa uwekezaji mkubwa wa kujenga hospitali ya mkoa. Niombe sasa Hospitali yetu ya Mkoa wa Manyara ikamilike kwa sababu bado haijafika kuitwa hadhi ya Hospitali ya Mkoa kwa sababu tuna upungufu mkubwa wa majengo. Hili nimeshalisemea mara nyingi hapa ndani, ninaomba tena niliseme kwa mara nyingine tena. Tuna upungufu wa majengo, sasa hivi tuna jengo la *maternity ward* na jengo la utawala tu hivyo imewalazimu hata jengo la utawala kutumika kama *ward. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sasa fedha zipelekwe ili majengo yakamilike. Jengo la *ICU* likamilike kwa sababu ina umuhimu mkubwa hasa kwa wagonjwa wanaofika hatua ya kwenda *ICU*. Jengo hili la *ICU* limesimama kwa muda mrefu na hakuna mfumo wa gesi. Kwa hiyo, niombe fedha zipelekwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia jengo la damu salama na jengo la *emergency* bado kuweka mfumo wa maji na mfumo wa *floor* pamoja na jengo la idara ya watoto, jengo la upasuaji na wodi ya wanaume na wanawake. Kwa hiyo, niombe sana majengo haya yakamilishwe. Fedha zipelekwe kwa wakati ili basi hospitali yetu ya mkoa ifanye kazi kama Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara badala ya kuendelea kuwasumbua wagonjwa kwenda kutafuata huduma kubwa kubwa katika hospitali kubwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna upungufu mkubwa sana wa madaktari. Kama nilivyokwisha kusema kwamba tuna upungufu wa watumishi kuanzia mtaalam wa *radiology,* lakini pia manesi hatuna wa kutosha pale kwenye hospitali yetu ya mkoa ukilinganisha na *population* iliyopo katika hospitali yetu ya mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hatuna madaktari bingwa wa mifupa na madaktari wa magonjwa ya ndani kwani mpaka sasa tuna daktari mmoja tu. Kwa hiyo, Serikali ione namna ya kutuongezea daktari. Pia madaktari wa watoto nao waongezeke ili huduma ziweze kutolewa kwa wagonjwa bila kuwasumbua wagonjwa kwenda kutafuta matibabu katika hospitali nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Hospitali yetu ya Mirembe. Ninaomba nikumbushie hapa Hospitali yetu ya Mirembe iongezewe watumishi. Kulingana na uhitaji uliopo kwa sasa watumishi ni wachache na hawatoshelezi. Pia hata majengo yaliyopo ni chakavu. Kwa hiyo, Serikali ijielekeze kuangalia namna ya kuboresha yale majengo ili huduma itolewe vizuri katika hospitali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona taa imewaka basi niunge mkono hoja kwa mara nyingine na pia nishukuru sana. Niwatakie kila la kheri Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwenye uchaguzi mkashinde na mrudi hapa mkiendelea kuwatumikia wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndege. Nilimwita Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mheshimiwa Selemani Kakoso ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya kwa Wizara yetu ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kuwekeza kwa kiasi kikubwa fedha nyingi kwenye sekta hii ya afya ambayo imeleta tija kubwa sana kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimpongeze mtani wangu, dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa kweli yeye ni mchapakazi. Ninakumbuka tangu akiwa Ofisi ya Waziri Mkuu alifanya kazi kubwa sana na hasa wakati ule tukiwa na kadhia kubwa ya mafuriko na mvua za *El-Nino* kule Kilwa alitusaidia sana kuweza kutatua changamoto mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amefika huku vilevile amefanya kazi kubwa sana. Ninakumbuka kama zaidi ya mara mbili wananchi wangu walikwama kutoa maiti zao pale Muhimbili, aliweza kutoa ushirikiano mkubwa na tatizo lile lilitatuliwa. Tuliweza kuchukua miili ya ndugu zetu tukaweza kwenda kuzika kwa wakati. Ninampongeza sana na ninamshukuru sana, aendelee na moyo huo huo. Ni imani yangu wananchi wa Peramiho wanaliona hilo, watampa kura zote za ndiyo ili apate miaka mingine mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Mollel, tulishirikiana vizuri kuwaleta madaktari bingwa wa lile kundi la Madaktari wa Mama Samia na kwa kweli kwa mara ya kwanza baada ya miaka mingi katika Hospitali ya Kipatimu iliyoko jimboni kwangu walifanya kazi kubwa sana ya kuwasaidia wananchi wetu. Huduma zilizotolewa zilikuwa hazipatikani pale, lakini kwa kushirikiana na madaktari wa pale na wa Wilaya yetu ya Kilwa na Mkoa wa Lindi, kazi ilifanyika nzuri na watu walifurahi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi kubwa zilizofanywa katika kutatua changamoto mbalimbali za sekta hii na kufanya ufanisi uongezeke na tija kubwa ipatikane katika sekta ya afya, nilikuwa ninaomba nishauri mambo yafuatayo; kwanza kumekuwa na shida kidogo kwenye vifaa vile vikubwa vikubwa vya kitaalam kama *MRI* na *CT-Scan*. Bado kuna changamoto; kwa mfano hizi *MRI* zimekuwa zikitolewa mpaka katika *level* ya kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninafikiri kuna umuhimu mkubwa wa hivi vifaa vya *MRI* kuweza kupelekwa katika hospitali za mikoa. Hii ni kwa sababu leo wananchi wengi wa vijijini kwetu wanasumbuka sana kuweza kufuata huduma hizi katika hospitali kubwa zilizopo Jijini Dar es Salaam, Benjamin Mkapa hapa na hospitali nyingine kubwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hospitali nyingi kwa mfano za mikoa hizo hakuna hivyo vifaa. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba Serikali iangalie hilo jambo ikiwezekana hospitali za mikoa watu wapate nafuu ya kufika kule kupata huduma kubwa kubwa kama hizo ili hatimaye waweze kutatuliwa changamoto zao za maradhi. *CT-Scan* pia nilikuwa ninaomba zipelekwe mpaka wilayani ili tuwe na uhakika wa kuwatibu wananchi wetu kwa kutumia hii mitambo ya *CT-Scan*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwa na changamoto kubwa ya ugonjwa wa figo na wagonjwa wengi wamelazimika kufuata mashine za *dialysis* katika hospitali kubwa. Matokeo yake wengi wamekuwa aidha wanashindwa au wanazifikia kwa kuchelewa sana au katika mazingira magumu sana kwa sababu zipo katika hospitali kubwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba ugonjwa wa figo sasa hivi umekuwa ni ugonjwa mkubwa mno kuliko ilivyowahi kutokea huko siku za nyuma. Kwa maana hiyo nilikuwa ninashauri Serikali ipeleke mashine za kupima *dialysis* mpaka katika hospitali za mikoa na wilaya ili wananchi wetu wasisumbuke kwenda mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mtu anatoka Nandete huko Kilwa anakwenda mpaka Dar es Salaam - Muhimbili au Mloganzila kufuata huduma hii, kwa kweli inakuwa ni shida. Pia kumekuwa na gharama kubwa sana ya kutibu huu ugonjwa. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba Serikali itengeneze programu kama ilivyokuwa kwa wagonjwa wa kifua kikuu au kama ilivyokuwa kwa wagonjwa wa saratani ambao wanapata huduma hii bure na huduma hii ya

kutibu ugonjwa wa figo pia itolewe bure. Katika eneo hili nilikuwa ninaishauri Serikali itafute chanzo cha mapato kwa ajili ya ku-*subsidize* hii huduma ya tiba ya figo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nikiendelea kuchangia niende kwenye *NHIF* na vifurushi vyake. Ninafahamu kwamba kuna vifurushi takribani vitano; kuna kifurushi cha Tarangire ambacho kinaanzia shilingi 168,000; Ngorongoro shilingi 240,000; kuna cha Mikumi kinaanzia shilingi 432,000; kuna cha Serengeti kinaanzia shilingi 660,000 lakini kipo cha *Tanzanite* ambacho hiki kinapeleka hadi wagonjwa nje ya nchi ambacho kinaanzia shilingi 1,500,000 mpaka 11,493,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi kwanza nishukuru na kuipongeza Serikali wameweza kupunguza viwango vya kuanzia vya chini kabisa vya hivi vifurushi vya bima ya afya. Ninakumbuka kabla ya mwezi Mei mwaka huu, hiki kifurushi ambacho tunalipia shilingi 168,000 kilikuwa kinatolewa kwa shilingi 192,000 (hiki cha Tarangire). Pia kile cha chini kabisa cha Ngorongoro kilikuwa kinatolewa kwa shilingi 360,000 lakini leo kinatolewa kwa shilingi 240,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru Serikali imepunguza, lakini ninafikiri bado tunao wananchi ambao hawawezi kumudu hizi gharama. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba tuangalie uwezo wa watu pia ikiwezekana tupunguze hadi kiwango cha chini kabisa chini ya hapo ili wananchi wetu waweze kunufaika na hizi huduma ambazo zinatolewa kwenye hivi vifurushi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nilikuwa ninaomba kwamba kwa wazee tusifike mahali wazee wakatuona kama vile wao kundi lao ni kama kundi ambalo limepata laana au kama kundi ambalo limepata balaa au kama vile hatuwataki kwa sababu viwango vinakwenda kwa mujibu wa umri. Kadri umri unavyopanda na viwango vinapanda. Kwa hiyo, wazee wanatibiwa kwa gharama kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilifikiri katika eneo hili Serikali pia iangalie ile programu ambayo inakwenda kwenye *dialysis* pia waiangalie kwenye bima ya afya. Ikiwezekana huu mfuko uwe unapewa *subsidies* kutokana na chanzo fulani ambacho tutakibuni ili kuweza kuwasaidia wazee, ili hawa wazee ambao wamelitumikia Taifa hili kwa miaka mingi na wamezalisha sana tu wakulima, wafanyakazi na wengine nao waweze kunufaika au kuishi vizuri katika uzee wao. Tutakuwa tumewasaidia sana wazee wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa ninaomba hii taasisi yetu ya *NHIF* imekopesha maeneo mengi sana kwa ajili ya kuimarisha miundombinu. Ninakumbuka kule *MOI* waliwahi kukopeshwa, hapa Benjamin Mkapa waliwahi kukopeshwa na taasisi ya *NHIF* zaidi ya shilingi bilioni 200. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali ihimize taasisi ambazo zimekopa hizo zaidi ya shilingi bilioni 200 waweze kurejesha hiyo mikopo ili taasisi yetu iweze kuwa himilivu, iweze kuwa endelevu, isifilisike na iweze kutoa huduma bora kwa wananchi wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa ni suala la matumizi ya TEHAMA. Serikali imefanya kazi kubwa ya kuboresha huduma ya TEHAMA kwa kushirikiana na wadau wetu. Hii huduma ni nzuri sana kwani imeboresha kwanza kazi za madaktari wetu, manesi wetu na watumishi wengine katika kada hii ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninafikiri uimarishaji wa huduma hii ya TEHAMA uendelee ili kuhakikisha kwamba huduma hii ya afya inaendelea kuboreshwa, lakini pia tutadhibiti wizi na ubadhirifu wa fedha kwenye mapato. Kwa hiyo, ninaomba sana Wizara yetu na Serikali yetu itilie mkazo kwenye matumizi ya TEHAMA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye *NHIF* ningeomba tuendelee kuboresha huduma ya upatikanaji wa dawa na vifaatiba kwenye hospitali zetu. Hii ni kwa sababu kama alivyozungumza

Mheshimiwa Asenga, kuna maeneo unakwenda unaambiwa dawa ukachukue eneo lingine. Ukienda kule unaambiwa dawa hazijafika au kuna upungufu hazipo hivyo dawa nyingine unapata na nyingine unalazimika kwenda kununua kwa sababu ya hali ambayo unayo ya maradhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba yote haya yaimarishwe ili kuhakikisha kwamba huduma ya afya inasonga mbele na inaendelea kuboreshwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninasema ninaishukuru na kuipongeza Serikali kwa huduma bora ya afya inayoendelea kuimarishwa na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tuna wageni ndani ya Ukumbi wetu wa Bunge ambao inabidi tuwatambulishe.

Tuna wageni wa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel ambao ni Dkt. Alex Msoka, Rais wa Chama cha Madaktari Tanzania *(MAT)*, tumuone yuko pale; na Dkt. Mwanaada Kilima, Mwenyekiti wa Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani, yuko pale. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 83 wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga ambao ni wanafunzi 73 na walimu 10 wa Shule ya Sekondari *St. Glory* kutoka Wilaya ya Mafinga, Mkoa wa Iringa, karibuni sana kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Tuna wageni 64 wa Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, hawa ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Sekondari Nakwa kutoka Babati, Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni ambao wamekuja kwa ajili ya mafunzo; wapo wageni wanne na walimu watano wa Shule ya Msingi Lukobe kutoka Kata ya Lukobe, Mkoani Morogoro, karibuni sana.

Pia tunao wanafunzi 55 na walimu watano wa Shule ya Msingi Madizini kutoka Mkoa wa Morogoro, karibuni sana watoto wetu. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 100 na walimu 13 wa Shule ya Msingi na Awali Canossa kutoka Dar es Salaam, karibuni sana sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Nimwite sasa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Kakoso, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay ajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninakushukuru kwa kuweza kunipatia fursa ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Afya, Wizara ambayo ni muhimu sana kwa uhai wa Tanzania na zaidi kwa uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwa kweli na mimi niwapongeze Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kazi ambazo wamezifanya. Nimepitia pia hotuba hii inatia matumaini kuendelea kuboresha miundombinu ya afya. Zaidi nimpongeze pia Ndugu yetu Dkt. Janabi kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi wa *WHO* kwa Kanda ya Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee kabisa nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwani ameonesha dhahiri kabisa amekuwa na *political will* ya kuweza kuboresha miundombinu ya sekta hii ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona na kweli tunatambua kwamba kipindi chake takribani hospitali tisa za kanda zimejengwa, hospitali za rufaa za mikoa takribani 28 ikiwemo Hospitali yetu ya

*Mwalimu Nyerere Memorial* kule Musoma, Mara ambayo kwa kweli tangu tukiwa Bunge la 10 Mwenyekiti wetu akiwa Mheshimiwa Wasira hapa tumekuwa tukiiomba hiyo hospitali iweze kujengwa kipindi hicho ikiitwa Kwangwa. Sasa kwa kipindi hiki imeweza kujengwa na inaenda kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni pongezi kubwa sana tunatoa na zaidi kwa kuboresha hiyo miundombinu ambayo imepelekea hata kuweza kuboresha zaidi huduma ya afya ya uzazi na kupunguza vifo vya akina mama wajawazito kutoka 556 mpaka leo tunaongea ni 104 kwa vizazi hai 100,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo kubwa na ni *step* kubwa ambayo imepigwa na tunatamani sana huko mbeleni tuwe na *zero cases* za mama wajawazito ambao wakati wakijifungua wanafariki. Kwa kupitia hii tumeona mpaka taasisi za kimataifa, kwa mfano Taasisi ya *Gates Foundation* iliweza kumpa hiyo *The Global Goalkeeper's Award.* Kwa hiyo ninampongeza sana kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali yetu ya Rufaa ya *Mwalimu Nyerere Memorial* ya Mkoa wa Mara tunashukuru, lakini bado haijakamilika kwa 100%. Inahitaji takribani shilingi bilioni 18, sasa hivi tumepata shilingi bilioni nne tu kuweza kukamilika, lakini kuna wakandarasi ambao wame-*stop.* Kuna mkandarasi wa umeme wa *TEMESA*, mkandarasi wa *lift* na mkandarasi wa kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi wamesimama kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji fedha ziende ili hospitali iweze kuwekewa vifaa kwa ukamilifu. Mmetuletea vifaa ambavyo vinahitaji umeme, lakini havitumiki. Kwa mfano *mortuary* hai-*operate*, *x-ray* na mashine nyingine za kisasa hazi-*operate* kwa sababu umeme haujawekwa kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba sana fedha ziende kwa sababu hii hospitali imeshaanza kufanya kazi iweze

kusaidia wananchi wa Mkoa wa Mara. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri hilo muweze kulizingatia, fedha ziende kwa wakati ili hawa wakandarasi waweze kumalizia kazi zao ambazo wanaendelea kuzifanya pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika hospitali ile barabra ya kufika hospitali hii ni mbaya sana. *TARURA* walisema wangeweza kuitengeneza mwaka huu wa fedha, lakini hawajafanya, wameweka kwenye *phase two*. Tunaomba kama inawezekana mtutengenezee barabara ambayo inapitika kwa uhalisia kwa sababu ile ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ili waweze kutoa huduma ambayo ni bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *campus;* jana aliongea Profesa Muhongo hapa, tulitaka *campus* ijengwe pale ya chuo kikuu. Ardhi imepatikana na kabla hatujatoa hiyo ardhi ekari 20, walikuwa wanasema fedha zipo zinahitaji ardhi. Tunaomba muweze kuongea na Wizara ya Elimu, kama fedha zilikuwepo za mradi, watujengee ile *campus* ya Chuo Kikuu cha Afya pale ndani ya Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea kuna kijana anaitwa Edward Chimoi, huyu kijana amevumbua *robot medical beds* ambayo ina uwezo wa kumchukua mgonjwa akiwa katika *level* yoyote ile, anaweza kutembea, hawezi kutembea, ikambeba kutoka pale ikampeleka sehemu mbalimbali kwenye *emergency, ICU,* wodini na kwenye *radiology* na pia inapima kilo za mgonjwa. Ikikubeba inapima kilo za mgonjwa. Pia ametengeneza kifaa kingine cha *gauze* ambacho kina *bend gauze,* kama mtu amepata *accident* ina mawasiliano, ina-*communicate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huyu kijana amewatafuteni, hebu muwezesheni, kitanda kimoja kina-*cost almost sixteen million.* Ametafutwa na watu wa nje ili aweze kuwapa *code,* nao wamefika bei mpaka ya shilingi milioni 200 aweze kuwapa huo ujuzi wamchukue, wampeleke nje, wakae naye miaka mitatu.

Tusipomchukua tukamtumia sisi kama Watanzania, kama Wizara, akienda nje tutaishia ku-*import* hivyo vitanda kwa bei ghali zaidi, mtafuteni ameshawafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niliona *presentation* yake akifanya kule Iringa kwenye kongamano la kisayansi kwa wauguzi, anasema kufanya hivyo atasaidia wauguzi wengi. Amesema amefanya tafiti wauguzi wengi wanalalamika migongo kwa sababu ya wanavyofanya ile *pushing*. Sasa hili *robot* litasaidia na lita-*save time* ya wauguzi ambayo wana-*spend* pale na mbaya zaidi au nzuri zaidi ni lile *robot,* anasema lina-*memorize,* linaweza hata likamkumbusha muuguzi kwamba ni muda gani mgonjwa anatakiwa kupewa dawa, linampunguzia muuguzi majukumu mengi, anabaki tu na ile *patient operation care* ya kawaida, anajua nitafanya hivi, lakini mengine mengi hiki kitanda cha *robot* kimeyachukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaenzi hawa watoto wa Kitanzania ambao wamekuja na huu uvumbuzi tuweze kuwaendeleza na Serikali mnaichukua hiyo sasa inakuwa ni ninyi. Mnaweza mkawa mnauza hata nchi nyingine za nje vitanda hivi. Ninaomba sana mlizingatie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Sera ya Afya ya Taifa ya mwaka 2007 ambayo inasema inatoa huduma bure kwa mama wajawazito na watoto, ni muhimu sana. Nimetoka kusema hapa, dhamira ya Mama Samia na Serikali yake kuhakikisha tunakuwa labda na *zero rate* ya vifo vya mama na mtoto, nina imani kwanza Serikali mnatakiwa mfanye tafiti ya kina. Tunatambua kwamba kuna Watanzania wana uwezo wa kulipia hizi *delivery kits,* lakini kuna wengine hawawezi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fanyeni utafiti wa kina muweze kugundua na mtambue kwamba hata maandiko matakatifu yanasema, nikirejea kwenye Mwanzo 1:28; "Mungu akawabariki na kuwaambia, zaeni muongezeke mkaijaze nchi na kuimiliki..." Sasa

Tanzania tusigeuze wamama wajawazito kama vile ni adhabu, yaani leo nikipata ujauzito kama sina uwezo, sitaenda hospitali. Sina *delivery kits that mean* nitakaa nyumbani. Nitajifungua isivyo salama na ninaweza nikapoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana, fanyeni utafiti wa kina muweze kugundua na kupitia hata sensa, ile inachukua *data* za Watanzania. Wale ambao hawajiwezi kabisa wapeni nafuu, wawe wanakuja kujifungua *for free. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vile kwenye umeme walivyofanya, wa mjini wanaunganishiwa kwa shilingi 320,000 wa vijijini kwa shilingi 27,000. Fanyeni utafiti wa kina, wale ambao wanajiweza waje na *delivery kits,* wale ambao hawajiwezi Serikali iweze ku-*take care,* tuweze kutafuta hela sehemu nyingine zozote zile ambako kuna imani ya ubadhirifu wa fedha, ikaja kujazia Watanzania waweze kuokoka na kuijaza dunia na kuijaza Tanzania. Anaweza akawa mama amefariki na mtoto, labda anakuja kuwa Rais wa Tanzania. Tuokoe maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ninashukuru sana, nilitembelea mabanda, Wizara ya Afya mmeleta mabanda mbalimbali pale. Sasa katika kupita nikapata hiki kitabu, "Mtindo wa Maisha na Magonjwa Yasiyoambukiza." Nimekisoma kwa muda mfupi tu jana usiku, baadhi ya maneno, ni kitabu kizuri sana. Pamoja na kwamba mnasema mnatoa elimu, mkitoa elimu siyo wote kwanza wenye *TV!* Pili, siyo wote wapo kwenye *social media!* Tatu, siyo wote wanasoma magezeti na nne, siyo wote wanasikiliza redio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *printing* ya hiki kitabu tuhakikishe kila kaya inapata. Kama kweli tunataka tu-*save* nchi yetu iwe na watu wenye afya, namba moja ni kila kaya iweze kupata hiki kitabu, lakini haya magonjwa myaoneshe mengi na mseme; "tafiti ya mwaka 1986/1987 ilionesha katika watu hai 100, mtu mmoja alikuwa na kisukari na watu watano walikuwa na shinikizo la damu." Tafiti ikaja mwaka 2012 ikasema, "katika watu 100 watu tisa kisukari, 26 shinikizo

la damu." Kuanzia mwaka 2012 nina imani hamjafanya mpaka sasa hivi. Mkifanya, *it is worse,* yaani ni mbaya zaidi na mmeonesha hapa mambo mbalimbali, vyakula, kutokufanya mazoezi na sijui pombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ninaenda kwenye mawili tu kwa sababu ya muda na nitaomba uniongezee muda kidogo. Kwenye mazoezi tumekuwa tukiongea na nina imani wale wa vijijini wengi wako *active naturally,* lakini mjini. Mmeeleza hapa, kukaa sana, kutokufanya mazoezi na kufanya nini, hatuna miundombinu. Serikali muongee, Wizara ya Afya muongee na Wizara ya Michezo muweze kuweka viwanja, katika kila mtaa hakikisheni kuna sehemu za kukimbia. Watu wakitoka kazini waende wakimbie, kusema eti wanafanya mazoezi asubuhi, mimi ninaamka nikimbizane kwenda, kuna foleni, nitafanya mazoezi saa ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi baada ya kazi nitajua kuna sehemu kwenye mtaa wangu. Nitaenda nitakimbia, nitafanya mazoezi, watu wajengewe hii *culture*. Wekeni miundombinu wezeshi kuweza kuwa-*save* Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye nyingine, wamezungumzia pombe. Tena hapa mmeweka pombe za kawaida kabisa, ila mkasema *excessive* pombe ina madhara mengi. Mmeainisha hapa, moyo, kongosho, sijui figo, kisukari, ini, ubongo, sijui nini, mengi. Utapiamlo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu linateketea na uzazi na vingine. Taifa letu linateketea kwa pombe, achilia hizi ambazo mmeziandika hapa nzuri. Tumeshaongea mpaka huku Bungeni hadi Mheshimiwa Spika akaelekeza mkafanye uchunguzi, mlete tafiti za kina, vijana wanateketea kwa pombe ambazo nyingine ni *fake*, leo sitaji, siku ile nilitaja. Zinauzwa holela mpaka kwenye maduka ya chakula, mnasema sijui figo ni *expensive, if we don't prevent, definitely* itakuwa *expensive*.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatutazuia pombe ambazo zinaleta magonjwa mengi tutatumia fedha nyingi sana kuwatibu Watanzania.

**MWENYEKITI:** Taarifa. Mheshimiwa Festo Sanga.

**TAARIFA**

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mbunge hodari kweli kweli wa Tarime, Mheshimiwa Dada Esther kwa mchango wake mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi tumezungumza hapa kuhusu bima ya afya kuchangia, tutatafuta fedha nyingi sana kuweka kwenye Mfuko wa Bima ya Afya na bima ya afya itawezeshwa, lakini mzigo tunaoutengeneza utakaotumia hiyo hela kwenye bima ya afya unaotokana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ilani mpya inaelekezwa, ukurasa wa 62, itakuwa ni changamoto kubwa sana, kama Wizara haitakuwa na mkakati wa kudhibiti pombe zinazoleta magonjwa ya figo na magonjwa tofauti tofauti kwa sababu mzigo wote wa fedha tunaoupeleka kwenye bima ya afya utaenda kuishia kwenye magonjwa haya, kama hatutadhibiti mapema.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, umepokea Taarifa hiyo?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea *in a very positive aspect.* Ni kweli sasa hivi watu wanajituma ila tukija kuweka *universal health coverage* itakuwa ni *bombshell* kwa sababu tutakuwa tunatumia hela nyingi sana kutibu haya magonjwa. Kwa hiyo, tu-*prevent,* tuhakikishe tunadhibiti. Shirikianeni na Wizara ya Viwanda na Biashara, shirikianeni na mamlaka nyingine zozote, hizi pombe ziko mtaani, hata haziuzwi kwenye *store*

ambazo zinatakiwa kuuza pombe, zinauzwa kwenye maduka ya vyakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaua Watanzania, unakuta mtu anakunywa pombe, tunazika sana, labda ninyi hamziki. Mtu anakunywa pombe, tena siyo mpaka kwa figo, mwingine anakufa tu kwa sababu anakunywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu ameshikilia ki-*energy drink,* siyo *energy drink that one!* Bodaboda wengine, siyo *energy drink,* vijana wanakufa. Wengine wanakuwa hawali, wanakufa, Taifa linateketea. Tuwa-*save,* yaani kama nchi mnatumia mitutu ya bunduki kulinda mipaka ya nchi wakati ndani vijana wanateketea kwa vitu ambavyo Serikali mngeweza kuvifanya mkapunguza vifo vya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana, hii ni *crisis,* mui-*take as a priority* mhakikishe mnadhibiti pombe zote hizi na hata watu wanaouza rejareja. Wakikamatwa washtakiwe, watu wakinywa, wanywe kwa staha kwa mamlaka ambazo zimepewa leseni ambapo wanauza kwa mujibu wa taratibu na kanuni za nchi yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Matiko.

Nilimuita Mheshimiwa Selemani Kakoso, atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nawapongeza sana Wizara ya Afya kwa juhudi kubwa ambazo wamezifanya kwenye Taifa letu. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuleta fedha nyingi za maendeleo hasa kwenye maeneo ya jimbo langu. Wilaya ya

Tanganyika imepokea vifaatiba vingi na vya kisasa ambavyo kiukweli vinavutia sana na vinatoa huduma nzuri kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia kuipongeza Serikali, Serikali ya Awamu ya Sita imeleta fedha nyingi sana za maendeleo kwenye maeneo mbalimbali katika sekta ya afya. Kwenye eneo hili ni lazima tuipongeze Serikali kwa sababu vitu vilivyoletwa na Serikali vimeonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Katavi ulikuwa hauna Hospitali ya Mkoa, lakini leo hii tunayo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ambayo inafanya kazi na inawasaidia wananchi wote wa Mkoa wa Katavi. Wilaya ya Tanganyika tulikuwa hatuna Hospitali ya Wilaya, leo tunavyoongea huduma zinatolewa na tunapata huduma nzuri, tuna vifaa ambavyo hata maeneo mengine hawana, sisi tumepata. Bahati mbaya tu ambayo ningependa kuishauri Serikali, itusaidie wananchi wa Wilaya ya Tanganyika, ni uhaba wa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili tuna uhaba mkubwa sana. Mahitaji ya watumishi wa kada ya afya ni 776, waliopo mpaka sasa ni 276; kwa hiyo, tuna tofauti ya watumishi 500. Ukiangalia uhalisia wa kile ambacho kimepelekwa, bado huduma tunayoipata ni duni sana kutokana na uhaba wa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya kutolea huduma za afya ambavyo vipo kwa sasa ni 43. Kabla ya hapo tulikuwa na vituo 28, vituo vingi havina watumishi. Tulikuwa na vituo vitatu vya afya, lakini kwa sasa tunavyo vituo tisa, kati ya hivyo, vituo vingine vimeshindwa kufanya kazi kwa sababu ya kukosa watumishi. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri tuangalie kwa jicho la huruma, tunahitaji watumishi kwenye hospitali ya wilaya, kwenye vituo vya afya na kwenye zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Naibu Waziri alishafika kwenye maeneo hayo, anatambua amefika na anajua mazingira ya Wilaya ya Tanganyika jinsi yalivyo. Nawaomba sana mtuletee watumishi, kada ya manesi na madaktari. Tumepewa vifaa vya

kisasa vya *x-ray* karibu vituo vyote vya afya na hospitali ya wilaya; tuna mtaalam mmoja tu ambaye yupo anatumika maeneo yote hayo kiasi kwamba huduma nyingine zinashindwa kufanyika kwa sababu huyo ndiye anayetembea kwenye maeneo ya wilaya nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba sana Mheshimiwa Waziri watuletee watumishi wa kada ya afya ambao wanahitajika kwa wakati, kwa muda huu ili waweze kuja kutatua tatizo lililopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninazungumzia ni bima ya afya. Kwenye eneo hili bado hatujafanya vizuri. Halmashauri yangu ya Wilaya ya Tanganyika iliingia bima ya afya kupitia vijiji vile vinavyopata fedha za hewa ya ukaa, wamelipa; vijiji vyote nane ambavyo vinanufaika vilipata fedha na kulipia, lakini bahati mbaya sana huduma hii imekuwa haipatikani kwa sababu ya mfumo wa bima ya afya ulivyo na vikwazo. Naomba hili mlifanyie kazi na muangalie ni jitihada zipi ambazo zitafanyika ili tutatue tatizo la bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kulingana na Mwongozo wa Bima ya Afya kwa Wote uliopo kwa sasa, ninataka tupate ufafanuzi; je, wale waliolipia kwa mfumo huu mwingine mpya unaokuja kwa bima ya afya ya watu wote, Serikali itafanya vipi kuhakikisha wale waliolipia kipindi hiki cha nyuma wanaingia kwenye mfumo huu uliopo au wataenda kwenye mfumo mpya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tupate ufafanuzi wa Serikali, ili tupate mwongozo wa bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia sana juu ya kulinda matumizi ya vyakula na pombe kali. Hili ni jambo ambalo kila eneo linaathirika sana hasa kundi la vijana. Bodaboda wengi wameathirika sana na matumizi mabaya ya pombe ambayo yanatumika siku hadi siku. Naomba maeneo haya tuyafanyie kazi, bila hivyo Taifa litaingia kwenye

gharama kubwa sana ya kutibu Watanzania na fedha hizo hatutakuwa nazo, gharama ya kutibu wagonjwa karibu wote nchi nzima itakuwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee juu ya wataalam wa maabara kwenye Wilaya ya Tanganyika; pamoja na jitihada zilizofanywa za kuleta vifaatiba, kila kitu kimeletwa kwenye eneo hili, lakini hatuna wataalam wa maabara. Eneo hili tunaomba muweze kuliangalia vizuri ili kutatua kero ambayo inatokea pale wataalam wanapokosekana ambao ndiyo wanaobaini chanzo cha magonjwa ambayo yamekuja kuripotiwa kwenye vituo vya afya au hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliomba *ambulance;* Wilaya ya Tanganyika iko na mtawanyiko na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri mmefika huko. Tunaomba *ambulance* moja ili iweze kusaidia kwenye Ukanda wa Ziwa Tanganyika ambao hauna kabisa *ambulance*. Eneo hili ni muhimu sana tuweze kupata *ambulance* walau mbili, moja iende eneo la Mishamo na nyingine iwepo kwenye eneo lile la Ukanda wa Ziwa na ile iliopo iweze kusaidia kwenye eneo la hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Serikali na ninampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na watumishi wote wa Wizara ya Afya kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuleta fedha nyingi kwenye kada ya afya. Ninaomba kuishukuru sana Serikali kwa dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kakoso.

Nilimuita Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula. Baada ya hapo atafuata Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE: ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa rehema zake kwetu sote, lakini pia kwa Taifa letu kwa mambo mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa sana iliyofanyika. Kwanza, kwenye Jimbo la Mbulu Mjini na pia katika majimbo mbalimbali nchini kwa kazi kubwa katika Wizara hii ya Afya na sekta nyingine. Kwa kweli, kazi kubwa sana imefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naishukuru Serikali nzima ya Awamu ya Sita kwa nafasi mbalimbali. Pia nakushukuru wewe Mheshimiwa Waziri, kwa kazi kubwa unayofanya toka tulivyoanza hapa Bungeni hadi sasa ukiiongoza Wizara hii, hongera sana kwa utendaji wa kazi. Nakushukuru Naibu Waziri, tumeshirikiana mambo mengi sana kwa miaka mitano ya kwanza na mitano hii ya pili ukiwa kama Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa imefanyika, tunashukuru kwa ujumla na mimi ninakushukuru sana. Pia natoa shukrani nyingi kwa wateule mbalimbali wa Wizara kuanzia Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Serikali wa Wizara hii pamoja na Wizara nyingine kwa kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kueleza mafanikio na changamoto zilizoko. Kwanza, nizungumze suala la mafanikio; kazi kubwa ya ujenzi wa miundombinu mingi sana imefanyika katika Wizara hii kwa kipindi cha miaka minne ya Dkt. Mama Samia na pia kwa Serikali za awamu zilizopita, kwa kweli, hatujatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwa ujenzi wa majengo, lakini pia kwa miundombinu na vifaa vya matibabu katika sekta yetu ya afya na hasa Jimbo la Mbulu Mjini. Tumefanikiwa pia ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali ya mji, kwa kweli, majengo mengi sana yamefanyika. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nieleze kwamba fedha hizi nyingi zilizopatikana katika miundombinu imepunguza matatizo mengi kwa wananchi wa Jimbo langu la Mbulu Mjini. Kwa zahanati kama tisa zilizojengwa zinatoa huduma, vituo vya afya vinne, magari, vifaatiba na majengo katika hospitali ya mji; kuna majengo mengi yamejengwa kwa mabilioni ya fedha na huduma zimeboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto chache tu; kwanza nielezee kwamba Jimbo la Mbulu Mjini ni jimbo lenye kata nyingi kati ya majimbo ya miji kwa Taifa letu kwa sababu sisi tuna kata 17 tofauti na majimbo mengine ya miji yenye kata nane, kata 10, kata 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna jiografia ya aina mbili, tuna vijijini na mjini. Kule vijijini tuna kata 10 na mjini tuna kata saba. Maeneo haya ya vijijini kijiografia ni magumu kidogo kuyafikia, lakini Serikali tumejenga vituo vya afya, nishukuru kwa fedha zilizopelekwa. Hivi juzi, ndani ya mwezi huu wa tano tuna ujenzi wa Kituo cha Afya Murai na tunaendelea kuomba fedha hizi zingine zilizobaki kwa ajili ya kituo cha afya, kwanza kile cha Bunyoda na kile cha Gehandu. Kwa kuwa iliwekwa kwenye mipango yetu na nimeahidiwa na Mheshimiwa Waziri na watendaji wa Wizara ya TAMISEMI kwamba fedha hizi zitapatikana kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha, basi tunaishukuru Serikali walau hata zile za shilingi milioni 250 zikija zitaanza ujenzi kwa sababu bado ni mwendelezo na bajeti zetu ni hizo ambazo tunatarajia kupata na wakati huo kwenda kutekeleza miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie eneo hili la mafanikio. Hospitali ya Mji wa Mbulu tumejenga majengo makubwa, tumeletewa vifaa, kwa maana ya jengo la dharura pia na jengo la uangalizi wa wagonjwa. Majengo haya yamekuwa chachu kubwa pamoja na gari za *ambulance* zilizopelekwa mbili. Kule kwenye Kituo cha Afya Kainam tayari imeanza kutoa huduma. Katika mgao unaokuja kituo hiki cha afya kiko kijijini na kinahudumia kata karibu nne. Kwa hiyo, tukipata gari la *ambulance* itasaidia sana

Mheshimiwa Waziri kwa sababu tunaamini zile zilizoletwa zinahudumia katika vituo ambavyo tayari sasa hivi zinatoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika bima ya afya, niwapongeze sana watendaji wa hospitali hizi za Taifa kama Muhimbili, Hospitali za Kanda, Hospitali za Rufaa na hizi za mikoa kwa huduma za kadi ya bima ya afya. Anapokwenda muhitaji, mgonjwa wa bima ya afya, wamemwandalia utaratibu mzuri sana, kwa maana anapokelewa, anahudumiwa, anapelekwa katika *department* mbalimbali kwa maana ya vitengo na baadaye anapatiwa huduma zake mpaka dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hospitali za miji na wilaya bado bima hii, baadhi ya dawa na baadhi ya huduma zinalipiwa. Mimi nilikuwa naomba kama inawezekana kwa Hospitali ya Mji wa Mbulu bado tuna tatizo kubwa la upungufu wa dawa. Huwa ninatembea wodini na kwenda kwenye wodi mbalimbali, ninazungumza na wagonjwa ninakuta mambo mengi, wagonjwa wengi wananunua dawa hizi na hasa kundi lile la mama na mtoto pamoja na wazee ambao kwenye sera yetu tumesema walau wapewe huduma ya afya bila malipo. Tukisema bure tunakwenda kinyume zaidi, tuseme bila malipo, kwa maana ya msamaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika eneo hili mimi ushauri wangu ni kwamba kwanza tutazame takwimu za wapokea huduma. Hospitali ya Mji wa Mbulu inahudumia iliyokuwa Halmashauri ya Mbulu ambayo sasa ni Halmashauri ya Karatu, kwa kuwa iko katikati inahudumia Halmashauri ya Babati, eneo la Magara na Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu. Kwa kuwa ni hospitali yao kongwe ya zamani, basi watu wana imani kubwa kwenda hapo na mara nyingi wakienda wanategemea watapata huduma. Kwa hiyo, kuna mwingiliano wa takwimu ambazo haziko kwenye takwimu za Halmashauri ya Mji wa Mbulu kwa ajili ya wapokea huduma, akina mama wajawazito pia unakuta kuna wagonjwa kutoka hizo halmashauri zinazopakana kwa ajili ya ukaribu wanakwenda pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba walau niiombe Wizara ione namna, kwanza kuangalia zile takwimu halafu iongeze huduma ya dawa na vifaa tiba kwa ajili ya bajeti, kwa sababu inaonekana idadi ile ukiitazama ni takribani 30% kwa mwaka wanatoka katika halmashauri hizo zinazotuzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili litahitaji sana, sana, sana, kutazamwa kwa sababu eneo la afya ni eneo *sensitive* na inategemewa na watu wengi. Namna pekee ninayoona ni kwamba kama tunaweza kuongeza ruzuku basi tuongeze ruzuku kwenye upatikanaji wa dawa na vifaatiba ili walau wale wananchi ambao hawana uwezo wa kulipia hizo gharama waweze kuhudumiwa na hasa kundi hili la akina mama kwa sababu ukizungumza gharama ya upasuaji shilingi 150,000 ama shilingi 120,000 kwa mama mjamzito unaweza kukuta familia hiyo haina huo uwezo.

Kwa hiyo, tunatakiwa kupunguza baadhi ya huduma kuzilipia. Tunajua zingine lazima wananchi walipie, Serikali kwa uwezo wake haiwezi kulipia gharama ya matibabu kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hizi bima za afya tunazozungumza zile *package* za mwisho zile za chini tunajua inahudumia kwenye ngazi fulani fulani za matibabu. Mimi ninadhani bado kwa matatizo ya magonjwa kuna wananchi wengi sana kule chini wanahitaji wapate huduma hizi za ngazi ya wilaya, ngazi ya mkoa na ngazi ya hospitali za rufaa. Tuitazame upya namna ambavyo huduma hii itatengamaa na itatoa huduma nzuri kwa makundi haya ya wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye eneo hili la pombe sitazungumza sana, lakini tutazame. Ninadhani *alcohol* hizi za viroba Mheshimiwa Waziri na Serikali kuna haja ya kwenda kuandaa vipimo maalum ili kuona athari zikoje na kwa namna gani tunaweza tukakabiliana nayo. Kwa nini nazungumza hivi, mimi pia ni mshiriki au mfanyabiashara wa baadhi ya pombe, lakini ninachojifunza ni

kwamba pengine mwananchi anatumia chupa za *mills* 250 kama mbili au za *mills* 200 kama mbili tayari amelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, hii hali inakuwaje? Hatuoni kuwa yawezekana ukali wa hiyo pombe iko juu sana? Kuna haja ya kutazama na pia kuboresha eneo la kuzuia uingizaji wa bidhaa hizi au vyakula tunavyoingiza pamoja na dawa ili kuweza kuzuia badala ya zimeingia nchini tunakwenda kukagua, halafu tunakwenda kuteketeza kumbe tunaathiri uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *solution* kubwa au jibu sahihi lililo kubwa ni namna ya kuzuia ili wasiingize nchini ama wasitengeneze kwa kadri ambavyo mamlaka zetu zikifanya uchunguzi na inaona kwamba kwa vyovyote vile haijaweza kufanikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia eneo lingine ambalo nazungumzia ni kwamba kwa namna ya pekee Serikali iongeze bajeti ya Wizara ya Afya. Hii nchi tumekuwa wengi, yaani takwimu ya nchi ya watu milioni 61 mahitaji ya magonjwa mbalimbali yameibuka kiasi kwamba hata Serikali haiweze kukabiliana na hali hii kwa sababu bado ina deni kubwa na mapato yetu bado ni madogo. Ushauri wangu ni kwamba tutazame upya namna ambavyo bajeti hizi tunazitazama. Hata kama tuko zaidi ya trilioni moja pointi kadhaa basi tuangalie maeneo nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee pia kama inawezekana ruzuku ya wazee, kwa maana ya wazee katika bima yao ama kitambulisho kinachoonekana, lakini wakaongezewa. Nchi kama Tanzania tunaweka ruzuku kwenye mafuta, lakini mwenye gari ana uwezo kuliko maisha ya mtu ambaye ni Mtanzania, unapoweka ruzuku kwenye mafuta ya magari halafu huku kwenye afya tunaacha, hasa kwa makundi haya ya wazee pia kwa makundi haya ya mama na mtoto. Jambo hili hebu litazamwe namna gani tunaweza tukapata fedha mahali tukaboresha eneo hili na kuijengea uwezo *MSD* ili iweze kufanikisha jambo hili kwa namna ya pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni uzuiaji au matumizi ya dawa hizi za kuzuia au kuangamiza mbu. Nchi zingine zinaagiza kwetu zinanunua, sisi kwetu msambazo umekuwa mdogo na namna ya kuzipata au kuzipunguza gharama ili tuweze kudhibiti mazalia ya mbu na namna ya kuyateketeza bado mwendo wetu ni mdogo. Tutazame namna gani tunaweza tukatekeleza programu ya kitaifa ya kuweza kuzuia ama kuangamiza mbu kwenye masalia na maeneo mbalimbali ili tuweze kufanikiwa kwa namna ya pekee ambapo itaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango wangu huu kwa namna ya pekee niishukuru Serikali, niipongeze Serikali kwa kazi kubwa inayofanyika. Tuiombee nchi yetu kuelekea uchaguzi. Hao wanaotusema vibaya, wanaosema Serikali haijafanya kazi wanatembea kwenye barabara tulizojenga, wanapiga simu kwa mitandao tuliojenga, wanawasha umeme ambao Serikali imekwishatekeleza, pia wanapanda ndege na treni. Hawa tuwaache waendelee, Watanzania watawaelewa tu. Sisi jukumu letu liwe kwenda mbele na kutekeleza na kuitakia nchi yetu uchaguzi mwema wa mafanikio. Bado Watanzania wana imani kubwa kwa chama chetu na kwa Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunisikiliza na kwa muda wako, ninashukuru sana, ninaunga mkono hoja kwa 100%. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zacharia Issaay, nilimwita Balozi Liberata Mulamula atafuatiwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel.

**MHE. BAL. LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi nichangie kwenye hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Afya. Ninaomba kwanza kabisa na mimi nitoe pongezi nyingi za dhati kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa hotuba nzuri na timu yake yote akiwemo Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia nimpongeze sana sana Profesa Janabi kwa ushindi wa kishindo na kuaminiwa kushika nafasi ya Mkurugenzi wa *WHO* Kanda ya Afrika. Profesa Janabi kama upo nakukaribisha kwenye uwanja wa diplomasia za kimataifa na kikanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia niungane na wenzangu kumshukuru sana, sana, sana Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel kwa msaada wake mkubwa. Kama wengine walivyosema, hata ikiwa usiku wa manane una dharura Mheshimiwa Dkt. Mollel atakusaidia pamoja na msaidizi wake Daniel Pyuza, kwa kweli wamekuwa msaada sana, sana, sana na hawachoki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba uniruhusu niwapongeze madaktari na wafanyakazi wote wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Mloganzila, Hospitali ya *MOI*, *Jakaya Kikwete Cardiac Institute*. Kwa namna ya pekee niwashukuru sana madaktari wa *Mbeya Referral Hospital.* Nimefurahi kumuona Mkurugenzi wa *Mbeya Referral Hospital* hapa ambaye niliunganishwa na Mheshimiwa Dkt. Mollel wakati nilikuwa na dharura ya kijana wetu alikuwa amepata ajali ya bodaboda. Kwa kweli wamefanya miujiza kuweza kumsaidia na akapona na hasa naomba kupitia kwa huyo Mkurugenzi kama bado yupo anifikishie shukrani zangu kwa daktari mtaalam wa *neurosurgeon*. Ni daktari kijana, anaitwa Dkt. Boazi; kwa kweli tunao madaktari. Katika kumsaidia huyu kijana ilikuwa kwa kweli ni *medical miracle*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hizo hospitali nilizozitaja ikiwemo ya Benjamin Mkapa ninawashukuru sana, sana kwa *customer service,* yaani huduma zao ni ya viwango vya kimataifa. Ukienda kwa kweli unasema kumbe tunaweza. Maana kwa wale ambao wameenda Benjamin Mkapa siombei kwamba muende, lakini ikitokea umeenda ukifika tu utakuta wale vijana waliovaa *uniform* huko nyuma yameandikwa maandishi makubwa uliza nikusaidie na kweli wanatusaidia. Kwa hiyo, naomba kupongeza menejimenti ya hospitali hiyo kwa kweli mmeboresha sana huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa msemaji wa mwisho bahati nzuri ni kwamba mengi yamesemwa. Mimi ninaomba nijikite katika maeneo machache tu. Kwanza, kabisa ninaomba niungane na wenzangu nimshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali na Wizara kwa mikakati thabiti ambayo imeinua sana sana sekta ya afya na imeendelea kuboreka na upatikanaji wa huduma za afya kwa kweli umeimarishwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba uniruhusu niongelee kuhusu Taasisi ya *Benjamin William Mkapa Foundation*. Nilibahatika kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Taasisi hii na Mheshimiwa Msadifu wa Taasisi hii Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye ni Setra wa Taasisi hii. Ninaongelea kwa uchungu sana, ninaomba unisikilize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takribani miaka 19 taasisi hii imekuwa ikichangia sana kupunguza uhaba wa wataalam wa afya hususan katika maeneo yenye changamoto kubwa ya wataalam nchini kote. Kwa ushirikiano kati ya Wizara ya Afya na wadau wa maendeleo mpaka sasa taasisi hii imechangia ajira za wataalam wa afya wapatao 7,322 wakiwemo madaktari, wauguzi na kada nyingine mbalimbali nchini kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ninasema kwa masikitiko. Kufuatia tamko la *Executive Order* ya Rais Donald Trump, na kama mnavyofahamu, kufatia tamko hilo Shirika la Misaada la Marekani *(USAID)* lilisitisha na kufuta misaada kwa miradi ya afya takribani 17 iliyokuwa inatoa mchango mkubwa katika kutoa huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mradi huo mkubwa ni mradi uliojulikana kama “Afya Endelevu” uliokuwa unasimamiwa na taasisi ya *Mkapa Foundation* ambapo ulitoa ajira kwa wataalam wa afya 1,299 ambao walikuwa wanatoa huduma za afya katika hospitali na vituo vyote vya afya vya umma nchini, vituo 701 kwenye mikoa 22

yote ya Tanzania ikiwemo Mkoa wa Kagera, Kanda ya Ziwa na mikoa mitano ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusitishwa kwa ghafla kwa mradi huu adhimu kumesababisha kusitishwa kwa ajira ya watumishi hao 1,299. Hili limekuwa ni tishio na limeathiri kwa kiasi kikubwa kasi ya upatikanaji wa huduma za afya hasa za mama na mtoto, UKIMWI na kifua kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua juhudi za Serikali kupitia Wizara ya Afya pamoja na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambayo imekuwa ikilifanyia kazi suala hili. Kulingana na udharura na umuhimu wa jambo hili kuna wengine ambao wamekuwa wanabeza wanasema kufungwa kwa miradi ni kwamba tulikuwa hatunufaiki, kwamba fedha zilikuwa zinarudi kule zilikotoka. Mimi ninataka kusisitiza hili, kwamba kwa kweli hapa napoongea wafanyakazi 1,299 katika sekta ya afya nchini kote wamesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi napongeza juhudi zinazoendelea, Mheshimiwa Waziri Jenista anajua, nimekwishaongea naye kuhusu hili. Mimi ninaomba Mheshimiwa Waziri akija kutoa hitimisho tafadhali atueleze ni wapi tumefikia katika kuhakikisha kwamba watumishi hawa wanabakizwa katika vituo husika na kuendelea kutoa huduma adhimu za afya kwa wananchi. Amesikia kilio cha Waheshimiwa Wabunge, kuna vituo vya afya, lakini havina wafanyakazi na hawa wafanyakazi tayari walikuwa kwenye ajira sasa wanakwenda mtaani. Kwa hiyo, nitashukuru sana kusikia tamko la Serikali kuhusu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niongelee suala ambalo limeongelewa sana, suala la kuhusu gharama za matibabu ya *dialysis* nchini. Ninatambua gharama, hili ni kama janga kubwa sana. Nina ndugu yangu ambaye anakwenda mara tatu kwa wiki na kila akienda Muhimbili kupata hii *dialysis* analipia shilingi 150,000 na inabidi aende mara tatu. Kwa hiyo, kwa wiki wanalipa shilingi 450,000. Kwa hiyo, *you can imagine,* ni mtu gani ambaye ana

uwezo huo? Na hii *dialysis* ikiendelea inaendelea maisha. Kwa hiyo, ninaomba hili liangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna gharama pia ambazo zinaitwa *catheter in session,* Muhimbili zinauzwa hadi shilingi 2,000,000 kwa *arteriovenous fistula* na shilingi milioni 2.3 kwa *permcath insertion, one PPM,* najua madaktari wako wanaelewa kutegemea wanamwekea ipi. Je, ni wangapi wana uwezo huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi narudia kilio cha Wabunge wenzangu kuhusu hili suala, kwa kweli liangaliwe na Mkurugenzi wa *NHIF* mdogo wangu Irene analijua, ndugu zangu walikwishakwenda kumwona lakini akawaambia mikono yake imefungwa. Sasa sisi tufanyeje kwa kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho *of course* limeongelewa suala la mfuko wa afya, ninashukuru Mbunge mmoja ameongelea kuhusu wazee. Kwa kweli wazee katika nchi nyingine wanabebwa vizuri sana, lakini huku naona wazee wananyanyapaliwa. Mimi nina mama mkwe ana miaka 98 amenipigia simu ameenda kwa daktari ameandikiwa dawa za moyo wakamwambia kwamba kumbe hazimo tena kwenye hicho kifurushi na hakuwa na taarifa.

Kwa hiyo, mimi ninasema jamani ninaomba hiyo bima ya afya sijui itakuwa kwa wote, lakini na vifurushi angalau wazee nao wapewe *priority* na *preference treatment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo naomba niunge mkono hoja, asilimia 100 kwa 100, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Balozi Mulamula, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Naibu Waziri tuna wageni ndani ya Ukumbi wa Bunge.

Wageni 58 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, walimu watatu, wazazi watatu na wanafunzi 52 wa Shule ya Sekondari Daora kutoka Jijini Dar es Salaam, hebu tuwaone, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tuna wageni 38 wa Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza hawa ni wanafunzi 35, walimu watatu wa Shule ya Msingi Gosheni kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee ninaomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza vyema miaka minne kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa Mheshimiwa Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa na pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Spika na Naibu Spika na pia uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Afya, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ya ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi chake akiwa Waziri wa Afya, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Awamu ya Sita, Serikali kupitia Wizara ya Afya, imetekeleza miradi mingi ya miundombinu ya afya. Katika kutambua ufanyaji kazi mzuri wa Wizara ya Afya, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amepokea tuzo ya heshima ya *The Gates Goalkeepers Award* kutambua juhudi zake za kupunguza vifo vya mama na mtoto kwa 80%, kuboresha upatikanaji huduma za afya na kukuza usawa wa kijinsia katika sekta hiyo. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kiongozi huyo anakuwa wa saba duniani na wa kwanza Afrika kutunukiwa tuzo hiyo ambayo hutolewa kwa viongozi waliowezesha

nchi zao kuharakisha maendeleo kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu *(SDG)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na kwa kushirikiana na TAMISEMI, imeendelea kutekeleza kwa ufanisi mkubwa miradi ya Hospitali ya Wilaya na vituo sita vya afya vya Kata za Ikukwa, Ilembo, Santilya, Ilungu, Swaya na Utengule Usongwe. Vituo vyote sita vinaendelea kutoa huduma kwa ufanisi mkubwa hasa huduma ya watoto na akina mama. Hospitali ya Wilaya pamoja na vituo vya afya vimekamilika na maandalizi ya vifaa tiba vya nyongeza yapo katika hatua za mwisho ili vianze kutoa huduma kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki tunapopambana na majanga, magonjwa ya mlipuko ikiwemo la *corona virus (covid-19)*, tumejifunza umuhimu wa utayari wa huduma ya afya hasa kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali na hivyo Serikali iongeze msukumo wa kupeleka vifaa tiba na kumalizia vituo vya afya na zahanati zilizojengwa kwa nguvu za wananchi. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wananchi wa Kata za Igoma, Isuto wamejenga vituo vya afya na kuna maendeleo mazuri ya kukamilisha na pia katika Mji Mdogo wa Mbalizi wenye wakazi zaidi ya 150,000 kuna uhitaji wa ujenzi wa Hospitali ya Mji wa Mbalizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo napendekeza Serikali kutoa kipaumbele katika bajeti hii kwa vituo vya afya hivi ili kukamilisha vifaa tiba na watalaamu ili vitoe huduma kikamilifu. Pamoja na Vituo vya Afya vya Ilungu, Igoma, Isuto na Ulenje, napendekeza kukamilisha zahanati zote ambazo zimejengwa kwa nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maboresho ya miundombinu ya hospitali na vituo vya afya, Serikali ihakikishe bajeti ya mwaka huu inaendelea kujielekeza zaidi kwenye ajira ya madaktari na watumishi wa afya kwa ujumla. Pamoja na maboresho hayo ya miundombinu, vifaatiba na ajira kwa watumishi,

napendekeza Serikali ikamilishe mpango kabambe na Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote na hasa kwa wazee na wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Serikali iangalie jinsi ya kuboresha Bohari ya Dawa *(MSD)* ikiwa ni pamoja na Serikali kuhakisha inaongeza mtaji wa *MSD* na kuboresha muundo wa shirika ili uendane na jukumu kubwa la kutoa huduma kwa tija na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki ambapo Serikali inaangalia kuanzisha Bima ya Afya kwa Wote, kipaumbele kielekezwe kwenye maboresho ya upatikanaji wa dawa pamoja na kuwezesha huduma ya hospitali zetu kutoa huduma bora zaidi kwa ukanda huu wa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MUNIRA MUSTAFA KHATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza viongozi wa Wizara ya Afya kwa kuwasilisha bajeti yenye mwelekeo wa kuimarisha huduma za afya kwa wananchi wote. Bajeti hii imegusa maeneo nyeti yanayohitaji msukumo wa pamoja kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza la kuchangia ni kuhusu huduma za kinga dhidi ya magonjwa ya mlipuko na yasiyoambukiza. Tunapoendelea kuimarisha miundombinu, ni muhimu fedha zaidi kuelekezwa kwenye elimu kwa umma kuhusu afya ya kinga, chanjo, lishe bora na namna ya kujikinga dhidi ya magonjwa kama kisukari, shinikizo la damu na saratani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele vya bajeti hii vimejikita kwenye kuimarisha huduma bora kutoka ngazi ya msingi hadi Taifa. Ni vyema Serikali ikahakikisha kuwa vituo vya afya vya vijijini vinapewa kipaumbele kwa vifaa tiba, huduma za dharura na wataalamu wa kutosha ili wananchi wasilazimike kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono juhudi za Serikali katika kuharakisha utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Hata hivyo, elimu kwa wananchi kuhusu bima ya afya bado ni ndogo. Bajeti hii isaidie kampeni kubwa za uhamasishaji hasa vijijini ili wananchi waelewe thamani ya kuwa na bima ya afya na namna ya kujiunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la afya ya uzazi, mama na mtoto, tunapaswa kuongeza uwekezaji katika huduma rafiki kwa wajawazito na watoto wachanga, hasa katika vituo vya ngazi ya kata. Vifo vya mama na mtoto vinaweza kupungua endapo huduma hizi zitapatikana kwa wakati na kwa ubora unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya afya haiwezi kuimarika bila wataalamu wa kutosha. Bajeti hii izingatie kwa makini ajira mpya za wahudumu wa afya, uendelezaji wa mafunzo ya ndani kwa wataalamu waliopo na mazingira mazuri ya kazi ili kuongeza morali na kupunguza uhamaji wa wataalamu kwenda sekta binafsi au nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kujivunia kuwa Serikali inalenga kuimarisha huduma za ubingwa na ubingwa bobezi. Hii itapunguza kwa kiasi kikubwa rufaa za wagonjwa kwenda nje ya nchi. Hata hivyo, tunahitaji kuwekeza katika vifaa vya kisasa na wataalamu mahiri katika hospitali zetu za rufaa za kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la kuimarisha tiba utalii ni zuri na linaweza kuiongezea nchi mapato. Hata hivyo, mafanikio ya tiba utalii yanategemea ubora wa huduma za afya, utawala bora wa sekta na mazingira rafiki kwa wageni. Bajeti hii itenge fedha za kujenga vituo vya mfano na maabara za kisasa zinazokidhi viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tiba asili na tiba mbadala ni eneo ambalo linahitaji uangalizi wa karibu. Ni muhimu kuhakikisha huduma hizi zinasimamiwa kitaalamu kwa kuzingatia viwango vya

usalama, ufanisi na uthibitisho wa kisayansi ili kulinda afya ya Watanzania na heshima ya tiba hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza jitihada za Serikali katika kuimarisha mfumo wa TEHAMA katika afya ili kuharakisha usajili wa wagonjwa, ukusanyaji wa taarifa na ufuatiliaji wa huduma. Hili ni eneo ambalo linaweza kuongeza ufanisi mkubwa wa sekta ya afya endapo litawekewa bajeti ya kutosha na usimamizi makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, naiomba Serikali kuhakikisha kuwa utekelezaji wa bajeti hii unaendana na thamani halisi ya fedha *(value for money)* na kwamba wananchi wawe sehemu ya ufuatiliaji wa miradi ya afya inayotekelezwa katika maeneo yao. Ushirikishwaji wa jamii ni nguzo muhimu ya mafanikio.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Afya, Mheshimiwa Jenista Mhagama (Mb.), Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel (Mb.), Katibu Mkuu - Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe, Naibu Katibu Mkuu - Ndugu Ismail Abdallah Rumatila, Mganga Mkuu wa Serikali - Dkt. Grace Elias Magembe, wataalamu wa Wizara na wadau wa afya kutoka sekta binafsi kwa kazi nzuri wanazofanya kwenye kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia kuhusu changamoto mbalimbali zinazoathiri huduma za afya hapa nchini na nitapendekeza namna ya kukabiliana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za afya ni mojawapo ya haki za msingi za binadamu na ni kipengele muhimu katika kuhakikisha tunakuwa na jamii yenye afya bora. Katika kitabu kitakatifu ninachokiamini, kuna mistari 108 ya Biblia kuhusu afya ya kimwili, jambo ambalo linatakiwa kupewa kipaumbeke na mamlaka zilizowekwa kutuongaza na Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mathayo 15:30 - watu wengi sana wakamjia wakiwaleta vilema, vipofu, viwete, bubu na wengine wengi waliokuwa wagonjwa, wakawaweka mbele ya miguu yake, naye Yesu akawaponya. Mathayo 9:35 - Yesu alitembelea miji yote na vijiji, akafundisha katika masunagogi yao akihubiri habari njema ya ufalme wa Mungu, na kuponya magonjwa yote na udhaifu wa kila namna bila kulipua gharama yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma bora za afya zinahitaji kuwa na upatikanaji wa vifaa, wataalamu wa afya, miundombinu bora na usimamizi thabiti. Hata hivyo, huduma za afya hapa Tanzania zinakabiliwa na changamoto nyingi zinazopunguza ubora na upatikanaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Watanzania wanatofautiana sana kwa uwezo wa kifedha. Kuna watu wa kipato cha juu ambao ni wachache sana kwenye jamii na watu wa kipato cha chini ambao ndio wengi. Kiuhalisia, huduma za afya ni za gharama kubwa ambazo watu wa kipato cha chini hasa wanaoishi vijijini hushindwa kuzimudu. Kama mwananchi hana bima ya afya ya gharama anayomudu hii huwafanya watu wengi wa kipato cha chini kushindwa kugharamia huduma za matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nchi yetu ina upungufu wa wataalamu wa afya katika nyanja mbalimbali. Wataalamu wa afya kama vile madaktari, wauguzi na mafundi sanifu wa vifaa tiba, ni changamoto kubwa katika sekta ya afya hapa Tanzania. Katika maeneo mengi yanayotoa huduma za afya hasa vijijini kwenye vituo vya afya na zahanati, idadi ya wataalamu wa afya haitoshelezi mahitaji ya wagonjwa. Hili husababisha mzigo mkubwa wa kazi kwa wataalamu wachache waliopo. Wataalamu wengi wa afya wanakosa muda wa kuhudumia wagonjwa kwa ufanisi, jambo linalosababisha msongamano katika vituo vya afya na kupunguza ubora wa huduma. Upungufu huu huongeza muda wa kusubiri kwa

wagonjwa na mara nyingi husababisha wagonjwa kukosa huduma muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, katika maeneo mengi hasa yale ya vijijini (vituo vya afya), kuna changamoto ya ukosefu wa miundombinu bora na vifaa tiba. Katika maeneo haya, vituo vya kutoa tiba vinakosa vifaa muhimu kama vitanda vya wagonjwa, majokofu ya kuhifadhi dawa/maiti, vifaa vya uchunguzi kama skana, *ultra sound machines* na mashine za kisasa za upasuaji. Pia kuna ukosefu wa magari ya kubeba wagonjwa kwa mfano, Hospitali ya Wilaya ya Mabogini iliyoko Jimbo la Moshi Vijijini haina gari la wagonjwa *(ambulance)*. Ukosefu wa vifaa tiba unaathiri uwezo wa vituo hivi kutoa huduma bora kwa wagonjwa, jambo linalosababisha baadhi ya wagonjwa kusafiri umbali mrefu kutafuta huduma za afya katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, pamoja na Serikali kupitisha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, lakini bado kuna changamoto ya watu kujiunga na Mfuko wa Bima wa Afya. Kwa watu wa kipato cha chini na wasio na ajira, ukosefu wa bima ya afya ni changamoto inayowazuia kupata matibabu kwa gharama nafuu. Wengi wanakosa bima ya afya kutokana na gharama kubwa za bima au kukosa mwamko kuhusu umuhimu wa bima ya afya. Kwa mfano, kifurushi cha bima ya afya cha bei ya chini cha Ngorongoro Afya kwa mtu mmoja mwenye miaka kati ya 18 hadi 35 ni shilingi 432,000. Bei hii ni kubwa kwa kundi la watu hawa wenye kipato kidogo. Ukosefu wa bima ya afya kunawafanya watu kushindwa kulipia matibabu yanayotokea kwa dharura bila kujipanga au huduma nyingine za afya kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuhalisia, wataalamu wengi wa afya wana ari ndogo ya kufanya kazi maeneo ya vijijini. Hii ni kutokana na mazingira magumu ya kazi na ukosefu wa miundombinu muhimu huko vijijini. Vijijini kuna shida ya nyumba za kupanga, maji na umeme. Madaktari wengi na wataalamu wengine wa afya wanapendelea kufanya kazi mijini ambako kuna miundombinu bora

na fursa zaidi za maendeleo. Hali hii inasababisha ukosefu wa huduma za afya za karibu kwa watu wa vijijini. Kutokana na hali hii, wananchi hulazimika kutafuta huduma za tiba mijini na kuongeza mzigo wa kifedha kwao na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika baadhi ya zahanati za Serikali, kuna changamoto ya ukosefu wa dawa muhimu, chanjo za watoto, vifaa tiba kama *gloves* za kutoa huduma kwa akina mama wanaojifungua, sindano na mashine za kupimia matatizo mbalimbali ya kiafya. Uhaba wa vitu hivi huathiri huduma za afya katika maeneo mengi vijijini. Katika baadhi ya zahanati, wagonjwa hupewa dawa zisizo kamili au hutakiwa kununua dawa kwa gharama zao. Akina mama wanaojifungua hulazimika kununua baadhi ya vitu kama *gloves* na sindano. Mambo yote haya huishia kuweka mzigo mkubwa wa kifedha kwa wagonjwa na huathiri sana familia maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika baadhi ya magonjwa, nchi yetu imekosa sera na mipango thabiti ya kupambana nayo. Kwa mfano, magonjwa yanayotesa raia wetu na yenye gharama kubwa za tiba kama yale ya figo, selimundu, upungufu wa damu na kansa hayana sera inayoelekeza namna ya kuwasaidia wananchi wasio na uwezo wa kifedha kukabiliana nayo. Sera na mipango thabiti ya Serikali kukabiliana na magonjwa haya ni muhimu ili kuhakikisha kuwa kuna upatikanaji wa huduma za afya kwa watu wanaokabiliana na magonjwa haya. Kutokuwepo na mipango madhubuti ya kutibu magonjwa haya kunafanya wananchi maskini kufa kwani tiba za haya magonjwa ni za gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupambana na changamoto hizi, ninaishauri Serikali ifanye yafuatayo:-

(i) Serikali iongeze bajeti ya sekta ya afya ili isaidie kuboresha huduma za afya na kuhakikisha huduma bora zinapatikana kwa wananchi wote na kuokoa maisha ya raia.

(ii) Serikali ifanyie mapitio na kuweka kifurushi cha gharama ndogo cha bima ya afya kwa watu wa kipato cha chini. Hii itawasaidia watu wa kipato cha chini kupata huduma za afya kwa gharama nafuu na kupunguza mzigo wa kifedha kwa familia maskini.

(iii) Changamoto ya uchache wa wataalamu, ninaishauri Serikali ipeleke wataalamu wa afya wa kutosha katika maeneo yenye uhitaji, hasa huko vijijini. Mafunzo ya mara kwa mara yanahitajika ili kuhakikisha kwamba wataalamu wa afya wanaendelea kuwa na ujuzi wa kisasa na uwezo wa kutoa huduma bora kwa wagonjwa.

(iv) Serikali ipeleke vifaa muhimu kama vitanda vya wagonjwa, vifaa vya uchunguzi kama *scanner* na mashine za kisasa za upasuaji katika vituo vyote vya afya na hasa vile vilivyopo vijijini. Pale panapohitajika gari la wagonjwa, Serikali ipeleke *ambulance*.

(v) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine kama viongozi wa dini na Wabunge wahamasishe wananchi kuhusu umuhimu wa kuwa na bima ya afya. Elimu hii inaweza kutolewa kwenye mikutano ya dini, siasa, mashuleni, vyuoni, ili kuwafikia watu wengi zaidi na kuwasaidia kujua umuhimu wa kuwa na bima ya afya. Kampeni za uhamasishaji zinaweza kuwasaidia watu kuelewa umuhimu wa bima ya afya na kusaidia kuongeza idadi ya watu wanaopata bima ya afya.

(vi) Kutokana na mazingira magumu ya kazi na ukosefu wa miundombinu muhimu huko vijijini, Serikali itoe motisha maalumu ya kifedha kwa wafanyakazi wa afya wanaofanya kazi katika mazingira magumu vijijini.

(vii) Kuhusu uhaba wa dawa na vifaa tiba maalumu, ninaishauri Serikali itoe ruzuku ya dawa na vifaa tiba muhimu ili kuhakikisha wagonjwa wanapata dawa wanazohitaji. Ruzuku hii itasaidia

kupunguza gharama kwa wagonjwa na kuongeza upatikanaji wa dawa muhimu.

(viii) Serikali iwe na sera inayoelekeza namna ya kukabiliana na kutibu magonjwa yanayotesa raia wetu na yenye gharama kubwa za tiba kama figo, selimundu, upungufu wa damu na kansa ambayo tiba yake ni gharama kubwa. Serikali ije na mipango madhubuti ya kitaifa ya kusaidia wagonjwa hawa na kuweka mifumo ya kufuatilia wagonjwa hawa popote pale walipo kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba changamoto za huduma za afya zinahitaji juhudi za pamoja na mipango thabiti ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Ukerewe nitoe shukrani kwa kuanza kwa ujenzi wa hospitali ya rufaa ngazi ya mkoa jimboni Ukerewe, kukamilika kwa hospitali hiyo itakuwa ni mkombozi wa maisha ya wananchi wengi. Niombe yafuatayo:-

(i) Majengo ya awali yaliyokuwa yanajengwa na SUMA JKT yaliyopo eneo la hospitali ya wilaya yakamilishwe haraka na kukabidhiwa halmashauri ili yapunguze shida ya miundombinu katika hospitali ya wilaya.

(ii) Ifanyike tathmini ya majengo yanayotumika kwa sasa kama ofisi za halmashauri na kama yatakidhi basi kianzishwe chuo cha uuguzi na uganga kwa sababu pale tuna jengo jipya la halmashauri, litakapokamilika basi majengo haya hayatakuwa na kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la upatikanaji wa huduma za afya kwa makundi ya wajawazito na watoto bure kama ilivyo sera bado lina changamoto nyingi sana, naomba kushauri Wizara iwe na kitengo maalum cha kufuatilia utekelezaji wa sera hii ili changamoto zinazojitokeza kwenye eneo hili ziwe zinapatiwa ufumbuzi na kuondoa malalamiko mengi kwenye jamii na kuepusha vifo kwa makundi haya.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea nimwite sasa Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kunisemea na kuisemea Wizara yetu. Nianze kwa kumshukuru Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye kwa kweli yote ambayo mmeyasema hapa na yote ambayo yanaonekana yamefanyika vizuri kwenye sekta ya afya yanatokana na juhudi yake yeye mwenyewe Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru kwa kuendelea kuniamini kwa miaka mitano na sasa tunaelekea ukingoni. Pia niwashukuru wananchi wa Siha kwa kuendelea kuniamini wakati wote na kunipa ushirikiano na niwaambie ninakuja tena kwa nguvu sana na kwa wale ambao wananyemelea kama kawaida yetu tutaenda kuwapiga na kimsingi wanaenda kufilisika, kwa hiyo, thelathini hawatarudi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Waziri wangu Mheshimiwa Jenista Mhagama. Sisi sote ni mashahidi hasa Naibu Mawaziri wenzangu kama ambavyo amekuwa kiranja wetu wakati wote hapa na watu hawajajua wakati mwingine alikuwa anachezea namba ambayo unacheza miguu yote unachezea Wizara zote na ameweza kufanya. Kwa hiyo, sasa alipo Wizara ya Afya ni *caterpillar* limeletwa kulima bustani na bustani itavurugwa kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niongee na wananchi wa Peramiho kwa kweli sisi watu wa Wizara ya Afya na madaktari wazuri waliozungumziwa hapa, watumishi wote wa Wizara ya Afya wanawaomba watu wa Peramiho waturudishie Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa sababu kwa kweli tumeletewa ndiyo tunaanza ku-*enjoy* utamu wake wakati tunaenda kulimaliza Bunge kuanza uchaguzi, tunamwomba tena arudi ili aweze kuendelea kuiongoza hii sekta yetu ya afya na tunaomba Rais kwa kweli huyu tunampenda na anafanya kazi nzuri na ameiunganisha Wizara yetu ya Afya na kazi inakwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Waheshimiwa Wabunge wenzangu mmesema sifa zetu nyingi za Mheshimiwa Waziri, lakini hata na mimi mkisema tumetibu wagonjwa, tumefanya nini, lakini ninataka niwaambie ukweli sifa hizo siyo za kwangu mimi wala siyo za Waziri kwa kweli ni watendaji walioko hapa nyuma. Kwa sababu kazi yetu sisi ukitupigia simu tunachukua simu tunapiga simu dakika tatu. Pia kuna mwingine ambaye kama alikuwa amelala na mke wake au mume wake anaondoka masaa matatu kwenda kuhakikisha huduma inayotakiwa kutekelezwa inaenda kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwapongeze Wakurugenzi wetu wa Hospitali yetu ya Jakaya Kaka yangu Dkt. Kisenge, kaka yetu Profesa Janabi; *MOI* kaka yetu Dkt. Ulisubya, lakini Dkt. Makubi wa Benjamin Mkapa, viongozi wetu wa hospitali zote za kanda nchini na mikoa tunawashukuru sana. Mmeona sasa matokeo ya kazi ambayo tumekuwa tukiwapigia kuwaomba kuwasaidia Wabunge katika maeneo mbalimbali na mmeona matokeo yake katika siku hii ya leo tukipitisha bajeti yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu ambao wanakuwa *background* mara nyingi hawatajwi. Ninaomba tu niseme Wabunge mmesema mambo mengi hapa, kama mimi nimepokea simu zenu 100 ninataka kuwaambia kuna mtu amepokea 70 kati ya hizo 100 na siyo mwingine ni ambaye sasa ni msaidizi wa Waziri ambaye

alikuwa msaidizi wangu na siyo mwingine ni Daniel Pyuza ambaye amesaidia sana na amewasaidia ninyi Wabunge mliopo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilisema nitumie hii fursa wakati tunaenda kumaliza Bunge kwa kwenda kwenye uchaguzi nimwambie Daniel Pyuza ahsante sana kwa kunisaidia na hata ndiyo maana umefanya kazi nzuri. Watu walipofikiri jembe kama Mheshimiwa Jenista Mhagama nani atembee naye kwa sababu ni *caterpillar* limekuja kulima bustani alionekana yeye pamoja kuwa ni mfamasia, hajasoma utawala, lakini ameonekana yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna afisa wetu wa Bunge, Alpha Cholobi tunakupongeza sana, tumejaa makaratasi hapa, lakini umekuwa ukihangaika na Katibu Mkuu kufanya mambo yote haya. Pia nimalizie kwa *heroes* wetu; dada yangu amesema vizuri, dada yangu Mheshimiwa Esther Matiko kuhusu daktari aliyegundua roboti, sitaki kulirudia hilo limefika na limeingia vizuri kama ambavyo nilitamani liingie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye la *innovations* ma-*nurse* wamekuja juu sana na wamekuwa kila tukihudhuria mikutano yao unaona kwenye *innovations* katika maeneo mbalimbali. Kuna mmoja anaitwa Wilson Fungameza walishindana watu 500 duniani na akashika namba tano kwenye *innovation* na akaenda Uingereza na akachukua nishani na akairudisha Tanzania hao ndiyo vijana wetu wanaotusaidia kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme kuna wengi wameandika vitabu na wamefanya vitu mbalimbali lakini ninaomba nimtaje mmoja atayewasilisha *heroes* wanaofanya mambo makubwa kwenye hii. Kuna *nurse* mmoja anaitwa Stella Ndogwisango, *nurse* huyu amemwokota mtoto mwenye ulemavu wa viungo na tundu kwenye moyo aliyetupwa uwanjani, lakini sasa amemtibu huyo mtoto. Pia ameendelea kumjali kama mtoto wake na yuko naye

hapa, amekuja naye hapa. Mtoto huyo ana miaka miwili sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *nurse* huyo hajaishia hapo, ndiyo maana ninawaambia Waheshimiwa Wabunge mmetuambia matatizo mengi sana hapa yanayotakiwa kutatuliwa ambayo ni kwenye majimbo yenu na maeneo mbalimbali. Ninachotaka kuwaambia Wizara ya Afya ina watumishi wazuri wa kutatua hayo matatizo, lakini pia Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kama amefanya haya makubwa ambayo ninyi mmekuwa mkiyasema hapa haya mengine mliyoyasema kwa kipindi hiki kifupi ni madogo sana hata tusipowajibu ninaombeni mwende kuamini kwamba yanaenda kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa *nurse* huyo amekwenda alikuwa wodini amelazwa na mtoto wake, kuna ajali ya basi la Sabena lilitokea Shinyanga, halafu walipokuwa wamelezwa majeruhi wakaletwa wodini kukawepo na mtoto wamekaa naye mwezi mzima hakuna ndugu yeyote aliyewatembelea wakati wagonjwa wengine wamelazwa na ni mtoto ana miaka mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati anaondoka yule mtoto akawa anamlilia, kutafuta ndugu na marafiki haikuwezekana kupatikana, akaamua kumchukua kumfanya mtoto wake. Huyo *nurse* alivyompeleka huyo mtoto kumfanya ndugu yake nyumbani, wakati anaenda nyumbani, mtoto yule kila akiona gari linapita analia anasema gari linakuja kutugonga. Anasema tunakufa, ndiyo mwisho wakarudi kuanza kuangalia *list* za wagonjwa wakagundua mama yake aliumia kichwa na yuko Bugando anatibiwa na amefungwa mikono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo mtoto alipopitishwa pembeni ya mama yake, mama yake aliweza kujigusa na kumtambua mtoto wake. Baada ya hapo pamoja na huyo mama kukaa wodini miezi mitano, lakini mama huyo akaanza kupata nafuu. Huyo mama

alikuwa ni Mkenya na yuko Kenya kwenye nchi yao anaendelea na mtoto wake. Hayo ndiyo mambo ambayo yanawatokea watu wetu wodini, nimesema nitumie hayo leo kuonesha kwamba tunatambua mambo makubwa yanayofanyika na wataalam na watu wetu kutoka chini mpaka kule chini wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mmetuambia mambo mengi, mmetuambia matatizo mengi, mmeeleza mambo mengi ambayo nikiangalia mliyoyasema ni zaidi ya makaratasi mengi na yote haya hamjatuambia sisi mnamwambia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia sisi. Hata hivyo, wakati mnamwambia msisahau Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan huyo ndiye yeye ambaye kwenye sekta ya afya amewaletea nishani ya *Goalkeepers Award* ambayo ni kwa Marais wa Afrika yeye ndiye pekee aliyewahi kupata. Ametuingiza katika *list* ya Marais saba duniani waliowahi kupata nishani hiyo na haijatokea kwa bahati mbaya, imetokea kutokana na huu uwekezaji mkubwa aliouwekeza kwenye sekta ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia huyo ndiye huyo aliyeifanya Tanzania sasa imeingia kwenye nchi ya pili kwa Afrika Mashariki kuwa na *PET/CT scan*. Ametuingiza kwenye nchi ya tatu kuwa na *PET scan* kwenye nchi za *SADC* na nchi ya tisa kwa kuwa na *PET scan* kwenye nchi tisa ambazo zipo Afrika. Maana yake ukiona ni nchi tisa ukilinganisha na nchi nyingi zilizo Afrika siyo jambo rahisi kuwa nalo. Huyo Rais ambaye leo mmetuambia matatizo yenu tumpelekee, hapa ninaombeni mtuamini tumeyachukua, tumeya-*record* huyu huyu ndiye sasa tunampelekea ili aende kuyatatua. Kwa hiyo, haya yote yanatatulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jiulize kwamba leo ukipanga *ambulance* 727 ukaleta hapa Dodoma ukazipanga ni kazi kubwa kiasi gani imefanyika? Huyo ndiye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tunayemzungumzia na ndiyo maana watu wanamlaumu Tundu Lissu kwa kukimbia uchaguzi, hata wewe ungekuwa Tundu Lissu ungekimbia, hata mimi ningekuwa Tundu Lissu ningekimbia.

Ningefanya *drama* zote ambazo Tundu Lissu anafanya na wale wote wanaomwonea huruma tungefanya hizo *drama* kwa sababu hamna namna nyingine ya mwanasiasa kukimbia zaidi ya kutengeneza *drama* na uzuri wake mimi nimeshakaa huko kila nikiwatazama ninajua hii ni *drama,* mimi ninajua hii ni *drama. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo huyu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Rais ambaye ameifanya leo Tanzania siyo tu kwamba amewekeza ndani ya sekta ya afya ikatatua matatizo ya afya yaliyoko ndani ya Tanzania, alichowekeza kimebubujika na kikaenda kwenye mataifa mengine leo tunapozungumza hapa mataifa 15 yanaleta wagonjwa ndani ya Tanzania kutibiwa. Maana yake ni nini? Uwekezaji wa Dkt. Samia kwenye sekta ya afya haujagusa tu sekta ya afya ndani ya Tanzania, umewapunguzia gharama nchi kumi na tano zinatotuzunguka sasa wanakuja hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Tundu Lissu akiangalia vyombo vya habari CHADEMA na wapinzani wengine wakiangalia wanakuta watu kule Comoro, wanakuta watu kule Zambia na kwingine wanapanga foleni wanawasikiliza madaktari wetu. Wakirudi huku ambao hawatatibiwa na teknolojia iliyopo huko wanaletwa ndani ya Tanzania wanakuja kutibiwa. Wakiangalia hayo wanafikiria na *impact* ya kutoka taifani mpaka inapofika kijijini na wanachokijua Watanzania wanaona kwenye huu mchezo hatuwezi kuingia, wanaamua kukimbia na ndiyo maana unaona hata kuna wengine ambao ni Wana-CCM wenzetu wameanza kuugua ugonjwa wa kifafa, wanakimbiakimbia na kusema mambo mengi ambayo wanataka kutuvuruga, sitaki kutaja majina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninataka kuwaambia, shetani ukivaa kola ya madhabahuni, ukifanya mambo ya kishetani tutakufuata madhabahuni, utanyooshwa na utawekwa sawa ili kuhakikisha nchi yetu inaendelea kubaki kuwa salama. Mambo ya msingi kama haya makubwa ambayo Rais wetu anayazungumzia

hatutaki mtu yeyote kusahaulisha Watanzania mambo makubwa yaliyofanyika. Leo katika hii nchi yetu ya Tanzania ilikuwa ukitaka kutibiwa bila kufungua kifua inabidi uende India, Ulaya au Marekani; leo unatibiwa ndani ya Tanzania na siyo sisi tu tunatibiwa ndani ya Tanzania wanakuja majirani zetu wa nchi zingine wanakuja kutibiwa ndani ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Tanzania hii tunaambiwa watu wanapata matatizo mbalimbali ya ubongo wanayotakiwa wafunguliwe ubongo, lakini leo ndani ya Tanzania hii kwa kutumia tu mawimbi ya sauti mtu anatibiwa bila kupasuliwa ubongo. Huyo ndiyo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tunayemzungumzia na ndiyo maana tunasema kwa wivu mkubwa Watanzania wanaungana. Ndiyo maana wenzetu walipoona kwamba wakiingia kwenye uchaguzi wanaenda kuvunja rekodi ambayo haijawahi kuvunjwa na CHADEMA katika kushindwa, wakaona hawako tayari kuvunja hiyo rekodi, wameanza *comedy* na kuzunguka kwenye maeneo mbalimbali nchi hii kudanganya na Watanzania wanajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunakaa hapa kuna watu kutoka nchi za mbalimbali, kwenye mwaka huu tu zaidi ya watu 12,180 wametibiwa. Leo tunakaa hapa watu 2,770 wamefuatwa nchini kwao na madaktari wetu, watu wakiangalia wanaona *Samia Aid* inakuja watu wa nchi nyingine ndani ya nchi yao wanapanga foleni kutibiwa na madaktari wa Tanzania waliotumwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ndani ya *Benjamin Mkapa Hospital* ya kwetu hapa kuna magari ambayo ni hospitali kamili inatembea hapa na zimekwenda Burundi, zimekwenda nchi jirani wamekwenda na wakienda wakipaki gari la Mheshimiwa Dkt. Samia na limeandikwa *Dr. Samia Service* limekaa hapo watu wa Taifa lingine wanakuja wanapanga mstari wanapokea huduma kutoka kwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hayo ndiyo tunataka dunia ijue kwamba Rais huyu tu siyo kwamba ameleta

suluhu za afya ndani ya Tanzania, ameleta suluhu za afya kwa Afrika Mashariki na Kati na majirani zetu waliotuzunguka… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mollel, ahsante sana…

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimalizie kwa kuwaomba wananchi wa Peramiho kwamba hili jembe tumeanza ku-*enjoy* utamu wake waendelee kutuletea kwa sababu tunampenda sana na watumishi wa afya watafurahi sana, ni mtu mwenye *emotional intelligence* ya kutisha tena ya kuzaliwa nayo, siyo ya kusomea darasani ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel. Nimwite sasa mtoa hoja, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama aweze kujibu hoja za wachangiaji na kuhitimisha hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa tena fursa ya kuja kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuweza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge kwa sababu na minajali ya muda ambao nimepewa, hoja zenu ambazo kwa bahati mbaya ama kwa namna moja ama nyingine tutashindwa kuzifikia ninaomba mridhie tutazijibu kwa maandishi na tutaziwasilisha kwenu kabla Bunge hili halijahitimishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa dhati ya moyo wangu niinue moyo tena wa shukrani kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya katika nchi yetu na kwa sekta zote ikiwemo sekta hii ya afya. Tuko katika kipindi ambacho kwangu mimi Waziri wa Afya baada ya kupata jukumu la

kumsaidia Mheshimiwa Rais nimeona katika sekta ya afya ulimwenguni tunapita katika mabadiliko na mageuzi makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulimwengu huu kwa sasa tuko katika karne ya 21. Sasa katika karne hii ya 21 ukiangalia na Mheshimiwa Waziri kaka yangu Profesa Kitila amekuwa akisema sana haya, kwenye karne hii ya 21 mabadiliko ya uchumi yamekwenda kwa kasi na ukisoma taarifa mbalimbali katika majalada mbalimbali ni kama vile *GDP* katika nchi ama ulimwengu mzima imeongezeka karibu mara tatu ya viwango ambavyo vilikuwa huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maendeleo haya na ongezeko la uchumi kukua kwa *GDP* katika nchi mbalimbali kuna maanisha nini katika sekta ya afya? Kunamaanisha mambo yafuatayo:- *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza upande mmoja maendeleo haya yanaendana na mabadiliko makubwa ya sayansi na teknolojia katika ulimwengu wote. Sasa mabadiliko ya sayansi na teknolojia ni *favour* kubwa katika maendeleo ya sekta ya afya ulimwenguni.

Vilevile, maendeleo haya ambayo tunasema *GDP* imeongezeka, uchumi umekuwa katika ulimwengu mzima yanatupelekea kuongeza shughuli zinazoendana na maisha ya kila siku ya binadamu. Miji yetu imekuwa mikubwa sana na *population* katika miji yetu imeongezeka. Pamoja na kuongezeka kwa *population* kwenye miji yetu, maisha ambayo tuliyazoea huko nyuma yamebadilika, kwa hiyo, mila, desturi na tamaduni za ulimwengu kwenye mataifa mbalimbali zimebadilika kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu sasa wanaishi kwa kimitizamo ya miji zaidi, ninataka kusema nini, baada ya kubadilika kwa mila, desturi, tamaduni zetu za maisha huko nyuma hapo ndipo tunakutana na tabia za wananchi na za jamii ambazo zimepoteza

asilia yake na kujiingiza kwenye mageuzi haya makubwa ambayo yaendana na mtazamo wa kiuchumi kwa sasa na ndiyo watu wengi wamesema na mdogo wangu Mheshimiwa Esther hapa amesema. Kwa hiyo, hata zile tabia bwete za kutokufanya mazoezi ni kwa sababu ya mabadiliko haya ya kiuchumi, mitazamo ya kimaisha na namna tunavyoishi kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wa mazingira, ni kwa sababu ya ongezeko la watu, lakini mabadiliko ya mtazamo mzima wa mwenendo wa maisha ulimwenguni na mabadiliko haya ya kiuchumi. Uwepo wa viwanda hiyo pia ni maendeleo makubwa, lakini kwenye sekta ya afya yanaathari kubwa kwa sababu ongezeko la moshi linaathari kubwa kwa maisha ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukataji wa miti na mazingira unasababisha mwingiliano kati ya binadamu na wanyama na matokeo yake ndiyo haya magonjwa ya mlipuko kama *m-pox*, ebola na mambo mengine ya namna hii haya *marburg*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa tunakabiliana na changamoto za namna moja ama nyingine. Huku tuna maendeleo makubwa, huku tuna maendeleo kweli yanayo-*affect* sekta ya afya, lakini *output* ya hayo maendeleo inaathari pia na inachangia kwa kiasi kikubwa kwenye sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumefika katika ulimwengu ambao maendeleo hayo ya kisayansi yanatuambia sasa hivi sayansi ndiyo afya na afya ni sayansi. Bila sayansi hakuna afya na bila afya hakuna sayansi, ndipo mahali ambapo tumefika kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tupo tena kwenye hali ambayo ni lazima hata sisi kama Watanzania na nitasema hapa karibuni wakati ninapitia majibu ya maswali yenu. Tunasema maendeleo haya ya sayansi ni mabadiliko ya teknolojia na vifaa tiba na namna ya uchunguzi kwenye magonjwa. Kukua kwa hii sayansi uwepo wa chanjo ili kufanya *prevention* ya magonjwa tunayoyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine yapo makundi ambayo hayaamini pia katika maendeleo haya ya sayansi na teknolojia katika vifaatiba na chanjo ambazo zinatumika katika ulimwengu kwa sasa. Tuna kazi kubwa na ninaomba niseme katika Taifa letu la Tanzania kama tusingekuwa na daktari bingwa mbobezi *number one* Dkt. Samia Suluhu Hassan, mwenendo huu wa ulimwengu kwenye sekta ya afya tungeweza kujikuta tupo mahali ambapo panatutatanisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati ya moyo wangu ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sifa alizonazo ambazo zimesaidia sekta ya afya kuendelea kuwa himilivu kukua na kufika katika viwango ambavyo leo Waheshimiwa Wabunge ninawapongeza sana kwa kutambua mchango huo mkubwa wa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais huyu ana maono makubwa kwenye sekta ya afya, makubwa sana. Mheshimiwa Rais huyu amefanya maamuzi mazito tena yenye uthubutu mkubwa katika kuleta ustawi wa afya za wananchi. Mnakumbuka wakati wa *Covid* alipofanya maamuzi ya kuhakikisha Watanzania tunachanjwa ili tuweze kuokoa maisha yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ana vipaumbele katika sekta ya afya nami wakati ninawasilisha hotuba yangu nimewaambia vile vipaumbele kumi. Vipaumbele vyote vile kumi vinajibu hoja za Waheshimiwa Wabunge ambazo zimesemwa hapa na kipekee ninamshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati yangu na Wajumbe wa Kamati kwa kazi kubwa waliyoifanya. Hivi vipaumbele tumevifikia kwa sababu ya maono ya Mheshimiwa Rais na ushauri mkubwa tulioupata kwenye Kamati yetu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI. Kwa hiyo, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwahakikishie Mheshimiwa Rais ni jasiri katika kuhakikisha maamuzi tunayoyafanya kwenye sekta ya afya yanaleta ustawi ndani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yaliyozugumzwa leo na Wabunge yanagusa maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza, ni jinsi Taifa letu lilivyojikuta kwa sasa na siyo sisi peke yetu kwa sababu siyo kisiwa, ulimwengu wote, magonjwa yasiyoambukiza yameendelea kuongezeka kwa kiasi kikubwa. Kila mahali utakutana na kesi hizi kwa mtazamo mmoja ama mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia eneo la pili; ni magonjwa ya mlipuko ambayo nimesema yanatokana na mageuzi haya ya ndani ya ulimwengu yanayosababisha pia uharibifu wa mazingira, tabia ya nchi kubadilika, mienendo, mitizamo, tamaduni na desturi zetu kuwa zimebadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo pia magonjwa yasiyopewa kipaumbele. Nimesema hapa wapo Watanzania ambao wameokolewa vifo kutokana na magonjwa yasiyopewa kipaumbele kama mabusha, matende na magonjwa mengine ya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile yapo magonjwa yale yanayoambukiza na Mheshimiwa Shigongo ameeleza sana kuhusu masuala ya *Hepatitis B,* lakini tumezungumza masuala ya *HIV,* ya *TB* na masuala ya malaria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba bajeti ambayo Mheshimiwa Rais na Bunge lako tukufu itakapoipitisha leo ambayo tumeomba shilingi 1,618,191,235,000 itakwenda kujibu hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge mlitupatia katika michango yenu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza, Waheshimiwa Wabunge mmezungumza sana kuhusu kiwango kidogo cha utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo katika sekta ya afya. Waheshimiwa Wabunge, tunalipokea jambo hili kwa mikono miwili na tutakwenda kulifanyia kazi, lakini ninaomba muungane na mimi kukubali kwamba Mheshimiwa Rais wetu huyu jemedari na mimi ndio ninasema yeye ndio daktari bingwa na mbobezi. Katika kipindi kifupi cha miaka minne amefanya mageuzi makubwa sana ya kuhakikisha fedha na rasilimali katika sekta ya afya zinapatikana. Sisi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mifano michache; mwaka 2015/2016 bajeti yetu na hasa katika eneo la maendeleo ilikuwa ni shilingi bilioni 8.3; mwaka 2021/2022 ilikuwa ni shilingi bilioni 278.4. Waheshimiwa Wabunge, mwaka 2024/2025 bajeti imefika shilingi bilioni 501.1. Kwa hiyo, ni lazima tuone nia, dhamira na utashi wa kisiasa wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha anaimarisha sekta hii ya afya na ninaomba tumpigie makofi mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, nitazungumza vizuri hapo mbele kama muda utanitosha. Hapa katikati tumepata mabadiliko ya sera za kimataifa kuhusu uchangiaji wa gharama kwenye sekta ya afya.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwaambie zipo nchi zimetetereka baada ya mabadiliko hayo ya kisera ya kimataifa. Hata dawa kwa ajili ya kuhudumia magojwa msonge ikiwemo *HIV, TB,* Malaria pamoja na hata hii *Hepatitis.* Dawa hizo ni tatizo, lakini wakati ninasoma hotuba yangu jana nimewaambia Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ilijipanga na ikaja kujipanga tena na imetoa na fedha nyingine, tuna uhakika na dawa hizi mpaka mwaka 2026 bila kutetereka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kweli ipo baadhi ya miradi fedha hazijapatikana, lakini unapokuwa na bunduki unataka

kuua adui, unaweza utumie risasi moja ikafanikiwa, unaweza kutumia zaidi ya risasi mbili ama tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye sekta ya afya ili kufanya isimame ni mambo mengi na ndiyo maana tunasema ajenda ya *universal health coverage* ukiitazama kama lengo endelevu la kidunia lina mambo mengi ndani yake, ni pamoja na hii miundombinu ambayo mmenikumbusha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninadhani Serikali tupo hapa na ninafurahi kumuona Waziri wa Fedha yupo hapa. Tunaendelea kufanya kazi na Waziri wa Fedha kwa karibu kuhakikisha kila bajeti inapopatikana tutaendelea kuimarisha, lakini tunamshukuru Rais kwa ile miradi ambayo tumeshaikamilisha na ninyi Waheshimiwa Wabunge mmempongeza Rais hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi hiyo tumewaambia ni pamoja na vifaa tiba na tumeeleza ni kwa namna gani tumeweza kununua vifaatiba. Waheshimiwa Wabunge ngoja niwape mfano mmoja, ukiacha mbali hii miundombinu ya ujenzi, tumezungumza sana tatizo la *cancer* (saratani).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwekeza kwenye matibabu ya magonjwa haya ambayo hayaambukizi ni jambo muhimu sana. Ninaomba niwapatie picha tu kidogo, ujenzi wa *bunker* moja ya kuweka mashine ya mionzi kwa ajili ya kutibu saratani unatumia wastani wa shilingi bilioni 5.5 kwa *bunker* moja. Ununuzi wa mashine moja ya kisasa toleo la sasa hivi maarufu kama *LINAC,* mashine hiyo inauzwa shilingi bilioni 7.8 kwa mashine moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ununuzi wa mashine nyingine ambayo ni maarufu kwa jina la *COBAT* yenyewe siyo chini ya shilingi bilioni 1.9. Hata hivyo ukiangalia *CT-Scan the same 1.8 billion shillings.* Ukiangalia ile *PET scan machine* niliyowaambia iliyofungwa pale *Ocean Road* ni shilingi bilioni 18.8. Ndiyo maana sisi kwa *East Africa* ni nchi mbili tu tumeweza kuwa na hiyo mashine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *MRI* ni zaidi ya shilingi bilioni 2.8; ninataka kusema nini Waheshimiwa Wabunge? Mmeona na mmeshuhudia dhamira ya Mheshimiwa Rais kuwekeza kwenye majengo, mmeona tumefika zaidi ya miundombinu ya kutolea huduma za afya zaidi ya 12,000. Kwa hiyo, tutaendelea kukamilisha majengo hayo yaliyobakia na tutaendelea kuweka vifaa hivi vinavyotumia teknolojia ya kisasa na hali ya juu. Afya kwa Rais wetu ni jambo namba moja ili kuokoa maisha ya wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumza Waheshimiwa Wabunge suala la ukosefu wa rasilimali watu. Ninamuona hapa Mheshimiwa Waziri mwenzangu wa Utumishi yupo hapa. Tunajadiliana kila siku tunatokaje? Mheshimiwa Profesa Muhongo ame-*provide data* hapa jana nzuri za kutosha za namna ambavyo tunatakiwa kuendana na mikataba ya kimataifa. Ile *rationale* kati ya daktari na mgonjwa inatakiwa iweje? Mheshimiwa Profesa ametuambia aidha daktari mmoja kwa wagonjwa 4,000, aidha daktari mmoja kwa wagonjwa 1,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme kupitia mashirikiano na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora jambo hili tumewaeleza, kwenye taarifa zetu tumepambana na leo tunahesbu watumishi 171,711. Tumepunguza *gap,* lakini tunakubali kwamba tunatakiwa kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwape tu taarifa ndogo Waheshimiwa Wabunge, sisi kwa mujibu wa taarifa ambazo tumeshirikiana na taasisi na mabaraza ambayo yapo ndani ya sekta ya afya nchini, uwiano wa daktari bingwa kwa sasa umefikia moja kwa 4,000, lakini zipo nchi zinazotuzunguka na sitataka kuzitaja, wenzetu bado wapo kwa daktari mmoja kwa wagonjwa 25,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa ni lazima tuone Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa ya kupunguza tatizo hili la watumishi na kama tungepata nafasi ya kutosha Mheshimiwa Waziri

wa Utumishi angetoa maelezo hapa, hakika Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuna kila sababu ya kumpongeza, lakini tunapokea hiyo changamoto, ni lazima tuendelee kuongeza watumishi kadri inavyowekezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmeniambia na Profesa alisema tunatakiwa kuwa na wataalam wa *Telemedicine, Teleradiology* na *Eco*. Ninakubali kabisa na ninamkubalia Mheshimiwa Profesa Muhongo, Mbunge mbobezi kwa mchango wake na ninaomba niseme yafuatayo; kwa idadi ndogo hii ya watumishi ni nini ambacho tumekifanya ndani ya Wizara kwa kushirikiana na wenzetu wa Utumishi. Kwanza tulichoamua, nimesema ndani ya utangulizi, ni lazima twende katika mifumo ya uwekezaji wa sekta ya afya unaotumia sayansi na teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukiweza kufika madaktari bingwa bobezi labda niseme tukifika madaktari 10,000 lakini tukawa na mifumo mizuri ya *telemedicine* ina maana madaktari wale wana uwezo wa kutusaidia kuwasiliana na vituo vyetu vya afya nchini, zile *referral* ambazo labda zitaanzia kwenye ngazi ya wilaya kuja kwenye ngazi ya mkoa na ukamuweka mtaalam kwenye ngazi ya mkoa akawasiliana na wataalam waliopo kwenye kata, zahanati kama mtu amefanyiwa kipimo labda cha *CT-scan*, *x-ray* ama *ultrasound.* Kwa uchache huo huo wa wataalam tukienda kwenye sayansi ya teknolojia ya sasa na hasa *artificial intelligence* na tukaendelea kusimama kwenye *telemedicine*. Wakati tunaelekea katika matakwa hayo mengine ya kimataifa, lakini tutakuwa tumeokoa maisha ya Watanzania wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mtu anapata kipimo cha *x-ray* wakati yupo kwenye Hospitali ya Kanda labda Mbeya, anakwenda likizo kwa mume wake Dar es Salaam, anapata ugonjwa au shida kiafya anaenda labda pale *MOI* kupatiwa matibabu, lakini kwa sababu hatuna hiyo mifumo inayosomana, anaambiwa aanze tena kufanya vipimo vilevile kwa mara ya pili na kwa gharama hizo hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hatuwezi kuvuka wala kufika, ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais na ninaomba niwaambie kwa Hospitali zote za Kanda na Mwenyekiti wa Kamati amelisema sana. Mifumo yote sasa hivi inasomana na hata leo, jana na juzi tumekutana Hospitali zetu za Rufaa za Mikoa mifumo inasomana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka sasa tuondoke kwenye mifumo kusomana kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa ikasomane kwenye Kanda mpaka Taifa, lakini tushuke mpaka kwenye wilaya na vituo vya afya mpaka kwenye zahanati. Tukiweza kufika hapo tutakuwa tumeitendea haki sana sekta hii ya afya na tutakuwa tumefanikiwa sana kwanza kupunguza gharama za wananchi wa Tanzania katika mfumo mzima wa tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani umetoka Songea umepimwa, unafika Njombe unapimwa, unafika Mbeya unapimwa, unafika Dar es Salaam unapimwa kitu ambacho kingeweza kurahisishwa kwa mifumo kusomana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokea ushauri huu kwa unyenyekevu na ninawahakikishia kwamba ni maelekezo ya Serikali tutapambana usiku na mchana kuhakikisha mifumo inakuwa ni *solution* ya uhaba wa watumishi na kupunguza gharama za matibabu katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea hapa hoja nzito kuhusu *MSD*. Ni lazima tuitazame *MSD* na Waziri wa Fedha nipo naye hapa atakuwa ni shahidi nimefanya naye vikao vingapi, tumekaa kwa ajili ya kuifanya *MSD* ifanye kazi vizuri. *MSD* iliwasilisha maombi ya shilingi bilioni 561.

Waheshimiwa Wabunge, toka *MSD* hii imeanza ni kwa mara ya kwanza mwaka jana (2024) wamepewa shilingi bilioni 100. Ninaposimama hapa ninaomba niwaambie fedha hiyo *whether* ni deni ama mtaji wameshaongezewa shilingi bilioni 50 na mpaka sasa

wana shilingi bilioni 150, ukiacha mbali juhudi zao wanazozifanya za kuwekeza ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ukiachia mtaji na deni Serikali imeendelea kutoa zaidi ya shilingi bilioni 42 kwa ajili ya kujenga maghala ya kuhifadhia bidhaa zetu za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa mwaka huu wa fedha taarifa ya Kamati ilizungumza madeni ya bidhaa msonge ambayo yamezidi kuifanya *MSD* iendelee kunyong'onyea katika utendaji wake. Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imetenga tena shilingi bilioni 48.2 kwa ajili ya ugomboaji wa bidhaa za miradi msonge ili kuifanya *MSD* iendelee kuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iliona hiyo haitoshi, kwa kuwasiliana na wenzetu wa China tunakwenda kupokea fedha ambayo ni *grant* na siyo mkopo wa dola za Kimarekani ambazo ni sana na shilingi bilioni 119 na fedha hizo zitatusaidia pia kuongeza kwa *MSD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo madeni ya TAMISEMI, ninamshukuru Waziri wa TAMISEMI jana wamekutana na *MSD* wameweka utaratibu wa kuyalipa, madeni ambayo yako kwenye Fungu 52 na mimi mwenyewe Waziri wa Fungu 52 tumeshaweka mkataba na taasisi zote zilipe madeni ya *MSD* haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni la *NHIF* ninamshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu - Waziri wa Fedha, tumekubaliana kutoa hati fungani ambayo itasaidia kubeba mzigo huo na taratibu zote zimekamilika. Waziri wa Fedha atakapokuja kwenye bajeti yake hili ni eneo ambalo atalitolea tena ufafanuzi wa kina ili tuweze kuiokoa pia *NHIF*. Lengo la *NHIF* ku-*provide* hiyo fedha kwa ajii ya ustawi wa sekta ya afya lilikuwa zuri, lakini tunaamini kwamba kulikuwa na kila sababu ya kuhakikisha tunalipa hayo madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba bajeti ya mwaka 2025/2026 tunakwenda kuanza Bima ya Afya kwa Wote. Lengo la Bima ya Afya kwa Wote ni nini? Ni kuhakikisha uwekezaji uliofanywa na Serikali yetu kila mwananchi wa Tanzania aweze kunufaika na uwekezaji huo. Akitaka matibabu kwenye wilaya, kwenye mkoa, kwenye *zone*, kwenye taasisi, kwenye hospitali yetu ya Taifa aweze kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umesema vizuri, vifurushi tulivyonavyo vya bima ya afya sivyo vifurushi vya bima ya afya kwa wote. Waheshimiwa Wabunge, kaeni sawa sawa, tutakuja na Bima ya Afya kwa Wote ili iweze kuwasaidia wananchi wote na lengo letu ni kupunguza vifo na kuwafanya wananchi wetu wawe salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli muda ni mfupi lakini ngoja niguseguse tu yote. Mheshimiwa Profesa Muhongo alitu-*challenge* hapa kama tunaangalia mwenendo wetu unaendana na *Sustainable Development Goals* na hasa *goal* namba tatu. Naomba nimhakikishie Profesa tunakwenda sambamba na *goal* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kuiangalia *goal* namba tatu ambayo inahusu sekta ya afya, inatutataka tupunguze vifo vya akinamama na watoto. Waheshimiwa Wabunge, tumpigie makofi Rais, *goal* hiyo vifo vya akinamama na watoto tumevipunguza. Inataka tupunguze vifo vya watoto *under five*, tumetoka 67 mpaka 43. Sasa hapo Waheshimiwa Wabunge kama mmenifuatilia kwenye bajeti yangu, hapo hatujafanya vizuri sana, tumeweza kutengeneza uzazi wa dharura, tumetoa watoto tumeweza kuwaweka pembeni, lakini tunahitaji kuwa na *Neonatal Intensive Care Unit* za kuokoa maisha ya watoto katika vituo vyote vinavyotolea huduma zetu, tumejipanga vituo 100 tutavipa vifaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yangu Mheshimiwa *Engineer* Ulenge alisema jana nakushukuru sana. Hata vile vifaa vya utambuzi

wa kusikia tunakwenda kuvinunua na kuviweka kwenye vituo vyetu hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *goal* hii namba tatu inaendana pia na *goal* namba moja ya kupunguza umaskini. Waziri wa Fedha atakapokuja atawaeleza ni kwa kiasi gani Serikali yetu imeweza kupunguza umaskini. Kwa hiyo, *goal* namba tatu inategemeana na umaskini, *goal* namba moja inategemeana na *goal* namba sita kama nitakumbuka vizuri ya uwepo wa maji safi na salama. Kwa hiyo, jambo hilo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Profesa tunakwenda nalo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepambana kuhusu magonjwa haya yanayoambukiza, nilikuwa nafuatilia mchango wa kaka yangu Mheshimiwa Shigongo. Naomba nimhakikishie kwamba kwa sasa kwa kweli tumeshajitahidi kiasi cha kutosha na tumeshafanya kazi ya kutosha. Homa ya *hepatitis* tumeiingiza kwenye Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Magonjwa Yanayoambukiza. Kwa hiyo, sasa hivi tunakwenda na magonjwa ya ngono, *HIV* na *Hepatitis*. Tunapambana nayo yote kwa pamoja na imetusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, tumetoka uambukizo wa asilimia 4.3 tumefika uambukizo wa asilimia 3.5; tumpongeze sana Mheshimiwa Rais. Nimekwenda kufuatilia kwa kina, *suppliers* wetu ambao wamepewa jukumu la kuleta chanjo la *hepatitis* nchini, kumbe Mheshimiwa Shigongo baada ya kutushauri tulishaachana na ile *monopoly* ya mtu mmoja, sasa hivi wako wanne na wanafanya kazi hiyo na tumeshaanza kuona kuna dalili za bei kuanza kushuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kujipanga na pale ambapo Serikali itakuwa na uwezo, basi tutafanya kazi ya kuwachanja wananchi kwa kuzingatia utaratibu wa chanjo nchini, kwa sababu ya muda, basi ninaomba tu nimwambie Mheshimiwa Mbunge Tabasam habari ya Serengeti tumeipata, lakini nimhakikishie Mbunge Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati tutakwenda

kuangalia uwekezaji uliofanywa na mwekezaji wetu kule Iringa. Nilisema wakati wa hotuba hapa tunawashukuru pia Ubaya Ubwela kupitia *MO Foundation*, naye anatusaidia sana sekta ya afya. Tunashukuru sana Wananchi kupitia *GSM* na wao wanatusaidia sana kwenye sekta ya afya zikiwemo taasisi nyingine za dini, benki zetu na mashirika mbalimbali ambayo yanatusaidia. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi kwa kuwa kengele imenigongea na bado nilikuwa na mambo mengi, lakini tutayaleta yote kwa maandishi. Kwa heshima kubwa ya juhudi iliyofanywa na daktari bingwa mbobezi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ninaomba Waheshimiwa Wabunge tuendelee kumuunga mkono na kumtia moyo kwa kiasi kikubwa kwa jinsi anavyofanya vizuri kwenye sekta ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapotaka kutoa hoja nitaomba pia nije kuleta mabadiliko wakati nahitimisha vifungu vyangu. Nitaleta mabadiliko ya maneno katika hotuba yangu, ile hotuba kuu ambayo niliisoma mbele yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge ninawashukuru sana kwa michango yenu. Ninawaombea kila la kheri kwa Mwenyezi Mungu mwezi wa 11 tukutane sura hivi hivi tukitazamana humu ndani. Niwahakikishie wananchi wa Tanzania, kama tumefaidi huduma za afya ni kwa sababu Wabunge hawa wameupiga mwingi ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tumekwenda kwa hatua hizo kubwa tukiongozwa na Mheshimiwa Rais, bajeti hizi humu ndani Wabunge hawa walizipitisha kwa umakini hawakukataa na ndizo ambazo zimekuja kuleta ustawi wa jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, ninaomba niahidi majibu yote nitayaweka kwenye makaratasi na kuyawasilisha kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na hoja imeungwa mkono. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaenda kwenye hatua nyingine nina majina hapa ya matangazo machache.

Tangazo la kwanza ni wageni ambao wameingia; tunao wageni wa Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo na hawa ni wanafunzi na walimu wa shule kutoka Mbagala Mkoa wa Dar es Salaam ambao wako upande wa kulia na upande wa kushoto. Tuwaone, naomba msimame. Karibuni sana kwenye Bunge letu, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la pili mnataarifiwa ya kwamba kuna Taasisi ya *Devcom Forum Publication* ambayo ipo kwenye Viwanja vya Bunge kwa ajili ya maonesho ya machapisho ya vitabu mbalimbali vya Uongozi wa Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maonesho hayo yanafanyika nyuma ya Ukumbi wa Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa kutembelea na kupata nakala ya vitabu hivyo ambavyo vimeletwa kwa ajili yenu.

Baada ya matangazo hayo mawili sasa tunaendelea.

Katibu.

**NDG. AZIZA MAKWAI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa Mheshimiwa Spika atakuja kuendelea na kikao.

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 52 – Wizara ya Afya**

Kifungu 1001 – *Administration Human Resources Management*..............................Sh. 11,291,233,800

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa muda uliosalia tutapitisha kwa mafungu.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 52 – Wizara ya Afya**

Kifungu 1001 – *Administration Human Resources Management*......................................Sh. 11,291,233,800
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……………Sh. 1,786,793,926
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*……………….Sh. 2,220,234,574
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*…………………………Sh. 913,770,500
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*……..Sh. 415,363,200
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*……...Sh. 1,298,898,900
Kifungu 1007 – *Legal Services Unit*…………………………Sh. 555,273,048
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*……………………………Sh. 885,193,206
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*…………Sh. 622,044,800
Kifungu 2001 – *Curative Services*……………………..Sh. 508,011,218,458
Kifungu 2003 – *Chief Medical Officer*…………………Sh. 24,309,608,877
Kifungu 2004 – *Nursing and Midwifery Services Division*…...................................................Sh. 930,198,003
Kifungu 2005 – *Pharmaceutical Services Unit*…………Sh. 1,381,700,500
Kifungu 2006 – *Diagnostic and Health Care Technology Services Unit*…....…………………….Sh. 11,408,856,607
Kifungu 3001 – *Preventive Services*……………………Sh. 29,526,781,807
Kifungu 3002 – *Health Quality Assurance Division*………Sh. 711,083,700
Kifungu 3003 – *Health Emergency Preparedness Response Unit*……………………………………….....Sh. 701,480,210
Kifungu 3004 – *Reproductive, Maternal & Child Health Division*……..………………………………Sh. 1,518,321,500
Kifungu 4002 – *Social Welfare*……………………………………………Sh. 0
Kifungu 5001 – *Human Resource Development*……Sh. 27,945,080,384

*(Vifungu vililotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 52 – Wizara ya Afya**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*………..……Sh. 45,750,082,816
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……………………….................Sh. 0
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*…………………………..................Sh. 0
Kifungu 2001 – *Curative Services*……………………..Sh. 168,089,880,711
Kifungu 2003 – *Chief Medical Officer*………………..Sh. 265,393,822,569
Kifungu 2004 – *Nursing and Midwifery Services Division*……………Sh. 0
Kifungu 2005 – *Pharmaceutical Services Unit*………Sh. 300,000,000,000

Kifungu 2006 – *Diagnostic and Health Care Technology Services Unit*…….…………Sh. 2,000,000,000
Kifungu 3001 – *Preventive Services*…………………...Sh. 144,474,312,904
Kifungu 3003 – *Health Emergency Preparedness Response Unit*…..…………………………Sh. 2,000,000,000
Kifungu 3004 – *Reproductive, Maternal & Child Health Division*……………………………………Sh. 45,050,000,000
Kifungu 5001 – *Human Resource Development*……Sh. 19,000,000,000

*(Vifungu vililotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc*– KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Mtoa Hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelekezo ya Kiti chako wakati nilipowasilisha hotuba yangu, ninaomba marekebisho ambayo tumekwisha kuyawasilisha kwa Katibu wa Bunge kuhusu ukurasa wa 16, kifungu cha 24, kichwa cha habari kitabadilika kwa kuzingatia maelezo mapya ambayo nimekwisha kuyawasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, maadam umesema yameshafika kwa Katibu wa Bunge, endelea nitayatazama.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake. Naomba sasa Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji, Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Afya kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Wote mmeafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwahoji sasa nitangaze rasmi kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 yamepitishwa rasmi na Bunge.

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hivyo nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wanayoifanya, pia kwa ushirikiano mzuri ambao wanao kwa Kamati yetu ya Bunge na tuwatakie kila la kheri katika utekelezaji wa yale ambayo mmeyaahidi katika hotuba yenu. *(Makofi)*

Pia ninatumia fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wetu wa Kamati yetu ya Bunge, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kuendelea kuisimamia Wizara hii vizuri, tunawashukuru sana. Waheshimiwa Wabunge wengi zaidi ya hao ambao ni Wajumbe wa Kamati, mmepata nafasi ya kutoa ushauri wenu ambao Mheshimiwa Waziri kama alivyokuwa anahitimisha hapa Serikali imeupokea, pia katika maeneo ambayo mmeuliza pengine na hoja zenu hazijaweza kujibiwa wakati akihitimisha kwa sababu ya muda basi mtapata majibu. Kwa hiyo, nanyi pia kwa ujumla wenu ahsanteni sana kwa ushiriki wenu katika kuhakikisha jambo hili linakwenda vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, marekebisho ambayo yalikuwa yametakiwa kufanyika jana yameshafanywa na nimeletewa hapa kitabu kipya tayari ambacho kinayo hayo marekebisho. Kulikuwa na neno nadhani ama maneno mawili yamesahaulika, kwa hivyo yalisababisha maana iwe haieleweki.

Waheshimiwa Wabunge, awali kitabu kilikuwa kinasoma ukurasa wa 16, "Kuimarika kwa Magonjwa ya Milipuko na Huduma za Dharura." Sasa kitabu kitasoma, "Kuimarika kwa Udhibiti wa Magonjwa ya Milipuko na Huduma za Dharura." Kwa hiyo, hapo yataongezeka maneno; "Kwa Udhibiti wa Magonjwa ya Dharura," naomba isomeke; "Kuimarika kwa udhibiti wa Magonjwa ya Milipuko na Huduma za Dharura."

Haya ngoja niwasomee kitabu kinavyosomeka; "Kuimarika kwa Udhibiti wa Magonjwa ya Milipuko na Huduma za Dharura." Kwa hiyo, marekebisho hayo yameshafanyika na Waheshimiwa Wabunge kwa sababu hotuba hii ilikuwa imewekwa pia kwenye vishikwambi vyenu, yatafanywa marekebisho kisha itawekwa hii sasa, kama Mbunge anataka kuendelea kujisomea, basi atakuwa anasoma ile ambayo ina kichwa cha habari ambacho kiko sahihi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo pia ninawashukuru kwa uvumilivu, tumevuta muda kidogo, lakini wote mko hapa ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 7.39 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 4 Juni, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*